ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake

41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim Katibu wa Baraza la Wawakilishi.

Kikao cha Ishirini na Saba – Tarehe 24 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezanni Taarifa juu ya hitilafu za kiufundi kwa Vyommbo vya Baharini siku za hivi karibuni.

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Taarifa ya Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano juu ya hitilafu za kiufundi kwa Vyombo vya Baharini siku za hivi karibuni. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha menzani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2011/2012. naomba kuwasilisha.

Mhe. Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mezangi maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea na kauli za mawaziri naomba nitoe taarifa mbili. Waheshimiwa Wajumbe mtakumbuka kwamba tuligawiwa madodoso *questioner,* yale ambayo yanahusu kuhusu suala zima la utawala bora, ambapo madodoso hayo yalitegemewa yawe yameshajazwa na Waheshimiwa Wajumbe wote na kurejeshwa kupitia kwa Katibu tangu tarehe 15 mwezi huu. Leo ni tarehe 24 kama siku tisa hivi zimeshapita. Tunaombwa basi Waheshimiwa Wajumbe, wale ambao hawajawasilisha madodoso hayo kupitia kwa katibu wamalize kufanya hivyo ikiwezekana leo yapatikane yote.
Waheshimiwa Wajumbe kama kawaida siku hizi vijana wamehamasika sana kuja kuona shughuli zetu tunavyoziendesha, kama vile mnavyopata salamu

nyingi sana kutoka kwa wananchi na tumshukuru sana Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwamba wananchi wanatuangalia na wanafuatilia kwa karibu sana nini ambacho wawakilishi wa wananchi wanawafanyia. Kwa hivyo, kwa leo kuna vijana wa *group* inayoitwa, *Zanzibar Initiative for Use* inatoka hapa Chukwani Zanzibar. Mheshimiwa vijana wako hawa naomba niwakaribishe sana kwa kusimama pale walipo ili wawasalimie Waheshimiwa Wajumbe. Hawa ni wageni maalum wanaotoka jimbo hili hapa tulipo, Wahehishimiwa Wajumbe nakushukuruni kwa kupokea taarifa hizo mbili pamoja na vijana wetu. Tunaendelea.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru na samahani sana, ulizungumza suala la dodoso lililosambazwa, wengi tumeipitia ile dodoso lakini kwa maoni yangu haikidhi kuwa dodoso ambayo haiko *bias*, ina mapungufu mengi. Kwa sababu dodoso ni *questioner* unataka maoni ukaifanyie kazi, humuulizi mtu jina lako, unakaa wapi, uko chama gani, una nini. Kwa hivyo, mimi niko tayari najitolea nikae naye mwenye dodoso nimuoneshe mapungufu yake airekebishe halafu tutaijaza. Ahsante.

Mhe. Spika: Nafikiri ni jambo zuri hata hayo mapungufu kama kuna *page* ambayo unaweza ukaonesha mapungufu hayo mimi nadhani tuelekeze tu, na kama alivyoshauri Mhe. Waziri, Dkt. Mwinyihaji basi katibu atawaelekeza dodoso hilo linaongozwa na nani ili tuweze kumfahamisha na labda kama kuna maoni ya mambo ambayo yangepaswa kuwemo na mambo ambayo hayapaswi kuwemo kama alivyoshauri basi tutafanya hivyo. Ndugu makatibu hapo mtawaelekeza Waheshimiwa Wajumbe waweze kuonana na hawa walioleta madodoso hayo. Tunaendelea.

KAULI ZA MAWAZIRI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ifuatayo ni Taarifa yangu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Zanzibar juu ya Hitilafu za Kiufundi kwa Vyombo vya Baharini Siku za Hivi Karibuni.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini imekuwa ikipokea taarifa mbali mbali kuhusiana na masuala ya usafiri na mwenendo mzima wa vyombo vya baharini. Taafira hizi zimekuwa zikifatiliwa kwa karibu sana na wizara yangu kupitia redio na magazeti. Hata hivyo, wizara imejitahidi kuzihakiki na kugundua kwamba nyingi ya taarifa hizo zinazotolewa na vyombo vya habari kuhusu hali ya usafiri wa vyombo vya baharini zinakuwa na utata. Hivyo basi, inapelekea

kuleta tafsiri nyengine kwa jamii yetu na zinasababisha taharuki kwa jamii na hata kwa serikali.

Kutokana na mabadiliko ya hali hewa katika kipindi hiki, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilitoa indhari ya utabiri wa hewa kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar. Hivyo, indari hiyo ilikusudiwa kuelimisha wenye vyombo vyote vya baharini, ili kujiweka tayari na hali ya hewa hiyo ya hatari pindipo ikitokezea. Aidha, indhari hiyo kwa kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar ilikuwa vile vile ni kwa ajili ya kutanabahisha wasafiri baina ya Unguja na Pemba na Unguja na Dar es Salaam.

Mhe. Spika, mnamo Tarehe 7/07/2011, Meli ya Buraq 1, ilifanya safari ya kuondoka Mkoani Pemba kuja Unguja saa moja na nusu ya usiku kama ilivyo kawaida. Kwenye saa mbili na nusu za usiku wakati meli hiyo iko maeneo ya Matumbilini ulitokezea upepo mkali wa kusi na kusababisha mwendo wa meli kupungua kwa kiasi kikubwa na kusababisha meli hiyo kuchelewa kufika Unguja. Taarifa zinasema kwamba meli iliyokuwa inakwenda kwa *knots* nane yaani maili za baharini nane kwa saa, ilipungua mwendo wake hadi kufikia *knot* moja, yaani maili moja ya baharini kwa saa. Hata hivyo, meli hiyo ilifika Unguja saa tano za asubuhi siku ya pili ya tarehe 8/07/2011 salama na abiria wote walifika salama.

Mnamo tarehe 14/07/2011 Meli ya Buraq 1, wakati ikifanya safari zake za kawaida iliondoka Mkoani, Pemba saa moja na nusu za usiku na wakati ikoo maeneo ya Matumbini upepo mkali wa kusi ulitokea na kusababisha meli kutoendelea na safari yake ya kuja Unguja. Meli ilirejea Mkoani, Pemba kwa kusubiri hali ya hewa kuwa ya kawaida. Siku ya pili tarehe 15/07/2011 meli hiyo iliomdoka Mkoani, Pemba kurudi Unguja saa sita za usiku na kufika Unguja saa sita mchana salama na abiria wote walifika salama.

Meli nyengine ambayo hivi karibuni ilipata matatizo ya kiufundi ni ile ya Serengeti ambao ilielezwa na vyombo vya habari kuwa abiria wamenusurika kufa kwa sababu ya hitilafu ya mashine moja iliyoendesha meli. Ukweli wa tukio hilo nikama ifuatavyo:

Siku ya tarehe 14/07/2011 Meli ya Serengeti iliondoka Unguja kama kawaida yake saa tatu na nusu za usiku kuelekea Mkoani, Pemba. Kwenye nyakati za saa tisa na nusu za usiku siku ya tarehe 15/07/2011, mashine ya kuendeshea meli ya upande wa kushoto (*port engine*) ilipata hitilafu ya kiufundi na kusababisha meli hiyo kutumia mashine moja tu, ya upande wa kulia (*star boat engine*). Hali hiyo ilisababisha mwendo wake kupungua kwa kiasi kikubwa na kufika Mkoani, Pemba sasa nne na nusu za asubuhi. Chombo kilifika salama na abiria wote walifika salama. Meli hiyo haikuruhusiwa kuchukua abiria na iliondoka Mkoani, Pemba kurudi Unguja siku ya tarehe 16/07/2011 kwenye saa

tisa na nusu za jioni na kufika Unguja saa moja na nusu za asubuhi siku ya tarehe 17. meli ilifika salama na wafanyakazi wote walifika salama. Hivi sasa meli hiyo inafanyiwa matengenezo hapa Unguja na haitaruhusiwa kufanya safari zake mpaka itakapokaguliwa na kufanyiwa majaribio na wakaguzi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini.

Mhe. Spika, meli nyengine iliyopata hitilafu ya kiufundi ni ile ya Kilimanjaro 2, siku ya tarehe 18/07/2011. Meli hiyo iliondoka Unguja kuelekea Dar es Salaam kama kawaida yake nyakati za saa moja asubuhi na baada ya kupita maeneo ya Chumbe nyakati za saa mbili za asubuhi ilipata hitilafu ya kiufundi na kusababisha mwendo wake kupungua kwa kiasi kikubwa na kusababisha kuchelewa kufika. Kilimanjaro 2 ilifika Dar es Salaam saa tano na nusu badala ya saa tatu za asubuhi, chombo hicho kilifika salama na abiria wote walifika salama. Baada ya kufika Dar es Salaam meli hiyo ilifanyiwa matengenezo na kuridhiwa na SUMATRA, Mamlaka ya Udhibiti wa Vyombo vya Baharini na Nchi Kavu ya Tanzania Bara na Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar ilijuilishwa na SUMATRA kuhusiana na suala hilo la kuridhiwa.

Mhe. Spika, naomba kuwasihi watendaji wa vyombo vya habari kushirikiana na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar katika kuelimisha jamii pindi tu panapotokezea kasoro za vyombo baharini ili kuepusha mgongano wa taarifa zilizokuwa si zakweli, taarifa ambazo zinasababisha tafrani kubwa, taharuki kwa jamaa za wanaosafiri, waliomo vyomboni na kwa Zanzibar nzima.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri Baharini inawaomba na kuwasihi wamiliki na manahodha wa vyombo kutoa taarifa kwa Mamlaka hiyo mara tu, tukio hilo linapotokea na taarifa ya maandishi kutolewa si zaidi ya masaa 48 tokea tukio hilo lilipotokea kama kifungu Nam. 138 ya Kanuni za Usalama za mwaka 2009 kinavyoeleza.

Mhe. Spika, naomba kutoa pole kwa wote wale ambao walipata athari na usumbufu kutokana na tarifa hizo. Aidha, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu na wananchi wote wa Zanzibar, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia Mamlaka yake ya Usafiri wa Baharini wanachukua hatua zote za kiusalama wa vyombo vya usafiri baharini kabla vyombo hivyo havijafanya safari zake. Aidha, tutaendelea kuchukua hatua zote za kiusalama kwa vyombo vyote vinavyofanya safari hizo na huduma hiyo ya kusafirisha wananchi ikiwemo kuvikagua na kuvithibitisha juu ya safari zake hizo.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatoa taarifa kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri baharini hapa Zanzibar, kwamba Chelezo cha Shirika la Bandari kilichopo Malindi kinaweza kutumika kufanyia matengenezo ya vyombo hivyo badala ya vyombo hivyo kupelekwa chelezoni Mombasa. Wamiliki wanatakiwa kuleta mafundi au wataalamu na vifaa tu,

kuna kuifanyia matengenezo hayo, jambo ambalo linapunguza gharama na muda wa matengenezo kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na utaratibu wa sasa wa vyombo hivyo kupelekwa chelezoni Mombasa moja kwa moja. Hivi sasa Meli ya M.S. Sepideh iko chelezoni Malindi kwa matengenezo kwa utaratibu huo tulioueleza na tunaamini kwamba meli hiyo itafanyiwa matengenezo yanayoridhisha na hivi sasa kazi hii inaendelea vizuri.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe hiyo ndio taarifa kuhusu vyombo vya usafiri baharini kama ilivyo chini ya kanuni ya 43 kifungu kidogo cha 3 sasa tunaweza tukauliza maswali kama yapo ili kuweza kufafanua zaidi. Samahani, nimkaribishe Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kutoa maoni ya upande wa kamati hiyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman (Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Nakushukuru Mhe. Spika, na Wawakilishi wako tuko macho kutetea haki zetu. Kwa hivyo, ukisahau tutakukumbusha Mhe. Spika.

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na uzima na kuweka *toufiq* ya kuzungumza Houba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu taarifa ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano juu ya hitilafu za Kiufundi kwa Vyombo vya Baharini siku za hivi karibuni.

Mhe. Spika, awali ya yote tunapenda kumshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri kwa uamuzi wake wa kuleta mbele ya Baraza lako tukufu taarifa hii muhimu na yenye maslahi kwa wananchi. Kwa kuzingatia kuwepo kwa pengo kubwa la kupashana habari baina ya taasisi za serikali na wananchi, kumekuwepo na umuhimu mkubwa wa kutoa taarifa kama hizi hasa pale yanapojitokeza matatizo yanayowahusu wananchi moja kwa moja.

Mhe. Spika, ni hivi karibuni tu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohammed Shein alitoa wito kwa viongozi wa serikali kutoa taarifa za mambo mbali mbali kwa wananchi kupitia vyombo vya habari wakati wa ziara yake ya Mikoa mitano ya Zanzibar. Kwa uzito wa matatizo yaliyokuwa yakijitokeza katika usafiri wa vyombo vya baharini katika siku za hivi karibuni, ni dhahiri kuwa taarifa hii kwa wawakilishi wa wananchi itavunja ukimya uliopo kwa kuwafahamisha wananchi hali halisi ilivyo na mtazamo wa serikali juu ya matatizo ya vyombo vya usafiri baharini.

Mhe. Spika, kama ilivyonukuliwa katika Taarifa ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, Kanuni za Usalama (*Safety Regulations, 2009*) zinaelekeza na kuwataka wenye vyombo vya baharini na manahodha wao kutoa

taarifa kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini ndani ya saa arobaini na nane tangu kutokea kwa tukio. Kamati yetu inadhani huo ni muda mrefu sana kuwekwa na Kanuni hizo hasa ukizingatia kukua kwa nyenzo za mawasiliano hapa nchini. Kwa mnasaba huo, tunashauri kanuni hiyo ifanyiwe marekebisho na kuwataka wenye vyombo vya baharini kutoa taarifa kwa Mamlaka ndani ya muda mfupi sana baada ya kutokea tatizo lolote baharini ili Mamlaka nayo iweze kutoa msaada haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, kwa kuwa baadhi ya matukio yaliyoelezwa katika taarifa ya Mhe. Waziri hutokana na mabadiliko ya hali ya hewa, Kamati inaishauri Mamlaka ya Usafiri Baharini kuwa na utaratibu wa kudumu wa kupokea na kusambaza taarifa zinazohusu masuala ya hali ya hewa kwa Mamlaka ya Hali Hewa na kuwapa wanaoendesha vyombo vya baharini. Taarifa ya Mhe. Waziri inaeleza kutolewa kwa indhari kwa wenye vyombo vya baharini kuhusu mabadiliko ya hali hewa kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kutokana na kuongezeka vyombo vya habari hapa nchini, ni vyema Mamlaka ikatumia vyombo mbali mbali vya habari kuhusiana na indhari hiyo, pamoja na njia nyengine zitakazofikisha habari kwa wenye vyombo na wasafiri baina ya Unguja, Pemba na Dar es salaam kwa wepesi zaidi.

Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa baadhi ya matukio ya vyombo vya usafiri baharini kukatisha safari zake au kutumia muda mrefu kuliko kawaida katika kufanya safari baina ya Unguja, Pemba na Dar es Salaam ni kutokana na uchakavu wa vyombo vyenyewe hasa kwa vyombo vinavyosafiri baina ya Unguja na Pemba. Kwa mnasaba huo, Kamati yetu inapendekeza mambo mawili. Kwanza, ni haja ya kuongeza kasi ya ukaguzi wa vyombo vya baharini kama ambavyo Sheria Namba 3 ya Mwaka 2009 inayoanzisha Mamlaka ya Usafiri Baharini inavyoelekeza.

Mhe. Spika, Kamati yetu ina wasiwasi mkubwa kama jukumu hili la kisheria kwa Mamlaka linaweza kutekelezeka kwa ufanisi kwa kuzingatia upungufu mkubwa wa watendaji. Wakati wa ziara ya Kamati kwa Mamlaka, Kamati ilielezwa kuwepo kwa wakaguzi wa meli wawili tu na *Safety Officers* wanne tu, ambao wana jukumu la kuzifanyia ukaguzi meli za ndani na zile za nje zinapokuwepo Zanzibar ili kujiridhisha na usalama wake.

Mhe. Spika, ukaguzi wa meli hizo haupaswi kufanywa katika kuzingatia uzima na uwezo wa chombo kufanya safari zake pekee, bali pia ukaguzi huo hauna budi kuangalia kama vyombo vya usafiri baharini vinapakia abiria kwa mujibu wa uwezo wa vyombo hivyo. Vyombo kadhaa vimekuwa vinapakia abiria na mizigo kuliko uwezo halisi wa vyombo husika na hivyo kuhatarisha maisha ya watu endapo litatokea tatizo katika vyombo hivyo. Inawezekana kabisa tatizo ndani ya chombo likawa si kubwa sana kiasi cha kusababisha maafa, lakini ujazaji wa abiria na mizigo kupita kiasi ukasababisha matatizo makubwa zaidi.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuepushe na maafa kama hayo lakini tunapaswa kuchukua tahadhari mapema.

Mhe. Spika, aidha ukaguzi huo hauna budi kuzingatia kuwepo kwa huduma muhimu ndani ya vyombo vya usafiri kama vile vyoo vya kutosha kulingana na idadi ya abiria pamoja na upatikanaji wa maji katika vyoo hivyo. Kutokuwepo kwa huduma hizo kwa kiwango cha kuridhisha, kunaweza kupelekea miripuko ya magonjwa kwa abiria ndani ya vyombo hivyo kutokana na vyombo hivyo kuchukua abiria wengi na wanaokaa ndani ya vyombo hivyo kwa muda mrefu.

Kama njia ya kupunguza matatizo yaliyoelezwa katika taarifa ya Mhe. Waziri na matatizo mengine ambayo yanaweza kujitokeza siku za usoni iwapo tahadhari zaidi isipochuliwa, Wizara haina budi kufanya jitihada kubwa ili kuhakikisha Mamlaka inakuwa na wakaguzi wa kutosha watakaoweza kufanya ukaguzi wa meli zetu ili kuwahakikishia wananchi wanaosafiri na meli hizo usalama wa kutosha. Kwa uzito wake, hatua hii inapaswa kuchukuliwa mapema ili kulinda maisha na usalama wa wananchi.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo Kamati yetu inapendekeza ni kwa serikali kuharakisha mpango wa kununua meli nyengine kubwa na za kisasa hasa kwa safari baina ya Unguja na Pemba, ambapo kumekuwa na matatizo makubwa ya usafiri hususan usafiri wa vyombo vya baharini. Vyombo vingi vinavyofanya safari zake baina ya Unguja na Pemba vinaonekana kuchakaa sana na hivyo kuleta shaka juu ya uwezo wa vyombo hivyo kufanya safari zake kama inavyotarajiwa. Hivyo suluhisho la kudumu ni kwa serikali kuchukua hatua za ununuzi wa meli zitakazofanya safari baina ya Unguja, Pemba na Dar es salaam na kuziba pengo la usafiri lililopo sasa hivi.

Mhe. Spika, hivi sasa Sekta ya Usafiri wa Baharini kwa kiasi kikubwa inaendeshwa kwa kupitia wawekezaji binafsi. Kamati yetu inawapongeza sana wawekezaji hao pamoja na serikali kwa kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji hao kuwekeza katika sekta ya usafiri hapa Zanzibar. Pamoja na umuhimu huo mkubwa kwa wizara na serikali kwa ujumla kuwajengea mazingira mazuri yatakayowawezesha wawekezaji hao kufanya shughuli zao kwa ufanisi mkubwa, la muhimu zaidi kuzingatiwa ni usalama wa maisha ya wananchi wa Zanzibar na wasafiri wengine wa vyombo hivyo. Hivyo Kamati yetu inainasihi wizara kuweka kipaumbele katika suala hilo la usalama wa abiria katika usafiri wa vyombo vya baharini lakini pia usafiri wa anga.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha ahsante.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kpata ufafanuzi juu ya suala hili. Mhe. Spika, kwa kweli tunampongeza waziri kuleta taarifa hii mbele ya Baraza, kwa sababu ni kweli

kwamba katika kipindi cha karibuni ndani ya mwezi huu mmoja wa saba ni matokeo manne yamejitokeza, matokeo ambayo yameiweka jamii katika hali ya taharuki katika masuala mazima ya vyombo vya usafiri.

Mhe. Spika, matatizo haya kwa kweli yanatokana na matatizo mawili makubwa, kwanza tukubali kwamba ni tatizo la serikali kutokuwa na meli, lakini ni tatizo la serikali kuipa nafasi sekta binafsi kuingiza vyombo ambavyo ni chakavu na vyenye usimamizi legelege. Sas akwa matatizo haya mawili mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri kwanza kwa upande wa serikali, kwa sababu suluhu ya suala hili ni lazima serikali kama walivyoanzisha waasisi wetu kwa kuwa na meli, lazima serikali imiliki meli zake na hili tumekuwa tukilisemea kwa kipindi kirefu. Sasa M.V. Maendeleo haipo, M.V. Mapinduzi ndio haipo tena nayo, Ukombozi haipo, sasa tunaiuliza serikali ina mpango gani wa dharura, ina mpango gani wa karibuni wa kuweza kulirekebisha suala hili.

Kwa sababu tulikwenda kwenye Shirika la Meli na wakatwambia kwamba shirika wao wameshafanya mipango yote ya kupata meli serikali ikazuia kwa upande mmoja, lakini wakasema serikali wao wana utaratibu wao wa kuwekeza katika suala kama hili kupitia wafadhili hawa na sekta binafsi. Sasa hivyo serikali ina mpango gani wa muda mfupi kwanza, kwa sababu tunalo tatizo hivi sasa. Watafanyaje ndani ya kipindi cha muda mfupi kutuondoshea tatizo hili, lakini vile vile si vibaya kutueleza kwa muda mrefu serikali ina mpango gani?

Swali langu la pili sera au sheria ya uingizaji wa vyombo hivi Mhe. Waziri atusaidie inasemaje? Hata kwa upande ule wa magari serikali ilifika pahala ikasema tunaruhusu magari yaingie aina hii na kodi zake zitakuwa ni hizi. Sasa kwa upande wa vyombo hivi vya usafiri wa baharini sera inasemaje?

Swali langu la tatu, kwa sababu tuna tatizo na tatizo hili Mwenyezi Mungu atuepushie lakini litaendelea kuwepo, litakapotokea tatizo baharini serikali imejipanga vipi katiak suala la uokozi pindipo hali itatokea ya serikali, mambo yanatokea Matumbilini serikali itachukua hatua gani za kuhakikisha kwamba wana *rescue* abiria pamoja na mali zao?

Lakini la mwisho kabisa kumekuwa na tabia katika hali hii tunayoendelea nayo, vyombo hivi vya makampuni mara kwa mara huahirisha safari na bila ya kuwaambia abiria, kitu ambacho kinasababisha usumbufu mkubwa wa abiria.

Sasa serikali inayasimamiaje makampuni hayo ili kuondosha usumbufu huo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi kumuuliza Mhe. Waziri maswali mawili madogo tu, kwanza napenda kumuuliza Mhe. Waziri anafahamu kwamba pole si dawa kwa Wazanzibari.

Lakini ni bora kutafuta vyombo vya uhakika ambavyo vitaletwa hapa Zanzibar ili kuondosha usumbufu kwa wananchi.

Lakini pili kwa nini Mamlaka ya Hali ya Hewa ya usafiri wa vyombo vya baharini haitoi taarifa mapema ili kusitisha vyombo hivi kuzuia safari zake na kuepusha athari kwa wananchi.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii. Lakini nipongeze sana Kamati ya Mawasiliano ya Ujenzi kwa sababu imechambua na imeeleza hali halisi. Kwa hivyo, mimi nitakuwa na maelezo tu kidogo ya kumuuliza Mhe. Waziri. Mhe. Spika, tunajua kwamba kiumbe ni mzito, wakati akishakuwa na safari yake atataka asafiri tu hajui kama huko mbele kuna hatari.

Je, Mhe. Waziri wakati vinapoondoka hivi vyombo kuna ukaguzi wa aina gani wa kuhakikisha kwamba kweli abiria walioingia katika chombo kile ndio abiria wanaotaka kuingia katika chombo kile.

Lakini jengine zaidi niseme kwamba je, Mhe. Waziri kweli anahakikisha maana yake ni kama katetea sekta yake na hapa tunazungumza jambo ambalo kwa kweli ni kwa maslahi ya wananchi. Maana yake lazima tuseme ukweli, ni vyema Mhe. Waziri angesema ukweli ili kulisaidia Baraza hili tukufu. Lakini je, ni kweli ana vyombo vingapi vya uokozi kama wenzangu walivyosema na kamati ilivyosema kuhakikisha kufuatilia kama tatizo lolote la ajali limetokezea na wingi wa abiria wanaosafiri katika vyombo hivyo na mizigo mingi.

Mhe. Spika, lazima tukubali kwamba sisi Wapemba ndio tulivyo, tukenda twike tukirudi twike, ndio maumbile ya kisiwa na ndio maumbile ya visiwa vyote kwa kweli. Unapotoka pahala pengine kwenda pengine na twike za mizigo lazima unakuwa nazo. Kwa hivyo, ningeliomba Mhe. Waziri kwamba hili suala si la mchezo ni suala linagusa wananchi na maisha yao. Ni vyema kama kuna sheria, kuna taratibu au kama sera zinatumika zimepitwa na wakati, tunamuomba Mhe. Waziri azishughulikie ili tuweze kuzichambua zaidi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi ili nimuulize Mhe. Waziri. Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka kujua utaratibu wa kukagua hivi vyombo ni kila baada ya muda gani wanavikagua. Je, kuna utaratibu wa kushtukiza kwenda kuvikagua hivi vyombo.
Halafu nilikuwa nataka kujua utaratibu wa kupata mawasiliano. Je, kuna mawasiliano wanayoyapata kutoka Idara ya Hali ya Hewa kujua hali ya hewa kwa siku nzima ikoje. Kwa sababu katika ripoti yake hapa ya tarehe 14 inaonesha meli ya *Buraq I* iliondoka Mkoani ikaanza safari, baada ya kufika Matumbilini ikaona upepo wa kusi mkali ikarudi. Sasa mimi nashangaa hapa

kidogo hivyo meli inaweza kuondoka ikaanza safari bila ya kujua taarifa za hali ya hewa huko inakokwenda.

Nafikiri kuna vyombo vinavyotoa taarifa za hali ya hewa. Sasa nilikuwa nataka nijue Mhe. Waziri utaratibu wake ikoje. Maana itoke imekuwa kama jahazi halina hata mawasiliano, likiona upepo mkali anatoa tanga anarudi, lakini hivi vyombo mimi nahisi ni vya kisasa. Naomba Mhe. Waziri atwambie labda hivi vyombo havina hata mawasiliano.

Lakini jengine Mhe. Spika, nilikuwa nataka kuelewa zaidi juu ya ukaguzi wa hivi vyombo unafanyika kila baada ya muda gani. Je, kama hii meli ya Buraq I anasema iliondoka Mkoani kuelekea Unguja saa sita za usiku na kufika saa sita za mchana, nafikiri ni masaa mengi sana haya. Sasa hili tatizo lilikuwa bado ndio ule upepo au hichi chombo chenyewe kinaonekana kilikuwa kibovu.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, nashukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia taarifa ya Mhe. Waziri. Lakini pia nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwa kutuletea taarifa hii ambayo ni muhimu sana kwa taifa letu na wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri alipokuwa anatoa taarifa yake alizungumzia zaidi matatizo ya meli haya kwamba yanasababishwa na hitilafu za kiufundi.

Labda Mhe. Spika, nieleze kwamba pamoja na matatizo ambayo ameeleza Mhe. Waziri katika taarifa yake lakini bado kuna tatizo ambalo wananchi wetu wanalilalamikia kwa muda mrefu sana, tatizo la meli zetu hizi kuongeza abiria kinyume na uwezo wa meli zenyewe. Mhe. Spika, inaonekana kwamba Mhe. Waziri Wizara yake imeshindwa kudhibiti na kutatua tatizo hili.

Mhe. Spika, pamoja na matatizo ambayo ameyataja Mhe. Waziri amejipanga vipi katika kuhakikisha kwamba wizara yake inadhibiti upandaji meli abiria kwa wingi sana.

Lakini jengine Mhe. Spika, meli zetu sasa hivi tumekuwa na utaratibu kwamba meli zinazoingia nchini kwa kuchukua abiria zinakuwa chakavu kwa maana ya kuwa zimeshatumika kule nchini kwao. Je, Mhe. Waziri tatizo hili pia atalitatua vipi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza maswali mawili matatu. Mhe. Spika, nianze kwa kutoa pongezi angalau kwa kupata taarifa ya mambo yalivyotokea bila ya kuelekezwa wizara inachukua hatua gani kuona kuwa haya yanapungua hatua kwa hatua.

Kwa hivyo, katika haya tuliyotoa mimi ningeliomba shirika kwa kupitia wizara litafute njia ya kuona kuwa ajali zinapungua kutokea. Kwanza ni kuhakikisha kuwa vyombo hivyo vibovu tunavyotumia hivi sasa kwa sababu hatuna vyengine ni lazima tutumie vinakuwa katika uangalifu mzuri sana kabla ya kuondoka.

La pili hakuna kitu muhimu kama kudhibiti idadi ya abiria wanaopanda katika hivyo vyombo kwa sababu vyombo ni vibovu na abiria wanaingia kwa wingi bila ya kiwango.

La tatu kwa sababu tuna chelezo na nashukuru kwa kupata chelezo. Ningelimuomba Mhe. Waziri aimarishe chelezo chake kwanza kwa kwenda kuwasomesha watu nje ili tuwe na mafundi wetu wenyewe. Kwa sababu kuna chelezo na kitakuwa kinatumika kwa matengenezo ya meli tofauti. Ningelimuomba Mhe. Waziri hili shirika lijipange wenyewe kwa kujua mafundi wako wapi wa kila fani na vifaa na kadhalika, ili mtu akija pale akipeleka tu chombo chake wakishughulikie, sio aje na mafundi yeye, aje na vifaa yeye, pengine inawezekana akaja na fundi sie na vifaa sivyo kwa sababu ni mtaalam.

La mwisho Mhe. Spika, ni tatizo kubwa ambalo pia linachangia kuingia watu waliokuwa hawana idadi. Kwanza kuna tiketi zinauzwa na watu wanaohusika na kuuza tiketi wenyewe, halafu zikimaliza zile tiketi kuna watu wanaouziwa kwa kutoa pesa mfukoni na halafu kuna tiketi za walanguzi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atafanya vipi kuona kwamba tiketi zinazouzwa ndio idadi ya watu wanaoingia ili kuhakikisha mambo kama haya ya maafa hayatatokea tena.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nadhani maswali au maombi yanarudia mle mle. Kwa hiyo, tumalizie wa mwisho Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mhe. Spika, kwa kuwa Wazanzibari wanaoishi katika kisiwa cha Pemba na kusafiri kutoka Pemba kwenda Tanga wanalipa kodi sawa sawa na wale wanaosafiri kutoka Tanga kuja Unguja na wanaotoka Unguja kwenda Dar es Salaam. Kwa kuwa Mhe. Waziri hakuzungumzia lolote kuhusu Wapemba wanaosafiri kwenda Tanga je, huko si kuwabagua.

La pili kwa kuwa wizara yake hii hii alipokuwa akiongoza Mhe. Pili Khamis alipokuwa Waziri wa Mawasiliano miongoni mwa waasisi hao aliweza kuwarahisishia usafiri wale wasafiri wanaotoka katika visiwa vidogo. Kwa mfano kutoka Fundo kuja Wete ameweka *fibre* ya kisasa na kutoka Makoongwe kuja Mkoani akawawekea *fibre*, pia kutoka Nungwi kuja Mkokotoni akawawekea *fibre*. Sasa je, nil lini Mhe. Waziri wa Wizara hii

atafuata nyayo za waasisi wa nchi hii kwa kuwapatia usafiri wa kisasa wale Wazanzibari wanaoishi katika visiwa vidogo vidogo.

Mhe. Spika, swali langu la tatu ni kwamba ajali tumeshazizoea za mara kwa mara hapa za baharini, zinatokea ajali baina ya Pemba/Tanga boti zinakwama haziwezi kwenda masaa 24 zimo baharini tu, walipa kodi wanapata shida. Sasa Mhe. Waziri ni lini wizara yake itaweka *special speed boat* ambazo kazi yake itakuwa ni kuwaokoa watakaopata ajali ya baharini tu baina ya Pemba na Tanga, baina ya Pemba na Unguja na baina ya Unguja na Dar es Salaam.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hasa Waheshimiwa Mawaziri mnapokuja humu ndani jitayarisheni sana kukumbukia mambo ya waasisi vyenginevyo mtapata tabu maana Mhe. Saleh Nassor Juma anafuatilia kwa karibu sana. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote na kwa ruhusa yako nataka kwa dhati kabisa niwashukuru wote ambao wamechangia taarifa yangu hii ama kwa maelekezo, kwa ushauri na kwa maswali. Mhe. Spika, utaratibu huu ndio utaratibu ambao kwa sasa unafaa.

Mhe. Spika, Baraza lako inawezekana wewe umeshapata habari au hujapata habari lakini sisi tunaambiwa kwamba hili ni Baraza la aina yake. Ukweli na uwazi hakuna kinachofichwa, watu wanazungumza kwa upeo na kwa ruhusa kamili ya Spika na anawapa muda unaotosha. Kwa hivyo, hii sio sifa ndogo na leo hapa ni muendelezo wa hayo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema nashukuru sana kwa wote waliochangia na kwanza haraka haraka niende kwenye maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Kamati hii kwa kweli maoni yake wao kama walezi wetu tunayachukua ni ya msingi, ni ya maana kabisa na naamini tukiyafanyia kazi matatizo ambayo sasa hivi hapa tunazungumza yatapungua kwa kiasi kikubwa kama hayataondoka kabisa.

Mhe. Spika, kwanza nimthibitishie Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kwamba mimi nimeanza tu lakini Mawaziri wote tumejipanga kuhakikisha kwamba tunatii na tunatekeleza kwa vitendo maagizo anayotoa Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein. Sio katika kutoa taarifa Barazani tu lakini hata kuita waandishi wa habari wakaelezwa mambo mbali mbali ambayo yanatokea mawizarani.

Mhe. Spika, baada ya taarifa hii Barazani huu hautakuwa mwisho wa masuala haya kwa wizara yangu, tutakuwa tunatoa taarifa kila wakati ambapo tunaona kwamba kuna umuhimu wa kutoa taarifa kwa jamii. Kwa hivyo, huku ni muendelezo tu na juhudi za kutii maagizo ya Mhe. Rais wetu.

Mhe. Spika, suala la marekebisho ya kanuni ya masaa 48 kwa kweli humu imeandikwa hivyo lakini mimi nilifanya marekebisho kidogo wakati nilikuwa nasoma. Nilisema tokeo linapotokea kanuni zetu zinamuarifu na zinamtaka mmiliki wa chombo au nahodha atoe taarifa haraka iwezekanavyo. Hiyo ni taarifa ama kwa simu, hiyo ni taarifa ama kwenda, ni mawasiliano, lakini ile taarifa ya maandishi kwa sababu taarifa ya maandishi inatakiwa kwanza ufanye *investigation* ilikuwaje, ni *details* za kutosha. Kwa hivyo, hii imetoa masaa 48 si zaidi ya hapo.

Kwa hivyo, kanuni yetu inakidhi haja, inapotokea tunaiarifu haraka ama kwa njia za simu au kwa namna yoyote ile lakini taarifa ya maandishi iko hivyo.

Mhe. Spika, jengine ni kuhusu taarifa za hali ya hewa. Mhe. Spika, sisi tunapata taarifa zetu za hali ya hewa kutokana na Kurugenzi ya Hali ya Hewa ilioko Zanzibar. Sasa hivi tunafanya utaratibu wa kuweka tawi la idara hii pale bandarini na hili limekuja baada ya kuona kwamba hakuna urahisi au wepesi wa Idara hii ya Hali ya Hewa kwa Shirika la Bandari na Mamlaka ya Usafiri Baharini katika hali ya hewa ya baharini. Kwa hivyo, hizi ni juhudi wenzangu wameziona na sisi tumeziona mapema na tunaamini sasa hivi baada ya kujenga jengo moja pale la ofisi za *terminal* tutajenga tena ofisi ndogo kwa ajili ya *division* moja ya Idara ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Zanzibar ili na sisi pale tuwe tuna taarifa za hali ya hewa wakati wowote tunapozihitaji.

Lakini jengine Mhe. Spika, Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi amezungumzia uchakavu wa vyombo na amependekeza mambo mengi. Nayataja haraka haraka lakini nayachukua kwamba ni mapendekezo ambayo sisi kama mamlaka, sisi kama wizara na wao tutasaidiana kwa sababu wao vile vile nasema ni walezi kwa wizara hii.

Kuongeza kasi ya ukaguzi nitaeleza huko mbele kwenye swali kwamba tunakagua vipi au inakuwaje. Kuongeza wakaguzi na *press officers* ni kweli tuna upungufu kama alivyosema, tuna wakaguzi kwa maana ya *inspectors* wawili tu na wapo hapa Makao Makuu. Tuna *safety officers* wanne. Sasa kwa hali ya sasa hivi ilivyo na vyombo tulivyonavyo basi tuna vyombo vya usafiri hapa zaidi ya vyombo 25.

Sasa hivyo lazima tuongeze wataalam wa kukagua *safety officers* na baadhi ya watendaji wakuu katika mamlaka. Hizo ni juhudi ambazo mamlaka hii imeundwa karibuni na zamani ilikuwa ni kitengo tu cha Mrajis wa Meli, sasa ni mamlaka kamili na sasa hivi tumeshaandaa mambo mengi ili kuimarisha mamlaka, mapungufu haya yaliyozungumzwa yasiwe yanaendelea.

Ukaguzi wa idadi ya abiria Mhe. Spika, kwa taarifa ya Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba ukisikia *safety officer* anatoka mamlaka ni mtu anayehakikisha

abiria wanaoingia mle ni wangapi. Kwa sababu kila chombo kina uwezo wake wa kubeba abiria haruhusu hata siku moja chombo hicho kuingia abiria wengi zaidi kuliko ule uwezo ambao umepewa.

Lakini hapa Mhe. Spika, nataka niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kitu kimoja. Unapozungumzia meli kuchukua abiria kwa mfano meli ya Serengeti, meli ya Serengeti ilikuwa na uwezo mkubwa lakini kwa sababu ya uchakavu tumewapa wasichukue zaidi ya abiria 600. Ukisema abiria 600 maana yake ni wale ambao wanakata tiketi. Sasa mtu wa Serengeti atauza tiketi 600 au chini ya hapo lakini matokeo yake haiko hivyo.

Wameeleza wenyewe hapa kwamba usafiri wa Unguja na Pemba ni usafiri tofauti, ni *unique*, Unguja na Pemba na Pemba na Unguja ndio hiyo hiyo, anayekata tiketi mmoja lakini wanaosafiri ni watano. Sasa mama amekatiwa tiketi anakuja pale ana watoto wake wanne wote hawana tiketi huwezi kumwambia hawa wanne wasiende atakwambia basi na mimi siendi.

Tuna tatizo nakubali kwa hivyo suala hili lina ugumu wake kidogo. Serengeti, *Buraq, Sea Gull,* utaratibu wao ni tofauti na meli hizi kama *Azam Marine.* Sio watoto tu ambao anafuatana nao meli ile sio ya kuchukua mizigo ni ya kuchukua vizigo, anakwenda kule pengine na sanduku lake la mbao au pengine na ukili, lakini utamkuta mtu ana ndundu hizo anazijua Mhe. Saleh Nassor Juma, kwa Kipemba tunasema pawapawa, maana yake ile mizigo yenyewe hajui hata aichukue vipi na hiyo yote ni lazima asafiri nayo.

Kwa hivyo, meli hizi baina ya Unguja na Pemba na Pemba na Unguja katika kupakia abiria ni kwa muda mrefu tunafanya hivyo. Mhe. Spika, ukweli ni kwamba kama hakuna tatizo lolote usafiri huo haupigiwi kelele, tatizo linakuja chombo kinapoharibika. Mambo haya tunayozungumza hapa ni kwa sababu vyombo ni vichakavu, vinaharibika mara kwa mara. Lakini kabla ya hapo ilikuwa husikii kelele hizi watu ni wengi, mizigo ni mingi, vyombo vichakavu ni kwa sababu vyombo vyetu vingi ni vichakavu na vinaharibika mara kwa mara. Ndio maana leo tunatoa taarifa hii kwa ajili ya wananchi wafahamu.

Kwa hivyo, suala la *safety officers* kuhesabu abiria linakuwepo lakini utata na ugumu wake ni huo Mhe. Makamo Mwenyekiti na Waheshimiwa Wajumbe.

Huduma muhimu, usafi, vyoo na hata yale ma-*jacket* ya kuokolea maisha. Mhe. Spika, moja katika mambo muhimu na ambayo tunazungumza hivyo hivyo meli ya Serengeti natoa mfano huo huo inachukua abiria 600, maboya ya kuogelea kukitokea hatari ni 600, watu waliokuwemo mle ni 1,300. Hebu mimi niambie ni boya gani hilo mtakalojipanga kwamba mimi na wanangu tutachukua boya moja. Kwa hivyo, kuna matatizo na hili lazima tukubali

kwamba kuna matatizo, lazima tutafute utaratibu mzuri na huko mbele nitaeleza utaratibu gani mzuri tunautafuta serikali.

Mpango wa serikali wa ununuzi wa meli nyengine mpya na kubwa. Mhe. Spika, nikijibu hili nitakuwa najibu yale mengine yote ambayo yanafuata. Mhe. Spika, ni kweli na sasa hivi suala la kupatikana kwa meli kwa serikali *is very serious* na serikali inalichukulia hatua za kutosha.

Mhe. Spika, wakati meli ya MV Maendeleo inafanya safari zake vizuri mambo mengine yote haya hayajitokezi, lakini ni kwa sababu meli ya serikali ya MV Maendeleo nayo vile vile tumeizuia isifanye safari yake yoyote mpaka imefanyiwa matengenezo turidhike ndio tuiruhusu.

Mhe. Spika, serikali sasa hivi kwa taarifa ya Waheshimiwa Wajumbe ni kwamba kesho saa tano asubuhi tunakutana na ujumbe kutoka Uturuki na wamenipigia simu kwamba wamewasili Dar es Salaam na watafika hapa leo saa saba na tutakutana nao katika kujadili. Hawa ni wajenzi wa meli, hawa ni watengenezaji wa meli, hawa ni wakodishaji wa meli. *Six in one*, tumewaita makusudi kama juhudi za serikali kuja kuzungumza nao ili serikali ipate meli.

Mhe. Spika, sasa hivi ndio wakati ambapo kuna tatizo hili hivi tunavyozungumza, kwa hivyo unapozungumzia kununua meli mpya sasa hivi sio kweli kwa sababu meli sio kama gari kwamba unakwenda kule unanunua hii unakwenda kiwandani. Meli unayotaka lazima upeleke *specification* ijengwe na *minimum period* wataalam wanasema ya kujenga meli mpya ni kati ya mwaka mmoja na nusu mpaka miaka mitatu. Kwa hivyo, *minimum* ni mwaka mmoja na nusu. Hata leo hii ukisema serikali inunue meli mpya maana yake angalau tutakuwa na mwaka mmoja na nusu wa kupata meli mpya.

Tatizo lipo sasa hivi kwa hivyo uwezekano, mbinu au njia za kupata meli ziko nyingi na hizo zote tutazijadili kesho. Hiyo kesho ni Waturuki lakini kesho kutwa Jumanne saa tano tena asubuhi tuna ujumbe kutoka Netherlands tumeweza vile vile tuje tulizungumze hilo kwa upana na urefu.

Mhe. Spika, jana mimi na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais tumekuwa na kikao na kampuni moja ya Kichina tumekaa karibu masaa mawili tumetoka Barazani hapa tunazungumzia ni vipi wanaweza wakatusaidia kupata meli haraka. Wametwambia tarehe 2 Agosti tutakuwa na kikao ili tupeleke tunataka meli ya namna gani, kwa muda gani na baada ya hapo tufahamiane.

Kwa hivyo, mbinu za serikali katika kupata meli haraka iwezekanavyo zipo na katika kupata meli mpya kwa muda mrefu vile vile zipo. Shirika hili la Meli halitakufa, shirika hili tunaliimarisha na *system* zetu ni hivi vyombo vya serikali tumekubaliana nao. Wawekezaji kwa kushirikiana na serikali ama *Joint*

Venture au wanasema *Public Private Partnership (PPP).* Serikali na wawekezaji mnakubaliana masharti basi mnakwenda.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wako kwamba juhudi zinafanywa na taarifa ya vikao vyetu vyote vitatu hivi vya kesho na kesho kutwa na cha tarehe 2 tunategemea japo kwa dharura tuandike waraka tuupeleke serikalini kwa ajili ya kufanyiwa maamuzi ya mwisho.
Mhe. Spika, niende na Mhe. Omar Ali Shehe tatizo la serikali kutokuwa na meli zake. Ni tatizo lakini hili nimeeleza vizuri juhudi ambazo zinafanywa ili serikali iwe na meli zake.

Tatizo la serikali kuhusu vyombo vichakavu. Mhe. Spika, meli zipo mpya, zipo kongwe mno, zipo za umri wa kati na kati. Kwa mfano tu MV Maendeleo imeletwa hapa miaka ya 80 ina zaidi ya miaka 30. Lakini ingekuwa meli ile inakwenda vizuri msingejua kwamba ni kongwe kiasi hicho. Kuna meli za miaka mpaka 50 na zikiletwa hapa unaweza kufikiria kwamba zimetengenezwa jana. Kwa hivyo, suala la meli chakavu ninalolizungumzia hapa ni kwamba utaratibu ambao unafuatwa hapa Zanzibar ni kwamba serikali imetoa upeo kwa wawekezaji wa kila namna na wa kila aina wawekeze kwa masharti ya uwekezaji Zanzibar. Moja katika wawekezaji ni katika Sekta hii ya Usafiri Baharini.

Mhe. Spika, tuna makampuni karibu manane hapa yanamiliki vyombo vya usafiri baharini *Azam Marine, Sea Express, Sea Gull,* tuna vyombo 25.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri labda nitoe maelekezo. Unajua maswali ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamekuuliza kimsingi masuala muhimu sana na mengi tuliomo ndani ni sehemu ya mashahidi wa hayo. Sasa mimi nadhani ungeyapokea kwa jumla na ukayafanyia kazi kwa undani sana na baadae utuletee ripoti nyengine.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru hawa kwa kuleta taarifa hii kwa sababu ni kweli kabisa, kwamba matukio ya hivi karibuni yameleta taharuki kwa abiria wengi waliokuwa wanasafiri kwa vyombo vya baharini. Sasa wanachohitaji hawa ni kwamba haya waliyokuuliza na haya ambayo baadhi yao wamekuomba ni mambo ambayo yapo hivi sasa yanaendelea. Wanachokuambia hawa uyafanyie kazi na kwa kweli baadae utuletee ripoti nyengine iliyo nzuri zaidi na inayoonesha umefikia wapi katika hayo waliyokuagiza.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tukubaliane kwamba wajumbe hawa waipokee taarifa hii ya awali, lakini kwa kweli kabisa ipo haja ya kuyafanyia kazi na kuleta taarifa nyengine baadae. Nadhani tufikie hapo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa muongozo wako huo, nikushukuru tena na niahidi mbele yako na nikuahidi wewe pamoja na wajumbe wa Baraza kwamba masuala yote yaliyoulizwa, maelekezo yote tutaandika taarifa na taarifa hiyo tutaiwasilisha Barazani kwa manufaa ya Baraza hili na kwa uelewa wa Baraza hili na wananchi wenyewe. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Sasa wajumbe sasa tuone kama taarifa hii ya awali tumeipokea wale wanaoipokea wanyanyuwe mikono. Waliokuwa hawakupokea. Waliopokea wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ya taarifa ilitolewa iamuliwe)
(Hoja ya taarifa iliamuliwe na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, taarifa ifanyiwe kazi zaidi na tunategemea kikao kijacho tupatiwe ripoti nyengine juu ya yote maagizo waliotoa Waheshimiwa Wajumbe. Nashukuru tuendelee.

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI KWA MWAKA WA FEDHA 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Wajumbe wangu wamezidi kutoka jana na wameshakuwa karibu 18. Nimegundua baadhi yamarejeo kutokana na taarifa hii. Kuna maombi mengi yaliyonijia kwa shughuli mbali mbali, tukielewa kuwa leo kwa kawaida ni siku ya mapumziko, lakini siku hii imekuwa na shughuli nyingi sana.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tufupishe muda wa kuchangia. Tujaribu kufupisha sana muda wa kuchangia ili tuone kwamba inapofika kwenye saa tano pengine na dakika kidogo tumwite Mhe. Waziri kwa ajili ya kutoa majumuisho. Kwa hivyo, haraka haraka naomba nimkaribishe Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, na baadae Mhe. Suleiman Hemed Khamis, mkitumia dakika kumi kumi basi mimi nitafurahi, mtakuwa mmeniokolea muda na itasaidia kutokurejea yale yaliyokwishazungumzwa. Karibu.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kunipa afya njema pamoja na wajumbe wako wa Baraza hili tukufu kuwepo asubuhi hii hapa.

Pia nakushukuru na wewe kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia hotuba ya Wizaa ya Kilimo na Maliasili. Kwa kweli nitajitahidi kuokoa muda ili na wenzangu wapate nafasi hii. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake iliyojaa matumaini kwa wakulima wa Zanzibar, nampongeza sana kwa hilo.

Vile vile nampongeza tena Mhe. Waziri hasa alipopita kupunguza bei gharama za pembejeo kwa wakulima wetu. Kwa kweli naamini kwamba wakulima wengi hivi sasa wana matumaini makubwa sana kwa Wizara yao ya Kilimo na Maliasili kukihuisha kilimo kwa ajili ya maslahi yao na maslahi ya taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa hapa nimuombe Mhe. Waziri kuhusiana na suala hili la pembejeo, pamoja na punguzo kubwa, lakini kupunguza tu kutakuwa hakuwasaidii wakulima, kitakachowasaidia wakulima ni kwamba pembejeo hizi zipatikane kwa wakati unaofaa. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri labda atakapokuja hapa kuleta majumuisho awape matumaini wakulima, ni muda gani pembejeo hizi zitapatikana madukani ili wakulima wajimwage kununua na kukiendeleza kilimo chao.

Mhe. Spika, pamoja na hayo nimuombe Mhe. Waziri kwa kuwa tunataka kufanya mapinduzi ya kilimo, basi wataalamu wake wahamie makondeni kwa wakulima, kwa sababu wataalamu hubakia ofisini tu, basi kutawarudisha nyuma wakulima na hakutowasaidia wakulima. Lakini kwa sababu ya maagizo ya kitaalamu, wataalamu watakaporudi mabondeni kwa wakulima, basi tuna imani kubwa kwamba wakulima hawa watafaidika na badala ya kupata mavuno madogo kwa ukosefu wa utaalamu, basi tunaimani kubwa kwamba tutapata mavuno ya kutosha.

Mhe. Spika, nategemea kwamba kwa nia halisi ya Mhe. Waziri basi mbali ya kupata chakula tu kwa kilimo chetu hiki basi tutapata hata kuuza katika maeneo mengine ambayo yatahitaji kutoke kwetu Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na pongezi zangu nyingi kwa wizara hii ya kilimo. Ningemuomba anipe maelezo ya kutosha ya wananchi wangu wa Jimbo la Chambani kutelekezwa kituo cha kilimo cha Chambani ambapo kituo hiki kiliwasaidia mno wakulima wa Jimbo la Chambani ambao kwa asilimia 90 ya watu hawa ni wakulima. Pale palikuwa na kituo ambacho walikuwa wakipata maelekezo kwa mabwana shamba, palikuwa na nyumba ya kilimo ambayo baadhi ya maafisa walihamia pale kwa miaka kadhaa. Lakini nyumba ile imetelekezwa, sasa hivi watu wa Chambani wanajiuliza jamani hii wizara ya kilimo imekufa. Kwa hivyo, namuomba Mhe.Waziri atakapokuja kutoa majumuisha atupe maelezo yanayoelezeka kwa wananchi hawa kujenga

matumaini na kituo au nyumba yao ile ambayo hivi sasa iko katika hali ambayo haieleweki.

Baada ya hayo Mhe. Spika, niende katika usanifu wa matunda. Kwa kweli Zanzibar ni nchi ndogo, lakini Mwenyezi Mungu ameibariki matunda mengi. Tuangalie unapofika msimu wa maembe tu, basi embezi zinaozeana ovyo na zinatushinda. Kwa sababu wakaazi wa nchi ya Zanzibar ni wachache mno kuliko embe zinazozaliwa. Lakini sasa tumeshindwa kuyasanifu matunda haya yanapotea mno. Ningemuomba Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili ashirikiane na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili watuwekee kiwanda japo kidogo cha kuweza kuyahifadhi matunda yetu. Mhe. Waziri tuna matunda mengi basi yasipotee tu ovyo matunda haya, tuyahifadhi ili matunda haya unapomalizika ule msimu basi tuyatumie kwa njia nyengine.

Mhe. Spika, nikiachilia mbali hayo, niende katika mikarafuu na minazi. Mhe. Waziri nakumbuka katika miaka kadhaa iliyopita, nafikiri kama sikosei ni utawala wa Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi. Kulikuwa na kanga zinasema "nazi na karafuu kwetu ndio nafuu", kanga hizi kinamama wengi walivaa, nafikiri hata humu wamo katika wanawake ambao walizivaa kanga hizi. Kwa nini zikaletwa kanga ambazo zimeandikwa nazi na karafuu kwetu ndio nafuu, kwa sababu karafuu ni miongoni mwa uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar. Sasa basi pamoja na kwamba zao hili kwa asilimia kubwa limemilikiwa na wakulima wenyewe, basi naiomba serikali kupitia wizara ya kilimo iwape uwezo wakulima wa mikarafuu ili yale maeneo ambayo mikarafuu inaota ikipandwa, basi wapewe uwezo mkubwa sana ikiwezekana hata kukopeshwa fedha kwa ajili ya kuuhisha mashamba yao ya mikarafuu. Vyenginevyo Mhe. Spika, utafika wakati mkarafuu hapa Zanzibar uonekane tunu, kwa sababu mikarafuu inakufa. Lakini pia kuna baadhi ya maeneo mikarafuu inaota, ikipandwa mikarafuu inaota. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri suala hili alipe nafasi kubwa.

Lakini pamoja na hilo, vile vile minazi Mhe. Spika. Minazi inatoweka sana. Kama walivyochangia baadhi ya wajumbe jana hapa kwamba inaonekana kuwa minazi kama kwamba hapa kwetu sisi tumeiondowa thamani yake. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili suala hili aliangalie kwa kina, kwa sababu kupotea kwa minazi hapa Zanzibar tunaiondoa rasilimali asilia mbayo tumeirithi, tumeondoa asilimia kubwa ya rasilimali asilia ambayo ilikuwa ikitupatia tija katika miaka iliyopita.

Mhe. Spika: Malizia Mhe. Mjumbe.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Naam, ahsante. Mhe. Spika, katika kuokoa muda niende katika maliasili. Jamani miti ni uhai. Mhe. Spika, nataka nimuambie Mhe. Waziri kwamba Mwenyezi Mungu alipoiumba hii dunia,

kwanza aliotesha miti ndipo alipotuleta sisi wanaadamu. Leo kwa nini tunaiwacha misumeno ya moto itaikata miti yetu na sisi tuko tunaangalia hivi hivi. Imepambwa dunia hii kwa miti. Kwa hvyo, Mhe. Waziri nakuomba uliangalie suala hili kwa kina sana ili nchi yetu isijekuwa jangwa wakati ambapo ilikuwa ina miti mingi na yenye rutuba na vivuli vyenye kuleta hewa nzuri na upepo mzuri. Kwa asilimia 80 naiunga mkono hoja hii na kwa asilimia 20 nitaziingiza pale nitakapopata maelezo ya kutosha kuhusu kituo cha kilimo cha Chambani, ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia hotuba ya Waziri wa Kilimo na Maliasili. Mhe. Spika, kwanza napenda nimshukuru na kumpongeza Waziri wa Kilimo na Maliasili, kwamba katika kitabu chake kuna maelezo mazuri sana na hayana tatizo yako wazi na yana muelekeo mzuri.

Vile vile Mhe. Spika, nataka niseme kwamba waziri mara hii amepania sana kuleta mageuzi na mageuzi ni mazuri sana kwa sababu bila ya kufanya mageuzi haiwezekani, kwa sababu mageuzi ni katika suala moja la kuleta maendeleo. Kuna mageuzi ya binadamu na kuna mageuzi ya kilimo, kwa hivyo hayo ni mabadiliko. Tunataka kutoka kule tulikokuwa na kuingia kwengine. Kwa hivyo, nimpongeze waziri kwa kuleta fikra hizo za kuleta mageuzi.

Pia Mhe. Spika, niseme kwamba waziri amechukua nasaha ya Mhe. Rais kwamba dhamira ya kuleta mapinduzi ya kilimo. Yeye anataka kuleta mageuzi, lakini na Mhe. Rais anasema tulete mapinduzi ya kilimo, ambapo ilifafanuliwa zaidi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba zake za uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi uliofanyika tarehe 05/11/2010. kwa hivyo, mimi nimpongeze kwamba na yeye ametii amri ya Rais kwamba papatikane mapinduzi ya kilimo.

Mhe. Spika, katika mageuzi haya ya sekta ya kilimo kwa njia ya umwagiliaji, ambapo huu ni umwagiliaji maji. Hii itakuwa ni nzuri na itakuwa inaleta faida kubwa sana kwa maisha ya wakulima wetu na hii itasaidia kuleta uzalishaji kwa wingi kutokana na njia hizi nzuri za umwagiliaji. Njia hii ni njia ya pekee ambayo vile vile itaweza kuleta tija kubwa sana na kuweza kuongeza mapato na kupata uhakika wa chakula. Haya ni mambo ambayo wakulima wetu wamekuwa wakiyasubiri kwa muda mrefu. Kwa hivyo, mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada zake za kuweza kuyafikiria haya kwamba mageuzi haya yataweza kuleta tija, kuweza kuleta chakula kwa wingi na kuongeza pato la wananchi. Hii itaweza kusaidia kupunguza umaskini.

Mhe. Spika, kama tunataka kufanya mageuzi haya ya kilimo, kuna mambo ambayo ni lazima tuyafikirie. Kuhusu mahitaji ya kilimo ambayo ni muhimu sana, mtu bila kupata mahitaji ya kilimo basi kilimo hakiwezi kufanyika. Kwa

hivyo, katika mahitaji ya kilimo suala moja muhimu ni suala la mbegu, jengine ni suala la mbolea, suala la madawa ya kuulia magugu ya shamba. Vile vile suala la chumvi ambayo itasaidia mipunga kukuwa kutokana na kudumaa. Kwa hivyo, haya masuala ni muhimu sana, lakini mimi nataka niseme kwamba nimuambie Mhe. Waziri kwamba suala hili la mbegu pamoja na mbolea na vitu vingine, basi mambo haya yanakawia sana kuwafika wananchi, hawayapati kwa wakati ambao unatakiwa. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri kwenye suala hili akafanya jitihada kubwa sana ili kuhakikisha kwamba mbegu za mpunga, mbolea na madawa ya kuulia magugu pamoja na chumvi iweze kupelekwa kwa haraka kwa wakulima ili waweze kufanikisha masuala ya kilimo.

Vile vile Mhe. Spika, kuna huduma za matrekta. Trekta huwa ni moja na mara nyingi huwa linachelewesha baadhi ya wakulima kuweza kufanya kazi zao kwa wakati. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri matrekta yakaweza kufanyakazi mapema katika mashamba ya kilimo ili watu waweze kulima mapema kwa wakati unaotakiwa.

Jambo jengine la msingi Mhe. Spika, napenda kumuambia Mhe. Waziri kwamba katika shughuli zote hizi ni lazima tupate elimu kwa wakulima. Mimi napenda kusema kwamba hili ni suala muhimu, wakulima wetu wanahitaji kupata elimu, kuweza kupata wataalamu ambao wanaweza kutoa elimu ile. Katika shughuli hizi utakuta kwamba kuna upungufu wa wataalamu. Kwa hivyo, ni vigumu sana kuweza kupitiwa wakulima na kuweza kupewa ushauri.

Mhe. Spika, tunachomuomba Mhe. Waziri ni kwamba hawa wataalamu ikiwa watapatikana waweze kuwapitia wananchi hawa. Wanaweza kuwepo katika maeneo wataalamu lakini wakawa hawapiti katika maeneo. Mimi ningemshauri Mhe. Waziri katika suala hili la wataalamu wake.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hapa aweze kupanga kama ratiba maalum kwa kila yule ambaye atafuatilia shughuli za wakulima, aweze kutoa ratiba yake kwamba leo atakwenda huku na leo atapitia hiki na hichi, basi wasiachiliwe tu katika maeneo yao wenyewe wakaamua, lakini iwe idara kwa makusudi iweze kuwapangia watu hawa kwamba wanatakiwa waangalie kitu kadhaa na kadhaa.

Kwa hivyo, kwanza wanatakiwa watowe elimu ya usafishaji wa mashamba ambayo yanatakiwa yawe masafi, wanatakiwa elimu ya kuweza kupanda kipando chao kwa wakati unaofaa. Vile vile wataalamu hao waweze kuwasaidia wakati wa mabadiliko ya hali ya hewa. Ni mara nyingi tuweze kukubaliana kwamba wakulima wetu wanakuwa wakaidi katika kufuata mabadiliko, wao wamezowea mabadiliko yao ya zamani yale yale, kwamba ikifika mwezi fulani na mwezi fulani tayari. Lakini mara nyingi wataalamu

wanajua kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa. Kwa hivyo, hili ni suala muhimu kuweza kuwapatia elimu wakulima wetu ni muhimu sana.

Mhe. Spika, wakulima wetu wamezowea kutumia mbegu zao za zamani za asili, ambazo tunasema ni sawa sawa na ufugaji wa ng'ombe. Ng'ombe hawa *traditional* tumesema kwamba hawana uwezo wa kutoa maziwa mengi. Ni sawa sawa na mbegu zao tunazotumia za kienyeji uzalishaji unakuwa ni mdogo. Kwa hivyo, mimi ningemuomba Mhe. Waziri hawa wataalamu waweze kuwazungukia wananchi na kuwaeleza aina ya mbegu ambazo zimetoka mara hii *super* pamoja na nerika, ambazo ni mbegu nzuri, muhimu na ambazo uzalishaji wake ni mkubwa sana. Masuala haya watu wengi hawayaelewi, sasa hao wataalamu wa mbegu wakipatikana waweze kuwapelekea hizo mbegu na ziweze kufikishwa kwa wakati mzuri.

Vile vile tungemuomba Mhe. Waziri kwamba maradhi yanaingia kwa wingi, hizi mbegu zinazokuja kutoka nje Mhe. Waziri ahakikishe kwamba hizi mbegu ni safi na hazina wadudu. Lakini katika kipindi hiki cha mpunga wa mwaka huu, umepatikana uharibifu mkubwa sana. Mimi katika jimbo langu Mhe. Spika, nilitoa dawa ya kuulia wadudu ili kuweza kuwasaidia wakulima.

Kwa hivyo, suala hili ningemwambia Mhe. Waziri ni muhimu sana na kila wakati tuwe na hadhari ya suala hili, wadudu wanapotokezea na wakulima waweze kupata hizi dawa na kupelekewa katika maeneo yao. Ni suala muhimu sana na kwa sababu ikiwa hatukupeleka dawa, mashamba yakibakia vile vile, ina maana wakulima kwenye mashamba yao hawatovuna kitu.

Jambo jengine Mhe. Spika, ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la kupotea kwa haiba ya vituo vya utafiti wa kilimo. Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri katika kipindi kirefu nilikuwa nazungumzia kituo changu cha Matangatuani, *Matangatuani Agricultural Station.* Kituo hiki kwa kweli kimekufa, maabara haina kitu na huu utafiti wenyewe kwa kweli umekuwa ni wa tabu sana. Nilimuomba Mhe. Waziri Matangatuani takriban inasaidia Jimbo zima la Konde. Kwa kweli wakulima hawajafaidika na kituo chao. Kuna matatizo chungu nzima ambayo yanatokea ya maradhi ya mimea. Kwa kweli hawajapata kufaidika na kitu chochote. Maabara hii tuliyokuwanayo sisi hapa, hakuna mtu kufanya utafiti na maabara ile hakuna mtu wa kusimamia sawa sawa na hakuna vifaa vya kufanyia kazi katika maabara ile.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kile kituo cha Matangatuani akiangalie sana, huduma ziweze kupatikana kwa wakulima na maabara ile iliyoko pale iweze kufufuliwa vizuri na ile iwe ni sehemu ya majaribio. Mimi nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba kilimo sio cha mpunga tu, lakini tumezungukwa na vilimo vyengine, kama ukulima wa mimea ya migomba ambapo tunaona maradhi mara nyingi yanatokezea, tunapata maradhi yale ya

sijatoka. Mpaka sasa hivi kile kituo cha Matangatuani na vituo vyengine vyote, wameshindwa kuweza kusawazisha suala la matatizo ya maradhi yao, kunyauka kwa majani ya migomba.

Vile vile tunapata maradhi mengine ya mihogo na maradhi ya michungwa, haya yote hayashughulikiwi. Kwa hivyo, nadhani vituo hivi kama vitakuwa *live*, naamini kuwa wataweza kufanya utafiti mzuri na wakulima kuweza kusaidiwa madawa ya kuulia. Utakuta miti mingi ya matunda inakufa.

Mhe. Spika, katika suala jengine nataka niseme kwamba kuna hii Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Kila Wizara, hata mara ile niliwahi kuizungumzia kila wizara inakuwa nayo hii Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Sasa kila wizara inakuwa na shughuli hizi za kufanya utafiti wake.

Mhe. Spika, mimi nilishauri mara ile, pamoja na huu utafiti uko kila wizara, lakini kwa nini hatuweki kituo kimoja cha utafiti kwa kila wilaya, ambacho kitajulikana mahali pamoja kama ni mkoa au mahali popote, lakini ikawa kuna kituo, kuna ma-*professor* na kuna wataalamu wakubwa. Utafiti wote ukawa unasimamiwa mahali pamoja, hili lingekuwa ni jambo la busara, kwa sababu naamini Mkurugenzi ambaye anashughulika na suala la utafiti pengine anafanya utafiti mdogo tu sio wa kina. Kwa hivyo, nina amini mimi kama kungekuwa kuna kituo maalum, hizi tafiti zote zikawa mahali pamoja, basi ingeweza kusaidia mambo yote na uwamuzi ukawa ni mzuri. Yeye atafanyakazi katika wizara yake, lakini vile vile atakuwa ni *answerable* katika kituo kile ambapo utafiti unakuwepo pamoja.

Mhe. Spika, mimi nataka kujua kutoka kwa Mhe. Waziri kwa kuwa hawa Wakurugenzi tunao na hawa Wakurugenzi ndio wanaoshughulika na masuala mazima ya utafiti. Hebu Mhe. Waziri katika majumuisho yake anieleze, kuna ripoti zozote ambazo kutokana na maradhi tuliyoyapata ya mimea yetu. Je, kuna ripoti zozote ambazo zipo zimetolewa, namuomba Mhe. Waziri wakati wa majumuisho yake aje atuambie. Je, kumetolewa elimu yoyote baada ya utafiti uliofanyika ukaonekana ili kuweza kuwasaidia wakulima, kuna elimu yoyote ya wakulima ambayo ilitolewa kwa watu hawa.

Mhe. Spika: Unadakika mbili tu Mhe. Mjumbe.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante Mhe. Spika, namalizia. La mwisho nataka niseme kwamba mimi katika eneo langu la Jimbo la Konde, nina eneo kubwa na ardhi hii nimewahi kuizungumza mara nyingi ni ardhi ya tambarare. Mimi katika Jimbo langu la Konde ninayo maji ya kutosha, ninavyo visima vya kutosha. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri ule ukulima wa kutegemea mvua, mimi naomba katika eneo ambalo ninayo tambarare kubwa sana na maji

tunayo katika tambarare hizo. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri anipitie tuje tuzungumze kama kuna uwezekano na sisi tupate ukulima wa umwagiliaji.

La mwisho Mhe. Spika, namalizia kuhusu hiki kilimo cha maweni ambacho ni muhimu sana. Nginemuomba Mhe. Waziri katika pirika zake zote za kuangalia maisha na mwenendo wa kilimo cha mpunga, lakini vile vile awatupie jicho watu wa maweni katika kilimo chao cha mtama, kunde, mbaazi, uwele, viazi vikuu, mahindi, fiwi na vyakula vyengine ambavyo vinaliwa. Hawa watu kwa ufupi tunasema mbegu za kupelekewa hawa wananchi hazipatikani kwa wakati. Kwa hivyo, hawa wakulima, ingawa wizara sasa hivi ina kazi kubwa sana ya kutafuta wataalamu na wale wa kuchanjagia.

Mhe. Spika, mimi niseme katika wizara, wizara haidhuru najua Wizara ya Kilimo na Maliasili ina wataalamu wengi, ina watu wengi wenye kujua masuala mengi ya kilimo, lakini suala la ufuatiliaji wa mambo haya ni mgumu sana. Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Waziri aelewe kuwa katika kila jimbo tunahitaji watu wa kuweza kufuatilia masuala yetu ya kilimo na haya yataweza kumrahisishia yeye. Bila ya kuweza kuwapata watu hawa wakaenda kutoa elimu ya namna kwa namna na kuwapelekea mbegu, mbolea na vifaa vyote hawa watu alioko chini katika maeneo yetu sisi yaani wako katika majimbo, kama hawakuitwa wakaelezewa na kuweza kuwafuatia wakulima, basi nasema kazi yote hii ambayo uliyoipanga nzuri Mhe. Waziri katika kilimo itakuwa ni ngumu sana.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Konde, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, ahsante.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia wizara hii. Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa hazina ya uhai na uzima kufika katika Baraza lako tukufu nikiwa na afya njema.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhati kabisa jinsi ya umakini wake na umahiri alivyoielezea bajeti yake hii iliyojaa matumaini kwa wananchi wa visiwa hivi vya Zanzibar.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 23 ibara ya 36 Mhe. Waziri alizungumzia kuwepo kwa mashamba darasa 720 yaliyomilikiwa na kaya 12,600. Kimsingi naipongeza sana wizara yake kwa kuhamasisha uzalishaji wa uendelezaji wa mashamba haya, yatatusaidia sana katika visiwa vyetu hivi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika miaka ya nyuma ilimiliki mashamba makubwa ambayo mashamba hayo yalikuwa yakiwasaidia

wananchi wetu, kwa ajili ya kupta utaalamu wa kilimom pejembeo, mbegu za kuuliza magugu na kadhalika. Kwa upande wa Kisiwa cha Pemba yalikuwaweko Mtakata Wilaya ya Chakechake, Dodeani – Weni kwa Wilaya ya Wete na Msaani kwa Pandani Jimbo la Wete.

Kwa kweli mshamba haya yalikuwa yakiwasaidia sana wafanyakazi pamoja na wakulima wa maeneo hayo kwa ajili ya kupata maslahi makubwa sana. Lakini kwa muda mrefu sasa ardhi hizo zinaonekana hazifanyiwi jambo lolote lile na zimekaa tu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa ajili ya kufanya majumuisho, basi tunamuomba atuelekeze jinsi ya mashamba haya atakavyoyaendeleza, ili wananchi wetu wa maeneo hayo wapate maslahi kama walivyokuwa wakipata kipindi cha nyuma.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu ukulima wa mboga mboga kama kuna maeneo ambayo watu wamehamasika na kilimo cha mboga mboga basi ni Kisiwa cha Pemba. Mhe. Spika, Kisiwa cha Pemba hasa wanawake wamehamasika sana na kilimo cha mboga mboga. Kwa mfano, kuna wanawake wa upande wa *Ali Khamis Camp* wanacho kikundi maalum, yaani wakulima wazuri sana wa mboga ya mchicha, kwa kweli inafikiwa wakati mboga ile inakuwa haina hata soko.

Vile vile tukija katika maeneo ya Wilaya ya Wete kuanzia Jimbo la Ole, Kiuyu, Kangagani, Tungamaa, Machengwe katika Jimbo la Mtambwe wako akina mama wanaozalisha sana mazao kama vile matikiti maji, matango, pilipili mboga, nyanya chungu, tungule, hivyo hizi zinafikia wakati hazina soko.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri awasaidie akinamama hawa katika kuwatafutia masoko ya uhakika ya kuuza bidhaa zao, ili wajikwamue na maisha, kwani serikali inapiga kelele kwa muda mrefu watu wajiajiri wenyewe.

Kwa kweli akinamama hawa Mhe. Spika, nataka nimwambie Mhe. Waziri kuwa wanafanyakazi katika mazingira magumu sana ya kujichangisha wenyewe kwa wenyewe, kuomba huko na kule kwa ajili ya kutafuta vifaa, mbegu, mbolea pamoja na mipira kwa ajili ya kumwagilia maji. Lakini baada ya gharama zote hizo inaonekana soko inakuwa ni tatizo kubwa kwao.

Mhe. Spika, naomba nimueleze Mhe. Waziri licha ya imani na azma nzuri sana aliyonayo kwa wakulima wetu wa Visiwa vya Zanzibar. Hivyo, naomba nimueleze kwamba wakulima wa kisiwa cha Pemba wameharibikiwa sana na mazao yao katika kipindi hiki ya mpunga na mihogo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba achukue jitihada za makusudi awapitie wakulima wale na kuwakagua na ikiwezekana awasaidie angalau kuwapata faraja katika kilimo chao kile kilichoharibika. *(Makofi)*

Mwisho namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atupe maelekezo yenye uhakika kuhusu wadudu wanaoshambulia matunda. Mhe. Spika, pamoja na mitego mingi aliyoieleza kwenye kitabu chake kwamba kuna mitego mingi ya kutegea wadudu hawa, lakini bado wadudu hawa wanaonekana kuwa ni wengi, hivyo yeye kwenye kitabu chake alisema mitego mingi ameipeleka Mkoa wa Kusini.

Kwa hiyo, nataka nimwambie katika sehemu matunda yanakoshambuliwa na wadudu ni Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba na hizo ndizo wilaya zinazozalisha matunda kwa wingi sana, kama ingekuwa kwenye matunda yale haya wadudu, basi njaa au tatizo lolote la matunda lisingeonekana kwenye visiwa vyetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kumalizia naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Spika. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia afya na uzima na leo kufika asubuhi hii kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, kuwa muda ni mfupi na mimi nitachangia kwa kutoa maelezo yangu mafupi tu. Kwanza nimshukuru Mhe. Waziri na kubwa lililolifanya nisimame hapa nilite salamu zake kutoka wakulima wa bonde la Cheju.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri uchukue salamu zako kwa wakulima wa bonde la Cheju wanasema mwaka huu wanakupongeza sana kwa kuwa pamoja nao na kuboresha kilimo chao na kupata mafanikio mazuri ya Cheju. Sasa wanasema kama uko tayari Mhe. Waziri pamoja na kambi yako, basi hata leo uende Cheju kwa ajili ya kuvuna. *(Makofi)*

Hivyo, nakuomba uchukue pongezi hizo, pia pongezi hizo uwapelekee maafisa wa kilimo kwa kuwa karibu mno na wakulima wa bonde la Cheju. Mhe. Spika, nadhani ukaribu huo ndio uliwapelekea mafanikio ya ukulima pamoja na mavuno mazuri kuyapata katika bonde la Cheju. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa kuwa kwenye kitabu cha hotuba ya Mhe. Waziri, basi ile kiu ya wakulima ya kutaka kupunguziwa pembejeo wamepata mafanikio na jana wamesikia katika hotuba ya Mhe. Waziri. Kwa hivyo, nampa pongezi kwa sababu nimepokea simu kutoka bonde la Cheju zinazopata 10 pamoja na *message*, ambapo wamefurahika sana na maelezo yako yaliyokuwemo kwenye bajeti. *(Makofi)*

Kutokana na mafanikio ya watu wa Cheju waliyoyapata mwaka huu ni mazuri. Hivyo, ombi lao katika Kilimo cha Mpunga ni kwamba utapanda, utapalilia na hatimaye wakulima wa mpunga wanakuja kuchoka wakati wa mavuno. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi ni mkulima mzuri wa mpunga, kwa hivyo najua wakati wa kuvuna nakumbuka huu ni kama mwezi mzima watu wako katika mavuno. Kwa mfano, kabla hatujaanza hili Baraza mimi nilikwenda Cheju kuvuna na iliiona ile hali, yaani mpaka leo watu wanatafuta wavunaji hawana. *(Makofi)*

Katika kitabu chako ukurasa wa 46 Mhe. Waziri hapa umeeleza jinsi ya utaratibu mzima wa kutayarisha zana za kisasa zikiwemo *harvester* za kuvunia. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alisema hizi hazitoshi kwa bonde zima la Cheju, hivyo nadhani hizi *harvester* 30 zingeingia bonde ka Cheju tu. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri pamoja na pongezi zote ulizopewa watu wa Cheju uwaona na zana hizi za kuvunia, kwa kweli hadi leo mpunga unawashinda kuvuna uko makondeni na wanatafuta wanyamwezi huku na kule kwa ajili ya kuvuna, siku hizi wanyamwezi hawataki kulima wala kuvuna. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri bonde la Cheju na wao awatizame kwa ajili ya kuwapatia zana za kilimo za kuvunia. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine nizungumze kwa haraka ni kuhusu misitu. Kwa kweli misitu inateketea, kwa sababu kuna matatizo makubwa ya watendaji wetu wa wilaya, wafanyakazi wa wilaya wana matatizo makubwa. Katika bajeti iliyopita, yaani Baraza la Saba nilizungumza na leo narejea tena Mhe. Waziri, hivyo naomba watizamwe wafanyakazi hawa.

Kwa mfano, mfanyakazi mmoja anakuwa na shehia nne mpaka tano azunguke mfanyakazi huyu na wala hana chombo chochote cha kuzungukia. Mhe. Spika, naomba wakopeshwe japo baskeli, ili wapate vyombo vya kufanyiakazi. Wakati mengine mtu anakaa Dunga anatakiwa aende Uzi na mazingira ya Uzi tunajua ya kuvuka. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunaomba kwa umahiri wako ulionao, naomba ukae nao wafanyakazi hawa na uwasikilize malalamiko yao na uwasaidie, kwa sababu hawa ndio tunaowapa kazi ya kulinda huu msitu wetu ambao unaathiriwa kila siku. *(Makofi)*

Suala jengine Mhe. Spika, ni kwamba wafanyakazi hawa wanafanyakazi wakati wote. Sasa msitu wetu unapovamiwa ni kuwa sio kama utavamiwa mchana au wakati wa jua kali, wakati mwengine inakuwa ni siku za mvua hawana hata *raincoat* kwa ajili ya kujihifadhi na mvua, sasa watakwenda vipi na wakati wa mvua watu ndipo wanapovamia msitu.

Kutokana na hali hiyo, naomba wapatiwe vitendeakazi kama vile *rain boot*, ili waweze kufanyakazi zao kwa umakini, wakati msitu tunauhitaji, unateketea na ikiwa wafanyakazi wetu hawa hatuwapi vitendeakazi, hivyo watashindwa kufanyakazi za kulinda huu msitu wetu. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Spika, kuna wananchi wa Charawe, Ukongoroni. Kwa kweli wananchi hawa ajira yao kubwa ni kuni tokea asili, Mhe. Spika, nimesimama hapa kama mwanamke nathubutu kusema kama wanawake ndio ajira yao kubwa na wala hakuna ajira nyengine wanayoifanya kule. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho anifahamishe tena na wananchi hawa wasikie je serikali imejiandaa vipi kwa ajira mbadala kwa wananchi hawa wa Charawe na Ukongoroni ikiwa msitu ndio ajira yao kubwa na sisi msitu tunauhitaji.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri aje atueleze kuhusu ajira mbadala kwa wananchi hawa ambao wanaoishi sehemu zile kuna ajira ambazo wamezizoea nyuma.

Mhe. Spika, naomba kwamba mengine niyaache kutokana na muda wako, kwa sababu napenda sana kukuheshimu. Hivyo, naunga mkono hoja hii.

Lakini moja nimelisahau kidogo Mhe. Spika samahani, nadhani suala hili kama sikulisema ingelikuwa mtihani. Kwa kweli kuna wakulima wadogo wadogo naomba wataalamu wawe karibu sana na wakulima hawa, kwa sababu ule utaalamu walionao wakenda kwa wakulima wadogo wadogo basi watabadilishana mawazo.

Kwa mfano, niliwahi kuona siku moja wakulima wa tungule Bungi, kwa sababu kuna tungule ambazo walikwenda wataalamu wakawafahamisha wakulima wadogo wadogo jinsi ya upandaji wake, basi wakulima wale walipanda konde ambayo walifundishwa na wataalamu.

Sasa baada ya kuondoka wataalamu wakaweka sehemu nyengine kwa kufuata ule utaratibu waliofundishwa na wataalamu, kwamba wakifika zile tungule kiasi wanazikwabua makwapa yale yaliko pembeni.

Vile vile waliweka na konde nyengine ambayo waliweka wao kwa utaalamu wao wakulima na ile konde ya pili hawakukwabua makwapa. Sasa lakini wakati wa mavuno wakenda wakawachukua tena wataalamu, kwa ajili ya kuangalia ule utaalamu waliowapa wao na ule waliofanya wale wakulima wadogo wadogo.

Mhe. Spika, kwa kweli walibadilisha na mawazo vizuri, wataalamu wale baada ya kuondoka basi walijua mafanikio ya utaalamu waliowapa pamoja na ule walioweka wakulima wenyewe. Kwa hivyo, ndio maana niliposema kwamba wataalamu hawa washuke, yaani wawe muhimu kushuka kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo na kuwapa utaalamu wao.

Hivyo, naomba Mhe. Waziri nadhani ni vyema kushirikiana sana na wataalamu wasikae kwenye meza, yaani umefika wakati wataalamu wa kushuka wataalamu kwenda kuwasaidia wakulima kuwapa utaalamu wao, ili kuweza kuwasaidia na kuwakwamua katika huu umasikini tunaosema tunataka kuondosha umasikini.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri na vikundi hivyo viko Bungi na wewe mwenyewe ukipata nafasi vitembelee, ukaone jinsi utaalamu wa tungule wananchi wetu wanavyojituma katika kulima tungule hizo.

Mhe. Spika, baada ya hayo, naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kuwasilisha bajeti *speech* yake katika Baraza lako tukufu, *speech* ambayo imekusanya kila kitu. Vile vile niwapongeze na watendaji wake wote wa wizara yake.

Mhe. Spika, kama walivyokwisha wenzangu kuchangia wizara hii ni kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu. Kwa hivyo, wizara hii ni muhimu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naona wajumbe wangu wanaondoka sana na si muda mkubwa nategemea nimwite Mhe. Waziri inaelekea naweze kubakia peke yangu na Mhe. Waziri, sasa itakuwa kazi kubwa sana naweza kushindwa kufanyakazi hii. Kwa kweli kazi yangu inawezekana nikiwa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo, niwaombe sana wanaokwenda nje kwa dharura si muda mkubwa warudi, ili tumalize hii kazi. *(Makofi)*

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri anayo kazi kubwa tena nzito ya kuongoza wizara hii. Wizara hii kama nilivyosema kwamba ni wizara ambayo ni uti wa mgongo wa taifa letu.

Lakini nimuombe Mhe. Waziri ili tupate mafanikio katika masuala ya kilimo ni kwamba awasaidie wakulima watumie vifaa vya kisasa, ili watumie nguvu ndogo na mapato yawe ni makubwa, kwa ajili ya kuweza kujisaidia na mambo

mengine, kama vile wapate mahitaji ya chakula pamoja na mengine wauzi na wapate mahitaji mengine ambayo ni muhimu.

Mhe. Spika, kilimo kinasaidia sana kwa vile taifa letu ni taifa la wafanyakazi pamoja na wakulima.

Kwa kweli Mhe. Waziri mbali na *Strategic Plans* zake pamoja na malengo yake aliyoyaweka kwa kipindi hiki cha mwaka 2011/2012, lakini hata hivyo kuna mambo lazima ayatilie mkazo kwa wafanyakazi wake pamoja na wakulima wetu wa Visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Kwanza naomba nimueleze Mhe. Waziri kwamba kuna haja ya kuwasaidia wananchi wetu kwa kuwawekea Viwanda Vidogo Vidogo, kwa sababu tunaona katika nchi zetu za *Tropical*,mara nyingi matunda yanakuwa mengi kwa wakati mmoja, ambapo kwa wakati ule yanakuwa ni mengi na kuozea mashambani tena bila ya soko.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aandae hizo *Strategic Plans* angalau tuwe na Viwanda Vidogo Vidogo vya kuhifadhi au kusindika matunda haya, ili kupata yale mahitaji yetu na nguvu kazi yetu ya kilimo iwe na tija kwa wananchi.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie kuhusu misitu. Kwa kweli misitu ni muhimu na bila ya misitu hatuwezi kuwa na maisha, kwa sababu tunapokata misitu tunaharibu mazingira na hata mvua hatupati pamoja na hicho kilimo hakitokwenda mbele.

Hivyo, ni muhimu kuhifadhi misitu na hasa ile misitu ambayo ni ya Hifadhi ya Taifa ni muhimu zaidi, kwa sababu tunapata wageni mbali mbali na hasa wale watalii ambao pia ni muhimu kwa taifa letu, tunategemea sana mambo ya utalii.

Mhe. Spika, ni ukweli usiofichika kwamba wakulima wetu wanajitahidi, lakini kuna suala ambalo linajitokeza sana siku hizi ni wizi wa mazao. Kwa kweli wizi wa mazao umekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wetu, yaani wewe unategemea kwamba kesho utakula ndizi, sasa unaiwacha ndizi ile ili kusaidia wewe pamoja na familia au jamii, wakati unapokwenda mwenzio tayari ameshaikata.

Kwa hivyo, ninaomba sheria za mazao pamoja zile za nchi kuhusu suala hili la wizi, mtu akipatikana na suala hili basi achukuliwe hatua, yaani apewe adhabu ya kutoa fundisho, ambayo hatuweza tena kurejea tena suala hili.

Vile vile suala jengine kuhusu Idara hii ya Uendeshaji na Utumishi. Kwa kweli wizara zote kama walivyosema wenzangu idara hii inakuwa kila wizara inakuwepo na zaidi inatizama zaidi maslahi ya wafanyakazi.

Sasa Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri katika bajeti yake angalau kwenye maslahi hayo ni pamoja na suala la likizo. Kwa kweli likizo ni haki ya mfanyakazi, yaani kila anayefanyakazi ni lazima apate muda wa kupumzika, pia kuna sheria inasema hapa kwamba unapata zile *facilities* pamoja na familia yako. Kwa mfano, kama ni mume basi ni mke pamoja na watoto wako wanne, ikiwa ni mke ni wewe, mume pamoja na watoto wako wanne.

Lakini mpaka hivi sasa naona hupati kabisa, labda mtu anapewa shilingi 40,000/= ama 80,000/=. Kwa hiyo, sijui kama hata zitatosha hata kwa wewe mwenyewe kwenda na kurudi safari yoyote. Kutokana na hali hiyo, ili wafanyakazi wapate ile *moral* ya kufanyakazi, basi naomba suala hili kwa wizara zote ilitizame suala hili na wafanyakazi angalau wapate ile tija ya kufanyakazi na inapofika wakati wa kwenda likizo, basi likizo hii waipate kikamilifu.

Mhe. Spika, kwa kujali muda wako na vile nahisi kuna wenzangu wengi ambao wanataka kuchangia, basi nisiende deep sana. Hivyo, niseme tu hii *speech* ya Mhe. Waziri ni nzuri sana, imejaza kila kitu katika *Strategic Plans* zake, pamoja na malengo yake, kwa kweli wanaleta ufanisi katika wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Amani, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ndogo na mimi nitachangia kwa muda mfupi tu, kwa ajili ya kuheshimu wakati.

Mhe. Spika, kwanza nampongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri ya Mapinduzi ya Kilimo. Kwa hivyo, naomba nianze mchango wangu katika suala hili la Mapinduzi ya Kilimo.

Kwa kweli hivi sasa ulimwengu mzima unategemea sana chakula na matatizo makubwa ya dunia hivi sasa yanakwenda katika mfumo wa chakula. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kutaka kufanya Mapinduzi ya Kilimo. Hivyo, jambo la kwanza ni kujenga imani katika Mapinduzi ya Kilimo, kwa sababu bila ya kujenga imani hatuwezi kuwa na Mapinduzi ya Kilimo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wizara ihakikishe inashirikiana na wakulima kwa ajili ya kuwaelimisha. Vile vile ihakikishe inawalimia wakulima kwa wakati, kwa

sababu sisi Wazanzibari tunafeli sana katika kupata mazao bora kutokana na kuchelewa kulima. Kwa mfano, matrekta wakati ule ambao wakulima, basi matrekta hayajafika mabondeni, sasa inabidi mkulima atape shida ama atoe chauchau ndipo alimiwe. Sasa hali hii haiwezi kuleta Mapinduzi ya Kilimo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakulima wengi wanachelewa kulima kwa sababu hawana fedha za chauchau. Mhe. Spika, naiomba wizara ihakikishe mambo haya yanaondoka ndipo tutakapopata Mapinduzi ya Kilimo.

Pili maafisa wetu wawe karibu sana na wakulima kwa ajili ya kuwafahamisha ili wapate kulima kwa wakati.

Mhe. Spika, suala jengine na Mhe. Saleh Nassor Juma aliwataja waasisi, hivyo naomba na mimi kidogo kuwataja waasisi. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Nassor Moyo alipokuwa Waziri wa Kilimo kabla ya wakati wa kilimo haujafika alikuwa akikutana na wazee anashauriana na wazee jinsi gani ya kuimarisha kilimo kwa wakati, kwa sababu nchi yetu haya masuala ya *irrigation* ni kidogo na tunatumia sana mvua za kuletwa na Mwenyezi Mungu tu na wala hatuna irrigation kubwa. *(Makofi)*

Kwa mfano, kama kwenye bonde letu la Kihemarini Kaskazini "A" hakuna *irrigation* kubwa, isipokuwa *irrigation* ipo kwa serikali tu, lakini wakulima wengi hawana *irrigation*. Kwa hiyo, Mhe. Hassan Nassor Moyo alikuwa akikutana na wale wazee wanaojua miongo ya mvua, kama vile mara hii mvua itakuwa vipi, itanyesha vipi, sasa wale alikuwa akikutana nao mara kwa mara.

Sasa naiomba wizara yetu hii ya Kilimo na Maliasili ambayo inaongozwa na Mhe. Mansoor Yussuf Himid na yeye lazima afanye hivyo, yaani akutane na wazee wakulima wa zamani, ambao anahakikisha kuwa wanajua miongo ya kilimo, basi watashirikiana na maafisa. Hivyo, mambo yetu yatakuwa mazuri sana na kuliko kuwatupa wale wazee wa zamani ambao wanaojua ile miongo ya kilimo.

Mhe. Spika, nikizungumziea katika Jimbo langu la Matemwe lina sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ambao inalimwa mpunga Kikobweni, Pwanimchangani, Kandwi watu wa maeneo haya wanalima mpunga. Kwa hivyo, naiomba wizara watu hawa wapewe pembejeo mapema hata kukopeshwa matrekta wakopeshwe, kwa sababu wanaweza kutumia matrekta kama watapewa au kukopeshwa tena wanaweza kusaidiwa na maofisa au wafanyakazi wa kilimo kwa kuendesha wenyewe haya matrekta, kwa hivyo namuomba Waziri awakopeshe wakulima wangu hawa wa jimbo la Matemwe.

Sehemu ya pili ni sehemu inayotumia kilimo cha maweni kama vile mihindi, mtama, viazi vikuu, muhogo na migomba na tungule, Matemwe ilikuwa namba moja kwa kuleta tungule wakati huo tungule ya Matemwe inakuja mjini basi kila mtu wa mjini hanunui anakwenda zake tu pale anazoa, lakini hivi sasa kutokana na maharibiko ya hali ya hewa tungule za Matemwe siku hizi huzipati, naiomba Wizara ituletee wataalam watuhakikishe mbegu gani ambayo sasa hivi inaweza kuja Matemwe ili tuzipate zile tungule za Matemwe itajwe kama zamani. Maana yake mjini zamani wakisema tu Matemwe hiyo lakini sasa hivi haipo tena kwa hali ya hewa yetu sasa hivi tungele zile zinakufa, kwa hivyo naomba wataalam waje jimbo la Matemwe waje watuhakikishie mbegu gani ambayo inaweza kuja na sisi tukaleta mwamko kama ule wa zamani.

Mhe. Spika, naiomba wizara tena hivi sasa kuna ukulima wa viungo Matemwe inatoa ndimu nyingisana, kwa hivyo naiomba wizara pamoja na serikali kwamba iwatafutie soko la uhakika watu wa Matemwe wapate kuuza ndimu, ndimu Matemwe zinapozaliwa zinashinwa kuuza na watu wote wanajua kwamba Matemwe kuna ndimu nyingi sana, zikichanganyika na sehemu nyengine basi haziuziki. Kwa hivyo naiomba Wizara itufatutie soko la kuuza ndimu wananchi wa Zanzibar sasa hivi wanakosa fedha nyingi sana kwa kukosa soko la ndimu. Kwa hivyo Mhe. Spika, nasisitiza tena kwamba soko la viungo tutafutiwe wananchi wanatupa mali nyingi sana ya soko la ndimu hakuna.

Mhe. Spika, nakwenda kwenye embe Jimbo la Matemwe kijiji cha Kandwi kinatoa embe nyingi sana kuliko Muyuni, Muyuni sasa hivi imeshashindwa kwa hivyo naiomba Wizara iwatafutie wananchi soko la matunda, soko la matunda hivi sasa kwa kwetu ni muhimu sana mimi namngojea Mhe. Waziri wa Biashara atujengee viwanda, hapa namhimiza waziri wa kilimo atutafutie soko japo la nje kwanza ili lakini Waziri wa Biashara na Viwanda aje atujengee viwanda vya viungo hivi.

Mhe. Spika, nikimalizia suala langu hili namhimiza tena Mhe. Waziri wakulima wanalimiwa wakati sio wanachelewa au wanacheleweshwa, kwa hivyo wakati ule wa kulima tunaukosea. Namuhimiza tena Mhe. Waziri pamoja na maafisa wake wakihakikisha sasa hivi tayari wafike bonde la Kihemarini mapema na sisi tutakaokuwepo pale tutawasaidia fikra, mawazo hata misaada midogo midogo tutawasaidia sisi wawakilishi tutakuwepo na tutakuwa pamoja nao na tutashirikiana nao.

Mhe. Spika, nawahimiza tena maafisa washirikiane na wakulima wale wa zamani kwa sababu tunasema hivi isiyo kongwe haivushi, kwa hivyo na sisi tutumieni kongwe ndani ya kilimo sasa hivi tutumie wazee wa zamani wale watatusaidia sana.

Mhe. Spika, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Matemwe naiunda mkono hotuba hii mia kwa mia na nitaiunga zaidi na kuipa mia mbili pale nitakapopata vifaa vya matrekta kukopeshwa watu wa Matemwe. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, nikushukuru na mimi kwa kupata nafasi asubuhi ya leo kuweza kuchangia, lakini pia nimshukuru Mhe. Waziri kwa namna alivyowasilisha hotuba yake hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa na michango kama miwili mitatu tu kwa sababu kadri ninavyoangalia kitabu nahisi kwamba mambo mwaka huu yameleta matumaini, wakulima wengi wameanza kupata faraja baasa ya kusikia hotuba ya Mhe. Waziri, lakini nianze kwa mchango Mhe. Spika, kwa kutoa salamu za wakulima wa mananasi wa Donge. Wakulima wa mananasi wa Donge wanashukuru baada ya kipindi kirefu kutokupata kutembelewa katika kilimo chao, lakini baada ya jitihada za Mhe. Waziri kipindi kifupi baada ya kuingia madarakani tayari wameanza kupata matumaini baadhi ya maafisa kuwatembelea na kuwapa matumaini na changamoto katika kuimarisha kilimo chao.

Mhe. Spika, lakini pamoja na utembelezi huu bado wakulima hawa wanaiomba Wizara kwamba wasiache kuwatembelea mara kwa mara ili kutoa msaada na changamoto katika kuanzishwa kwa kilimo chao, lakini pamoja na hayo wanaomba basi suala la pembejeo wizara walipe kiapumbele ili kuweza kupata ufanisi wa kilimo chao. Mhe. Spika, pamoja na hali yote hiyo bado katika ukulima huu unaonekana kuna matatizo mawili matatu, moja nalo ni suala zima la kuhifadhi mazao lakini nashukuru Mhe. Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 16 ameelezea adhma ya wizara kwa kujenga *food storage facility* hii ni hatua ambayo inaonyesha mwelekeo mzuri na nina imani kwamba yatakapojengwa basi yale matatizo yaliyojitokeza huenda yakamalizika.

Lakini pamoja na hilo nimuombe Mhe. Waziri pamoja na ujenzi wa *food storage* bado kuna haja ya kushirikiana na Waziri wa biashara katika kuwatafutia soko wakulima hao wa mananasi, kwa sababu hataka kama ukihifadhi kama soko halijawa zuri basi unaweza kuhifadhi kwa muda mrefu pasipo na kuuza, Kwa hivyo kuna haja ya kuwasaidia wakulima hawa katika kuwatafutia soko la uhakika.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nilikuwa naomba nizungumzie katika suala zima la kilimo cha minazi katika kipindi cha karibuni suala la nazi Zanzibar limekuwa ni tatizo sugu, kwa hivyo kuna haja ya Mhe. Waziri kuandaa mikakati ya kutosha kuona suala la minazi nalo linapewa kipaumbele, kwa sababu kuna hatari kwamba huenda tukalima mpunga na mchele ukawa shilingi elfu moja lakini nazi ikaja ikawa moja shs. 1,500. Sasa bado itakuwa tatizo la kuondoshea

wananchi wetu usumbufu wa matumizi ya vyakula ikawa bado ni matatizo, kwani hivi sasa Mhe. Spika, nazi Zanzibar imekuwa ni tatizo kubwa sana na Wazanzibari wengi wamekuwa wanategemea nazi kutoka Tanzania Bara katika eneo la Mtwara.

Mhe. Spika, hali halisi tunaifahamu kama nazi sasa hivi inauzwa Sh. 700 na 800 basi ikifika ramadhani sijui itauzwa kiasi gani, kwa hivyo ili kuondosha matatizo kwa miaka ya mbele kuna haja ya wizara kuandaa mikakati mizuri katika suala la upandaji wa minazi.

Mhe. Spika, nikitoka hapo kwa haraka haraka nilikuwa nataka kuzungumzia suala la pembejeo nishukuru Mhe. Waziri amelielezea vizuri suala la pembejeo, amejipanga vizuri nina imani kwamba tatizo hili huenda likatuondokea lakini nilikuwa napenda kutoa tahadhari katika hili Mhe. Waziri lazima aandae kwa kikamilifu nchi yetu ni kisiwa na mara nyingi nchi hii panapokuwa pana kitu ambapo pana wepesi wa kuuzwa basi wafanya biashara kwa kuwa ni watu wanaoangalia maslahi yao zaidi kuliko maslahi ya wananchi. Hofu yangu pembejeo hizi zisije zikasafirishwa nje ya Zanzibar baada ya kuonekana ziko nyingi na hatimae ikaleta usumbufu kwa serikali katika manunuzi yake na kuondosha ile taswira ya kusaidia wakulima, kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri pamoja na jitihada alizozifanya na mikakati yake bado aandae na mikakati ya kuweza kudhibiti suala la usafirishaji wa pembejeo pendipo zinataka kuingia katiak nchi yetu.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie katika eneo moja ambalo nimepata taarifa upande wa kaskazini kuna shamba la Selem Mhe. Rais wa kwanza Mzee wetu Marehemu Shehe Abeid Amani Karume baada ya mapinduzi matukufu aligawa maeneo mbali mbali ya mashamba kwa wananchi wa Zanzibar, kwa heka tatu tatu na baadhi ya maeneo Mhe. Spika, yakabakia mikononi mwa serikali lakini kuna taarifa kwamba kuna shamba la serikali la Selem shamba hili limegawiwa kwa wananchi mbali mbali. Pamoja na kugawiwa kwake imeonekana kwamba waliogaiwa hawalilimi na baadhi ya wananchi wanalihitaji kwa kutaka kulima hilo eneo.

Sasa hapa Mhe. Spika, nikitaka kusaidiwa taarifa na Mhe. Waziri kwamba kweli hizi taarifa ni za uhakika, na kama ni za uhakika ni nani ambae amepewa shamba hili kwa ajili ya hizo shughuli na wanalima nini, lakini pamoja na ulimaji huu ningepata pia Mhe. Waziri anisaidie ugawaji huo waliopewa hawa wananchi walipewa heka ngapi ngapi na kweli eka walizopewa zinastahiki kupewa, katika hili miongoni mwa waliogaiwa kuna taarifa kwamba ni mwananchi mmoja tu ndie ambae amegaiwa kwenda sambamba na kauli ya Mheshimiwa wa kwanza wa eka tatu tatu huyu ni mwanamama ambae inasemakana kwamba kapata hizo heka tatu na mwanama huyu hilo shamba la Selem wananchi wanampigia mfano tosha kwamba yeye ndio anaonekana

anatumia lile lengo na dhamira ya kupewa hizo heka tatu, yeye analima sana na inavyosemekana kila wikiendi basi shambani hatoki kwa kulima.

Sasa ni vyema na wale ambao kama kuna watu wamepewa wakaiga mano wa huyu mwanama ambae amekabidhiwa kulima katika shamba hilo la Selem, lakini kama kuna wengine ambao wamepewa basi ningeomba nao tutajiwe ni nani na nani ukiachilia huyu mwanamama ambeye sipendi kumtaja lakini ni mwanamama ambae ana sifa kubwa sana kwa ukanda wa kaskazini.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka nimalizie tu kwa kumuomba Mhe. Waziri punde tu tunategemea kukabiliwa na ufunguzi wa Mwezi wa Ramadhani na idadi ya watu wa Zanzibar asilimia 90 ni waislam, kila inapofika ramadhani kumejitokeza tabia kwa wafanya biashara kuweza kuongeza bei maradufu za mazao, nimuombe Mhe. Waziri wa Kilimo kwa kushirikiana na Waziri wa Biashara na Viwanda kujitahidi kukabiliana na wafanya biashara katika suala la kukabili mwezi mtukufu wa ramadhani kwa kutokupandisha bei kiholela ili kuwapunguzia ukali wananchi wetu wa Zanzibar.

Lakini pia nimuombe Mhe. Waziri kutumia jitihada tosha kwa wale ambao wana kawaida kwa mwezi huu mtukufu wa ramadhani kuvuna mazao machanga na matunda ambayo hayajapea na kuanza kuyapiga moto kuwaletea wananchi kwa ajili ya kadhia ambayo inawakuta katika kipindi cha mwezi mtukufu wa ramadhani.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru kwa dhati na niseme kwa niaba yangu na wananchi wa jimbo la Kwahani naunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii naanza kwa kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kutokana na mwelekeo wake wa kufanya mapinduzi ya kilimo katika utendaji wake huu wa serikali ya awamu ya saba, lakini vile vile nampongeza Mhe. Rais kwa kumteua Mhe. Mansour Yussuf Himid kwa kusimia wizara hii ambayo ina changamoto kubwa sana ya kuleta mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, hotuba imetupa matumaini makubwa na imetupa matumaini kwamba tunahitaji kufanya mapinduzi ya kilimo katika uchumi wa nchi yetu na katika kuondosha umasikini wa wananchi wetu, kutokana na sababu mbili kubwa kwamba kilimo ni ukweli kwamba kinachukua asilimia 70 ya wananchi wanaokitegemea, lakini vile vile tunahitaji kufanya mapinduzi ya kilimo kwa sababu tunahitaji mahitaji yetu ya chakula hasa kwa vyakula vile ambavyo vinatumika kwa muda mwingi na mara nyingi sana huwa vinapatikana kwa njia ya uwagiziaji kutoka nchi za nje. Tunafahamu athari ya uagizaji wa chakula

kutoka nje ya nchi ni mara nyingi husababisha mfumko wa bei ambao huathiri sana maisha ya wananchi.

Kwa hivyo ni lazima kwa sababu hizo mbili kwamba kilimo kinategemewa na sehemu kubwa ya wananchi, lakini vile vile katika kuwawezesha wananchi na katika kupunguza mfumko wa bei katika zile bidhaa muhimu ni lazima tufike pahala tuwe na mapinduzi ya Kilimo ya kikweli kweli, kama alivyosema Mhe. Waziri katika hotuba yake hii kwaba kilimo chetu kinakabiliwa na changamoto kubwa kama alivyoeleza katika ukurasa wa 67 katika kifungu cha 165. Kaeleza changamoto ambazo zitaathiri mageuzi hayo ambayo amekusudia kuyafanya, kati ya changamoto hizo alizozitaja zinahitaji ufumbuzi ili adhma ya serikali iweze kufikiwa.

Mimi nataka nijikite katika eneo moja kubwa na muhimu katika kukabiliana na changamoto alizozieleza Mhe. Rais kwa sababu waswahili wanasema mipango sio matumizi, Mhe. Waziri kaja katupa mipango mingi mizuri lakini hii ni mipango tu ukija kwenye utekelezaji wake hapo ndio penye wasi wasi wangu hizo zinatokana na changamoto kubwa ambazo zinatukabili na ambazo amezitaja ni uwezo wa wizara kibajeti. Mhe. Waziri kadiri tutakavyopanga ikiwa hakuwa na uwezo itafika pahala mipango yote hii itazidiwa na changamoto hizi ambazo kazitaja, sasa utekelezaji wa *program* changamoto hizo ambazo zinategemeana sana na uwezo wa wizara katika bajeti yake.

Mhe. Spika, tukiangalia katika bajeti ya mwaka jana utekelezaji wake katika miradi pamoja na *program* zote za wizara hakuna hata moja iliyotekelezwa kwa asilimia mia moja, sasa ikiwa bajeti ya mwaka jana haikuweza kutekelezwa kwa asilimia mia moja na kwa kuwa katika bajeti ya mwaka huu imeelekeza au imeashirika kufanya ongezeko la bajeti, kwa mfano kama program ya huduma za kilimo Mhe. Spika, imeongezeka bajeti yake wakati haikutekelezwa kama ilivyotakiwa lakini imeongezeka kwa asilimia tano, miradi ya uhakika wa chakula na lishe imeongezeka kwa asilimia 59, mradi wa ushirikishwaji wa maendeleo ya kilimo imeongezeka kwa asilimi 6, mradi wa HIMA umeongezeka kwa asilimia 74, mradi wa kukuza usarifu wa mazao kwa asilimia 10 na Mradi wa Kilimo cha Kisasa cha kuendeleza kilimo na bajeti ya mwaka huu imeongezeka kwa asilimia 76.

Mhe. Spika, hapa ndio penye tatizo langu kubwa na ndipo panaponipa wasi wasi kwamba ni kwa kiasi gani tutaweza kufikia malengo haya aliyoelezea, kama ilivyoelezwa kwamba malengo yetu ya Mapinduzi ya Kilimo yanahitaji sana kufanya kilimo cha umwagiliaji, mradi mkuu katika kilimo cha umwagiliaji katika bajeti iliyopita SMZ haikutenga fedha, wahisani walitenge milioni. 731 lakini utekelezaji wake walitekeleza kwa kutoa milioni 116 sawa sawa na asilimia 15.

Sasa tuangalie namna ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana ikiwa mwaka jana SMZ haikutenga wahisani ndio walioahidi na utekelezaji wake ulikuwa ni kwa asilimia 15 kwa hivyo hilo litakuwa ni changamoto kwenye changamoto, mradi wa kilimo cha kisasa cha uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji maji katika kipindi kilichopita SMZ ilitenge shilingi milioni 200 lakini imetoa asilimia 92 ikiwa ni asilimia 46 na wahisani kwa hapa tunawashukuru waliahidi kutoa milioni 137 na wakatekeleza kwa asilimia 100 hapo tunawashukuru sana.

Suali sasa ikiwa bajeti ya mwaka jana na mwaka huu, mwaka jana serikali ilitenga shilingi milioni 200 mara hii imefanya ongezeko la asilimia 86, lakini utekelezaji wake mimi ndio unaonipa hou, sasa nalizungumza hili katika suala zima. Najua hili sio suala la Mhe. Waziri lakini Mhe. Waziri kazi yake ni mipango lakini itakuwa ni suala la serikali kuona kwamba tunatekeleza sera muhimu sera ya kilimo. Kama nilivyotangulia kwamba kilimo kina umuhimu mkubwa sana katika suala la uchumi wa nchi yetu.

Kwa hivyo naiomba serikali imuweeshe Mhe. Waziri, vyenginevyo mipango yake yote mizuri kwa kweli mwaka kesho mungu akitujaalia tutakuja kuvutana mashati kwasababu utekelezaji wa bajeti na malengo ya serikali yaliyowekwa hayakuweza kufikiwa, na wawakilishi hatuwezi kukubali serikali kupanga mipango iliyokuwa haiwezi kutekelezeka, bajeti ya mwaka huu hakuna tatizo kwa sababu ni bajeti mpya kishindo tukijaaliwa kitakuja kuwa mwakani juu ya kuandalia utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu.

Nikitoka kwenye bajeti katika mambo ya mahesabu sasa naomba kwa ufupi kwa sababu ya muda wako Mhe. Spika, naomba niseme tu kwamba mapinduzi ya kilimo yanakabiliwa na changamoto ya ardhi, sasa kama hivyo ndivyo lazima tukubali kwamba ardhi yetu Zanzibar ni ndogo na ardhi hiyo hiyo ndogo tutaihitaji kwa ajili ya mambo ya kujenga na mambo mengine ya maendeleo, tumezowea tumesikia karibuni kuna nchi ya Malaysia baada ya nchi yao kuingia michikichi wamekwenda kukodi ardhi katika nchi ya Indonesia, sasa kama hilo ndilo serikali inaweza kuwekeza upande moja wa nchi na kuweza kuwekeza upande mwengine kwa ajili ya kilimo. Mimi niulizie ile hatima ya shamba letu la Bagamoyo kwa sababu kama ikiwa tutaitumia ardhi ile ya Bagamoyo hicho kipande tulichobakishiwa tunaweza kufanya mambo mengi sana kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha nchi hii. Kwa hivyo niulize hatma ya ardhi ile ya Bagamoyo imefikia pahala gani.

Lakini la pili Mhe. Waziri tunakabiliwa na changamoto ya ardhi tuna mashaka mengi ya serikali lakini bahati mbaya mashamba ya serikali yamekuwa na uvamizi mkubwa, ripoti za mkaguzi na mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali zimeainisha hilo masalam kuna uvamizi mkubwa sana katika mashamba ya Selem, Kidichi, Kizimbani, Wenu tumekwenda tayari kule watu wameshagawiyana viwanja na kamati tumekwenda tukaliingilia suala lile lakini

hatima yake hatujajua pamoja na shamba la Mziwanda. Mhe. Waziri namuomba atakapokuja aeleze namna ani serikali imechukua juhudi na hatua gani zimechukuliwa na serikali katika kurejesha mashamba yale katika mkono wa serikali.

Mhe. Spika, nakumbuka mwaka juzi Mhe. Rais wa Zanzibar wa Serikali ya awamu ya sita katika kuendeleza kilimo alitaka viongozi lazima wawe mfano katika hilo, alitoa agizo kwamba wajumbe wote wa Baraza la wawakilishi wawe ni mfano wa kulima na akatoa agizo kwamba wawakilishi wote wakatiwe mashamba ili wawe ni mfano, sasa utekelezaji wa agizo lile na kwa sababu Mhe. Spika, wawakilishi wako wengi tu tutataka kujielekeza katika sekta hii ya kilimo. Sasa namuuliza Mhe. waziri utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais wa awamu ya sita imefikia pahala gani.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri tunampongeza sana kwa kitendo cha kupunguza mbolea na pembejeo za kilimo, lakini tuangalie pamoja na uzuriwa kupunguza hivyo kwa maslahi ya maendeleo ya kilimo tuangalie na ile dhamira yetu ya kusafirisha matunda katika nchi za nje, kuna nchi zinaendelea sana katika usafirishaji wa matunda. Nchi yetu ya Zanzibar ni mzalishaji mkubwa wa matunda hasa embe juzi nilipata taarifa wa Philipin kila mwaka husafirisha nje embe zenye thamani ya dola zaidi ya milioni 200 kwa kila mwaka, ni bahati mbaya kwamba sisi tuna embe nzuri na zenye koliti nzuri kabisa hatujafikia hatua hiyo na ndio azma ya mapinduzi haya ambayo tunakusudia kuyafanya.

Lakini tuangalie haya matumizi ya mbolea hasa haya ya kemikali haiwezi kutuathiri katika azma yetu hiyo Mhe. Waziri atakapokuja kidogo atupe elimu hasa wawakilishi katika azma hii, karibuni tulipata taarifa kwamba kuna nchi moja hapa sijui Uturuki au nchi gani kuna kesi iliyojitokeza kwenye vitango ikawa ni balaa kubwa sana kwa biashara ile ya vitango, sasa Mhe. Waziri atakapokuja naomba atupe maelezo katika hilo.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nchi yetu bado narudia kwamba ina changamoto kubwa sana la ardhi na ardhi tuliyonayo imepandwa sehemu kubwa sana ya ardhi yetu hasa Pemba imepandwa sana kilimo cha zao la Mpira, ukienda maeneo ya Maziwani, Finya, Makangale kule ardhi kubwa imekuwa kwenye mazao haya ya mpira, Sasa Mhe. Waziri atakapokuja atupe elimu hasa hii mipira inaingiza kiasi gani katika pato letu. Kwa sababu kama ikiwa ni miti tu ipo kwa ajili ya utunzaji wa mazingira tufike pahala tufanye shauri jengine kama ikiwa haina faida yoyote ambayo nchi inanufaika kutokana na zao lile la shamba ya mipira.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja pamoja na mambo mengine lakini aje atupe ufafanuzi ni pamoja na nchi inafaidikaje na zao lile, kwa sababu kama ikiwa haina faida basi ni vyema tuikate tupande mkarafuu ambao

unaonekana una tija kwa maslahi na uchumi wan chi. Mhe. spika, kwa kuheshimu muda wako kwa mara ya kwanza kabisa na kwa kuzingatia mchango wa Mhe. Mansour Yussuf Himid katika mageuzi haya naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Kama nilivyosema niwaombe waheshimiwa wengine walioomba ingawa wengi hawapo waniwe radhi muda wetu uko finyu mno.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafsi, lakini pili niseme naunga mkono hoja hii mia kwa mia na kuwaomba wenzangu wote tuunge mkono hoja hii na tuipitishe mapema ili Jumapili ya leo tuweze kufanya shughuli nyengine.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na kututayarishia hutuba hii ya bajeti vizuri sana, hongereni sana watu wa kilimo kwa kazi hii nzuri sana.

Aidha nichukue fursa hii kumpongeza Mhe.Rais wetu Dk, Ali Mohammed Shein kwa kuanzisha kaulimbiu ya mapinduzi ya kilimo, Rais wetu ameleta kauli hii kwa makusudi baada ya kuelewa kwa kina matatizo ya kilimo na nia yake ni kuyaondoa matatizo hayo ya kilimo kwa nia ya kuimarisha sekta hii ya kilimo. Madhumuni makubwa ya Mapinduzi ya kilimo ni kuhakikisha kwanza kuwa na usalama wa chakula na kuongeza uzalishaji, pamoja na kuongeza kipato cha wakulima wetu. Kuhakikisha malighafi zinazotokana na bidhaa hizi za kilimo zinatumika katika kupanua viwanda nchini. Kuhakikisha tunawepesisha upatikanaji wa mikopo, mitaji, elimu kwa wakulima na matumizi bora ya ardhi. Kwa ufupi alikusudia kuhakikisha tunapambana na kila tatizo linaloikabili sekta hii ya kilimo ili tuwe na kilimo bora, chenye tija na chenye kipato kwa watu wetu. Kwa hiyo lazima tuchukue kila jitihada za kuunga mkono kauli mbinu hii na kumuunga mkono waziri na wizara yote ya kilimo kwa jitihada ambazo wanazichukua katika kupambana na kuimarisha kilimo nchini.

Mhe. Spika, kilimo kina mambo makubwa matatu.

1) Maji
2) Utafiti na utaalamu,
3) Zana za kisasa zikiwemo na pembejeo.

Mhe. Spika, kwa kweli wizara hii imeona matatizo haya. Jambo la kwanza tatizo letu kubwa ni kilimo hichi cha kutegemea mvua, kitu ambacho kinatupa matatizo makubwa sana. Wizara imejipana katika mambo mawili makubwa na

inafaa nimpongeze waziri na watendaji wake kwa kuleta mpango huu wa kilimo cha umwagiliaji.

Mhe. Spika, lilikuwa ni tatizo la siku nyingi. Wengi tumepitia kilimo lilikuwa hili kwetu ni jambo kubwa na gumu kulikamilisha. Mimi nataka ni wapongeze sana watu wa kilimo kwa kuweza kukamilisha mpango huu mkubwa wa umwagiliji ambao utakuwa mkombozi wa kilimo chetu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, la pili katika jambo moja ambalo wamelifanyia kazi kubwa ni kudhibiti uharibu wa mazingira hasa katika ukataji wa miti. Tunapokata miti tunapunguza kabisa kupatikana kwa mvua ambayo kwa kiasi kikubwa tunaitegemea kwa kuendeshea kilimo chetu. Pia inasababisha ukame na athari kubwa zinatokea katika kuimarisha kilimo chetu. Jitihada wanazozichukua za kudhibiti uharibifu huu wa mazingira lazima tuwaunge mkono hasa hili shauri ambalo wamekuja nalo, shauri la nishati mbadala. Kwa maana sasa tupunguze matumizi yetu ya kuni na tutumie gesi kwa matumizi yetu ya nyumbani kwa kupikia. Kwa sababu, moja katika tatizo kubwa sana linalosababisha kukatwa kwa miti ni suala zima la kuni. Utaratibu ambao wamekuja nao ningependa niwatolee wito kwa wananchi wenzangu tuunge mkono ili tutumie gesi kama nishati mbadala, kwa ajili ya kuhifadhi miti yetu hii itusaidie katika upatikanaji wa mvua na kuhifadhi vianzio vya maji, ili tuweze kuimarisha kilimo chetu. Nina hakika tukiitumie vizuri ardhi yetu tukafuata maelekezo waliyotueleza, basi kwa kiasi kikubwa tutaepukana na athari hii kubwa ya ukataji wa miti na tutaweza kuimarisha zaidi kilimo chetu.

Mhe. Spika, wenzetu wamekuja na suala la utafiti, utaalamu na teknolojia ya kisasa. Kitu ambacho kitatusaidia kuimarisha kilimo chetu, hasa kwa kuwa na matumizi ya mbegu bora, mbolea, pembejeo, maofisa ugani, kutoa elimu kwa wakulima na kuimarisha vituo vya kilimo hata chakula ambacho Mhe. Mwakilishi alikizungumzia hapa. Kwa hiyo, mambo haya ambayo wao wamekuja nayo ni wajibu wetu sisi wawakilishi kuwahamasisha wananchi wenzetu kuhakikisha kwamba huu utaratibu ambao wanatushauri tukauunga mkono ili tupate maslahi ya kilimo chetu.

Mhe. Spika, sasa wakati umefika kabisa kabisa kujenga ushirikiano kati ya watafiti wetu, wakulima na maofisa ugani, ili teknolojia iliyo bora tuipate sisi wakulima itusaidie. Kadiri tunavyojitahidi kushirika katika semina mbali mbali, kusikiliza vipindi vya redio na maelekezo mbali mbali yanayotolewa na maafisa wetu wa kilimo itatusaidia sana kuimarisha kilimo chetu. Kwa hivyo ni wajibu wetu sisi, hasa sisi wawakilishi tutakapotoka hapa tukarudi nyumbani kwenye majimbo yetu kuhamasisha wananchi wetu kuona umuhimu huo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo amelizungumzia ambalo serikali yetu imejipanga kupitia wizara hii ni suala la kuimarisha zana za kisasa za kilimo.

Lazima tuunge mkono jitihada hizo na sekta binafsi, wale wenye uwezo wajitokeze kuunga mkono jitihada za serikali kwa kuwa wao wana uwezo wa kununua matrekta na zana nyengine za kilimo ili na wao kuanzisha ikiwa ni kukodisha ikiwa ni kuanzishwa vituo vya kilimo kwa kushirikiana na serikali ili tuweze kuongeza wigo zaidi wa kuimarisha jitihada hizi za kuwa na zana za kisasa.

Naamini uwezo upo na wizara yetu mikono ipo wazi ya kusaidia na kushirikiana na sekta binafsi ili kuimarisha jambo hili. Ili tuwe na udhibiti mzuri wa zana za kilimo na waweze wananchi wetu kupata unafuu badala ya kutumia jembe la mkono, ambapo kwa kiasi kikubwa linapunguza juhudi zetu za kilimo. Yapo maeneo tutalihitajia, lakini kwa vyovyote vile tunahitaji kubadilika na kuwa na zana za kisasa.

Nia kubwa Mhe. Spika, ni kuongeza uzalishaji ili uzalishaji uwe mkubwa. Serikali imesema, nimewasikia wawakilishi wenzangu wakihamasisha sana jambo hili. Suala la kusindika bidhaa hizi za kilimo. Serikali imejipanga na imeanza kuhamasisha sana wawekezaji mbali mbali wajitokeze katika kusindika mazao haya ya kilimo kwa nia ya kuongeza juhudi za wakulima wetu. Lakini pia kwa nia ya kuhamasisha upotevu wa mavuno unaotokea baada ya mavuno. Kadiri tutakavyoimarisha kusindika bidhaa zetu maana yake tunaongeza jitihada za kuhamasisha wakulima wetu wajitokeze kwa wingi kwa sababu kipato kitaongezeka hasa kwa ile dhana ya uharibifu wa mazao baada ya mavuno.

Lakini kubwa zaidi ambalo napenda sana niipongeze wizara hii ni jitihada za kuwatafutia mikopo wakulima ili kuongeza mitaji yao katika kujiimarisha katika jitihada hizo za kilimo. Mheshimiwa serikali kwa undani imeangalia mambo yote haya na yale manung'uniko ya siku nyingi ya soko la bidhaa hizi za kilimo kwa kiasi fulani Wizara hii imetuonesha ni kilimo gani kinatusaidia ambacho hakitokuwa na tatizo la soko.

Kwanza wizara imetuhamasisha tulime mpunga ambalo soko lake liko wazi. Tumehamasishwa tulime mboga mboga ambalo soko lake nalo lipo wazi. Wametuhamasisha tulime matunda soko lake liko wazi. Kukuza kilimo cha biashara na hasa karafuu. Hapa nataka nimpongeze sana Waziri wa Kilimo na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuongeza bei ya karafuu. Sasa nina hakika wakulima wataitikia wito huo kwa kuuza karafuu zao serikalini kwa *ZSTC* ili tuzidi kuongeza nguvu ya kuimarisha bei kwa ajili ya wakulima wetu. Naomba wadau sote tushirikiane tuunge mkono bajeti hii ili tumuwezeshe waziri wetu na watendaji ili kuweza kutekeleza haya waliyoyaahidi. Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii, nawatakia kila la kheria wizara hii. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri nilikuwa nina maombi ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano lakini hayupo. Pia nilikuwa na maombi ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, lakini na yeye pia hayupo. Basi moja kwa moja nimkaribishe Mhe. Waziri wa Kilimo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa mara nyengine tena kutujaalia sote uwezo wa kuwepo hapa kwenye Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar.

Pili nikushukuru Mheshimiwa kwa kunipa nafasi hii kufanya majumuisho ya hotuba ya Wizara yangu kwa mwaka huu wa fedha. Niwashukuru pia wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao ambayo imetuelekeza, imetushukuru, imetupa moyo na imetuongoza.

Mhe. Spika, Wizara yangu imechangiwa na jumla ya wajumbe 36, kati ya hao 14 wamechangia kwa maandishi. Kwa idhini yako Mhe. Spika, naomba kuwataja.

1) Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambaye hotuba yake imesomwa na Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa wa Jimbo la Kikwajuni.
2) Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa
3) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4) Mhe. Asaa Othman Hamad
5) Mhe. Mohammed Haji Khalid
6) Mhe. Rashid Seif Suleiman
7) Mhe. Raya Suleiman Hamad
8) Mhe. Ismail Jussa Ladhu
9) Mhe. Mussa Ali Hassan
10) Mhe. Abdalla Juma Abdalla
11) Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
12) Mhe. Saleh Nassor Juma
13) Mhe. Jaku Hashim Ayuoub
14) Mhe. Mbwana Mohammed Hamad
15) Mhe. Suleiman Hemed Khamis
16) Mhe. Farida Amour Mohammed
17) Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak
18) Mhe. Fatma Mbarouk Said
19) Mhe. Abdii Mossi Kombo
20) Mhe. Ali Salim Ali
21) Mhe. Omar Ali Shehe
22) Mhe. Mohammed Aboud Mohammed

Waliochangia kwa maandishi ni
23) Mhe. Nasor Salim Ali

24) Mhe. Shadiya Mohammed
25) Mhe. Mgeni Hassan Juma
26) Mhe. Bihindi Hamad Khamis
27) Mhe. Salma Mohammed Ali
28) Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
29) Mhe. Kazija Khamis Kona
30) Mhe. Salim Abdalla Hamad
31) Mhe. Issa Haji Gavu
32) Mhe. Bikame Yussuf Hamad
33) Mhe. Hija Hassan Hija
34) Mhe. Dk. Sira Mamboya
35) Mhe. Ashura Sharif Ali
36) Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

Mhe. Spika, nianze kwanza kumshukuru sana Mhe. Mohammed Aboud Mohammed Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, ambaye amenisaidia kutoa majibu ya baadhi ya hoja zilizozungumzwa na wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa kutumia uzoefu wake kwenye wizara hii na uzoefu wake wakiwa kiongozi na mjumbe wa Baraza la Mapinduzi. Namshukuru sana amezungumzia masuala ya pembejeo, umuhimu wa zana za kisasa na namna serikali ilivyojipanga, amezungumzia masoko, amezungumzia masuala ya mboga mboga, viungo na maeneo muhimu ambayo wajumbe wengi waliyagusia.

Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wajumbe wako wengi wamezungumzia eneo moja au zaidi wakiwa wote wameyazungumza yale yale. Kwa mnasaba huo naomba uniruhusu nende moja kwa moja kwenye maeneo ambayo yamezungumzwa na wengi. Kwanza ni suala la nzi wa matunda. Mhe. Spika, walihitaji kujua waheshimiwa wajumbe mafanikio tuliyoyapata katika maeneo ambayo tumesambaza mitego hii. Baina ya mwaka uliyopita na huu maeneo ambayo tumesambaza mitege tuna mafanikio kati ya asilimia 57, kwa maana athari imepungua kutoka asilimia 70 mwaka 2009/2010 kupungua hadi kufikia asilimia 57 mwaka 2010/2011. Wengi wameonesha hofu juu ya mipango ya serikali na namna tulivyoweza kufanikisha tatizo hili. Tunafanya kazi kwa maeneo mawili kama nilivyozungumza kwa kina katika kitabu changu.

Mhe. Spika, tunashirikiana katika progarmu ya kikanda na Shirika la Nguvu za Atomiki dunia kukabiliana na tatizo hili. Hili sio tatizo la Zanzibar peke yake na wala hatuwezi kulimaliza sisi peke yetu. Kama alivyozungumza Mhe. Rashid Seif baina ya wilaya na wilaya hakuna pazia, baina ya Zanzibar na Bara hakuna pazia, baina ya Bara na Uganda hakuna pazia na baina ya Uganda na Kenya hakuna pazia. Tatiza la kikanda ni lazima tukabiliane nalo kikanda. Nimeeleza kwa kina namna tulivyokabiliana na tatizo hilo kikanda ndani ya kitabu changu. Mwaka huu tutasambaza mitego 42,000 wilaya zilizobakia kwa

maana kwamba hazikupata huduma hii ikiwemo Kaskazini ‘A’ na ‘B’ kama mlivyouliza kwa Unguja na kuendeleza katika Wilaya ambazo tayari kazi hiyo tumeifanya na mwaka huu huu tunategemea tufike mitego laki moja katika nchi yetu ili katika jitihada ya nchi yetu kupambana na tatizo hili.

Mhe. Spika, jambo ambalo pia tunalizingatia na kuwashajihisha wakulima kushirikiana na sisi kwa kutumia mbinu asili, kwa kutumia miti shamba na mbinu nyenginezo ambazo wataalamu wetu wanaendelea kuzifanyia kazi. Kwa hivyo tatizo hili tunakabiliana nalo kwa namna hiyo naamini tukipata mashirikiano na wakulima wetu tutafikia hatua nzuri kama mabadiliko yalipoanza kuonekana katika msimu huu wa matunda yetu. Sasa maembe tunayapata, ndizi tunazipata, sisemi kama tatizo halipo, tatizo lipo tunahitaji kuongeza nguvu na tutaendelea kufanya hivyo.

Mhe. Spika, misumeno ya moto na tamko la serikali kuhusiana na tatizo hili. Nimeeleza kwamba tumeshakamilisha kanuni ambazo zinatoa muelekezo juu ya namna ya usimamizi wa mitumizi ya misumeno ya moto nchini mwetu. Baada ya hapo tumeshampelekea Mhe. Mwanasheria Mkuu akishakuziona, akishakuzithibitisha, zikishakutangazwa, serikali itatoa tamko rasmi juu ya muelekeo wa nchi yetu kwenye usimamizi na matumizi ya misumeno ya moto.

Hivi sasa kupitia maswali na majibu nilieleza hapa tunaendelea na udhibiti na mengi sana tumeikamata, tutaiangamiza na wengi wametozwa faini kwa kutumia misumeno ile kinyume na utaratibu. Mhe. Spika, hapa pamezungumzwa je, serikali inayo uwezo wa kusimamia mageuzi ya mapinduzi ya kilimo hasa ongezeko hili la ruzuku ambalo tumelizungumza?

Mhe. Spika, niwaombe sana wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kuwajulisha kwamba serikali inaelewa na wizara inaelewa kwamba haya mageuzi ya kilimo, mapinduzi ya kilimo si kazi nyepesi na ni kazi endelevu. Ndio maana mpango huu wa kilimo cha mpunga peke yake ni wa miaka mitano mfululizo. Lakini niwaombe sana wajumbe wa Baraza hili tukufu, tuondoshe huu utamaduni wa kuwa kila jambo hatuliwezi. Kwa nini iwe hivyo?

Mhe. Spika, Zanzibar tunaumasikini wa kipato lakini yale pia si maradhi. Hatuna umasikini wa fikra, hatuna umasikini wa uwezo, hatuna umasikini wa kwamba tunapopanga kukamilisha. Nani ambaye alidhani kwamba tutaweza kujenga mabarabara tuliyoyajenga? Nani alidhani kwamba umeme utafika Pemba? Nani alidhani kwamba umeme tutafika Tumbatu? Lakini tumeyaweza. Tuliyaweza kwa sababu tumeshirikiana, tuliyaweza kwa sababu tulidhamiria. Sasa nataka niwahakikishie serikali inaelewa ugumu wake, serikali imejipanga vizuri.

Hapa nataka nimshukuru sana Raisi wetu, kwamba yeye tayari katika hii mipango yetu yupo hatua moja mbele zaidi. Hivi punde nilikuwa nazungumza na Mhe. Omar Yussuf ambaye na yeye namshukuru sana kwamba tayari kuna mambo ambayo sisi tumeyazungumza hapa, tuekelezaji wake umeshapangwa na punde tu tutaanza kuuona sasa hizo zana tunazozingumzia kuanza kumiminika ndani ya nchi yetu. Kila ninapopita kwa wakulima niliwaambia kwamba kuna mabadiliko mengine tutayaona kwa mara moja. Lakini wajumbe ni lazima tufahamu kwamba tunapozungumzia umwagiliaji wa hekta 2000 huwezi kuwekeza umwagiliaji wa hekta 2000 ndani ya mwezi mmoja. Mradi ule utaanza lakini utekelezaji wake utakuwa wa miaka mitatu.

Tukiingia kwenye *USID* uwekezaji katika umwagiliaji wa hekta 2000 hauwi kwa mwaka mmoja. Tumepanga tunaingia katika utaratibu wa utekelezaji, kuna mambo mengine sio ya siku moja, sio ye miezi miwili, si ya mwaka mmoja, yatachukua zaidi ya hapo. Tumeeleza kwenye kitabu chetu kwa hivyo tuna mipango ya sasa ya muda mfupi na ya muda mrefu. Nimeshawambia wakulima huko kila ninapowaona kwamba wawewastahamilivu mengine yatakuja na tutawaeleza.

Zao la karafuu hili tumeshalizungumza sana. Tumesema kwamba serikali imeliona tatizo la karafuu Mhe. Nasor Ahmed Mazrui Waziri wa Biashara atakuja kueleza kwa kina nini mipango ya serikali kuanzia uatikaji ya miche, uhifadhi wa miche, upandaji wa mikarafuu, uhifadhi wa mikarafuu, ulezi wa mikarafuu, bei za karafuu, kutakuwa na sheria na kanuni zitakazokabidhiwa ZSTC kuanzia siku ya mwanzo ya mkarafuu mpaka hatima yake. Kwa hivyo karafuu sasa itakuwa na mwenyewe kwa sehemu zote hizo. Mafunzo kwa wakulima ya kila aina, hayo yote yatakuja kuelezwa na Waziri husika. Mimi nimeeleza wizara yangu inamsaidia vipi. Halkadhalika na masuala ya minazi. Hilo nalo ni jambo la lazima kama tulivyofanya kwa upande wa karafuu minazi nayo halkadhalika itashughulikiwa.

Kunabaadhi yapa wamezungumza kwamba tunawekeza sana kwenye kilimo na hakuna nchi iliyoendelea kwa kutegemea kilimo. Si kweli hakuna nchi iliyoendelea bila ya kutegemea kilimo. Hata nchi zilizoendelea. Wakati tupo na bibi Hilali Clinton wao wenyewe Wamarekani walilisema hilo, kwamba misingi ya wao kuendelea ni kilimo. Lakini ni kilimo cha aina gani? Sio kilimo cha jembe kongoroka, kilimo kinachotumia zana za kisasa, ardhi ndogo, tija kubwa zaidi, usarifu wa mazao, viwanda vya usindikaji na matumizi ya malighafi nyengine inayotokana na kilimo kwenye viwanda. Kwa hivyo hayo yamo kwenye mipango ya serikali na yatatekelezwa.

Mhe. Spika, wengi wamezungumza utaratibu mzuri wa matumizi ya pembejeo na upatikanaji wake wa kwa wakati. Hilo tutalisimamia ipasavyo na tutaendelea kushauriana nanyi na wakulima na tutaendelea kuwapitia.

Karakana za matrekta niliulizwa hatima yake. Hivi sasa karakana zote mbili zipo chini ya Idara ya Kilimo na zitaendelea kubaki hapo. Lakini tutaendelea kuzisimamia ipasavyo ili ziweze kutoa huduma ambazo tunazitarajia kutoka karakana hizo. Wajumbe wako Mhe. Spika, walitaka kujua kila Wilaya kuna heka ngapi ambazo zinatumika kwa kilimo hivi sasa.

Wilaya	**Ukubwa wa hekta**
Kaskazini 'A' Unguja	15,446
Kaskazini 'B'	10,067
Wilaya ya Kati	16,417
Kusini	2,832
Magharibu	9,275
Wete	14,698
Micheweni	14,688
Chakechake	12,482
Mkoani	14,492
Laki moja elfu kumi mia tatu na tisini na tano	(110,395)

Hekta hizo zote zinatumika kwa kilimo kwa mgawanyo huo wa Wilaya niliouzungumza.

Mhe. Spika, athari ya maji chumvi kwenye maeneo ya kilimo. Mhe. Spika, katika mapango wetu mkuu wa mpunga eneo hili limezungumzwa kwa kina sana. Hatuwezi kwenye bajeti tukaelezea kila kitu, mpango ule wa miaka mitano wa zao la mpunga ni mkubwa na umezingatia yote haya. Huwezi kuzingatia athari ya maji chumvi kwenye mabonda ya mpunga na maeneo mengine ya kilimo na ukawa na ufanisi. hili limezingatiwa na litasimamiwa kwa pande mbili. Lakini hapa Waheshimiwa wajumbe ni lazima tuambizane ukweli. Maji chumvi yanaingia kwenye mabonde kwa sababu wananchi wetu wamekata mikoko, sasa hilo sio la serikali. Kwa njia moja jamii ni lazima ijiratibu wenyewe, tumekuwa na tabia za ajabu hivi sasa. Mfano.

Miaka ya nyuma kwa upande wa Kusini kwa kina Maalim Haroun na Mhe. Spika, kulikuwa kuna kipindi pweza wanafungwa. Wazee walikuwa wanatoa sababu nyingi za itikadi, lakini miongoni mwa hekma zile ni kwamba kutoa nafasi kujirudi. Sasa leo tunakwenda katika eneo kuna hekta 100 ya mikoko tunaikata kwa siku moja, tunategemea nini? Maji yatapita ya chumvi. Kwa hivyo niwaombe sana na nyinyi wawakilishi mulisimamie hilo na serikali itawasaidia wananchi wetu. Hatukatazi uvunaji wa maliasili, lakini tuvune kwa utaratibu ulioendelevu. Leo vuna hekta kumi, unapanda kumi, mwaja ujao unavuna kwengine tano, unapanda 15 namna hiyo. Nchi yetu tukiila katika mwaka moja tu tukavuna kila kitu mwaka wa pili tutakufa njaa. Kwa hivyo naomba hapa tusaidiane na wananchi wetu kuwaelimisha juu ya umuhimu wa utunzaji wa mali ya asili zetu na mazingira yetu.

Miradi yetu ya misitu asili, mradi wa hima, mradi wetu wa misitu ya ukanda wa pwani ambayo tumeieleza kwa kina sana ndani ya kitabu chetu. Ipo makusudi kuwaelimisha wananchi wetu, kuwasaidia katika utunzaji wa maeneo haya matatu ya maliasili ya nchi yetu. Wajumbe wengi wamezungumzia haja kubwa ya kupitia upya Sera ya Ardhi, kazi hiyo inafanywa na wiza husika na tutashirikiana nao pale ambapo yametuhusu.

Pia wajumbe wako wamezungumza kwamba bado wakulima hawajasaidiwa kwani hawashibi, mapembe hawayamudu.

Mhe. Spika, hapo nitofautiane kidogo na wajumbe waliozungumza hivyo. Mipango tuliyokuja nayo ni kuwapunguzia mzigo kwa kiasi kikubwa sana wakulima wetu ili fedha wanazozitumia kuwekeza katika kilimo zipungue, wapate kilimo chenye tija kwa misaada mbali mbali ambayo watapata kwa serikali. Wapunguze kutumia muda mwingi kwenye mabonde yao kutokana na zana za kisasa ambazo zitaagizwa ili na wao wapate kilimo chenye tija na nafuu. Tunawezesha ili sasa mpunga wazalishe wenyewe kwa wingi, tusinunue mapembe kutoka nje. Tukiendelea na jitihada zetu mapembe sasa mwaka hadi mwaka tutapungua kununua kutoka nje. Tutapata mpunga mzuri, NERICA, Super India, mipunga ambayo kwa kweli ina harufu, ina uzazi. Kwa hivyo yale yote tunayoyapenda Wazanzibari katika tafiti tulizofanya mbegu mpya hizi zinakidhi mahitaji yetu.

Wengi wamezungumzia huduma za ugani. Hilo tumelieleza kwa kina sana ndani ya kitabu chetu juu ya vijana wapya ambao tutawaajiri na namna tutakavyowatumia.

Lakini Mhe. Mtando alisema moja la msingi hapa, kwamba hao tunaowapeleka Kizimgani watoke majimboni na hatimaye wafanye kazi majimboni au maeneo ambayo wanatoka. Hili la msingi sana, tumeliona tatizo kubwa sana kwa hawa vijana tunaowaajiri. Ikiwa anatoka mjini hataki kwenda kufanya kazi shamba. Akishakupata kazi tu, anatafuta masomo sasa, kwamazingira ya kwetu ataanza kuombewa na kila mtu, maana kila mmoja anamlilia mwanawe, ukikataa wewe ni mkorofi. Mhe. Spika, tatizo hilo lipo, tumelizingatia na huko tunakokwenda tutajaribu kutizama kwa kuwatoa vijana kwenye maeneo wanayotoka na hatimae tutakapowaajiri wafanyakazi katika maeneo wanayotoka.

Mhe. Spika, kuhusu mbolea ya asili kwa maana ya samadi, mboji na nyenginezo wengi wametaka kujua kwa nini hatujayazungumza kwa kina. Mhe. Spika, katika mipango yetu matumizi ya mbolea hizi ni lazima na katika mipango yetu yote miradi yetu yote tunayozungumza hayo ya mashamba darasa na kwengineko, ni kwamba matumizi ya mbolea ya samadi, mboji kwa kweli yamepewa kipaumbele hata uzalishaji wake. Kwa hivyo, hilo tumelizingatia nalo.

Mhe. Spika, waheshimiwa wamezungumza umuhimu wa kurejesha mitaala Fidel Castro na kwengineko na pia kuanzisha *annex* ya Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa kule Pemba. Mhe. Spika, tunayapokea hayo na tutayazingatia, lakini kama tulivyoeleza kwenye kitabu chetu, mwenendo wetu wa mwaka huu na miaka mitano ujao tumeeleza kwa kina kwenye kitabu hicho na huo ndio mwelekeo wa serikali, lakini waliotueleza tutayapokea na kuyazingatia.

Mhe. Spika, vile vile waheshimiwa wamezungumzia mihogo kuvamiwa na maradhi, mahindi na migomba. Mhe. Spika, haya yote tumeshayazungumza kwenye kitabu kwamba tumeathirika sana na mpaka zile mbegu asili za mihogo nimezitaja kwenye changu. Mhe. Spika, pia namna tulivyoathirika nimeelezea, kazi kubwa iliyofanywa na watafiti wetu katika kutafuta na kuvumbua mbegu mpya na nimezitaja Kizimbani, Machui, Mahonda na Kama ambazo tayari tumeshaanza kuzisambaza na maeneo tuliyosamba tumeeleza. Mhe. Spika, pia wakulima wa maeneo yetu watusaidie kuzalisha mbegu hizo pia tumeeleza. Hayo yote ni kwa ajili ya kupambana na maradhi mbali mbali yanayoathiri mihogo yetu pamoja na yale maradhi mengine ambayo nimeyataja.

Mhe. Spika, mahindi tayari tumeshapata mbegu mpya, hilo pia naomba kuchukua fursa hii kuwatangazia kwa hivi *basic nation* yake ni *TAN 250* tunategemea kuvuna tani 15 kwa msimu huu ambao tayari karibuni zitaanzwa kuvunwa, mbegu hiyo ya mahindi nayo ina uzazi, ina ladha na inahimili maradhi. Mhe. Spika, tafiti hizo zimefanywa hapa hapa kwetu, labda wajumbe mkinikubalia kwa heshima na namna tunavyompenda Spika wetu mbegu hiyo tuiite "Kificho".

Mhe. Spika, makofi haya yanadhihirisha kwamba wajumbe wamelipokea hilo. Kwa hivyo, mbegu hiyo mpya ya mahindi kwa heshima ya Spika wetu tukianza kuzalisha na kuisambaza kwa wakulima itaitwa "Kificho". Naamini itakuwa na maslahi na tija kama alivyokuwa na maslahi na sisi Spika wetu.

Mhe. Spika, kuhusu Kiwanda cha Sukari labda niseme katika migomba bado hatujafanikiwa hadi hivi sasa, lakini tafiti zinaendelea. Kiwanda cha Sukari Mahonda hiki kimezungumzwa na wajumbe wengi hasa wanaotoka Kaskazini Unguja, atakuja kueleza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. Ni kweli Baraza la Mapinduzi limeunda kamati maalum na likizingata sasa kwamba je ipo haja, upo uwezekano, upo ukweli wa kutumia ardhi ile ya sisi kuweza kuzalisha sukari ambayo itatusaidia au dhana ile haina haja tena? Mhe. Spika, kuna umuhimu huo au tutumie ardhi ile kwa kuwapa wananchi wetu walime mpunga na mazao mengine ambayo yana umuhimu zaidi kwetu kwa hivi sasa. Mhe. Spika, nina amini maamuzi yatazingatia maslahi ya nchi yetu na watu wake.

Kwa hivyo, Mhe. Mazrui atakuja kukuelezeni je, mwekezaji yule amevunja mikataba, anafanya jambo la maana au hafanyi, uwezo anao au hana kwa muda

aliopewa, mikataba kaivunja au hajaivunja yote hayo atakuja kueleza Mhe. Mazrui. Kwa hivyo, nakuombeni waheshimiwa mumsubiri yeye. Mhe. Spika, mimi nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba Wizara ya Kilimo katika mazungumzo hayo serikali itaendelea kuzingatia na kulinda maslahi ya wakulima.

Mhe. Spika, kuhusu mashamba ya mpira wamesema hapa kakodishwa nani? Ni kwamba mashamba ya mpira yamekodishwa kampuni inaitwa *Agro Tax* kwa US$-1000 kwa mwaka sawa na milioni 160,000,000/. Mhe. Spika, ni kwamba kampuni tuliokodisha mashamba hayo hivi sasa tunaendelea na mazungumzo kutokana na mipira wenyewe sasa imeshafika uzeeni, kwa maana uzazi wenyewe umepungua. Mhe. Spika, ni kwamba wao wana mazao mawili. Moja ni kuikata ile na kutumia kama mbao, lakini *process* ya kukata mbao ya mti wa mpira ni ndefu, kiwanda cha kufanya *treatment* ya mbao ile kinagharimu zaidi ya US$-1,000,000,000 kwa sababu uwe na kiwanda maalum huwezi kukata mpira halafu ukaacha na mbao ukateegemea utaweza kutumia, mpira sote tunaujua hilo haliwezekani.

Kwa hivyo, unakatwa ule unafanyiwa *treatment* maalum mpaka misumeno yake ni maalum, halafu pia tuanze kupanda mipira mipya. Mhe. Spika, kwa sababu bei ya mpira hivi sasa imeongezeka sana duniani, hivyo tunaisubiri ripoti yao hiyo halafu tutapeleka ushauri wetu serikalini na serikali itaamua sasa tufanye nini na ardhi ile ambayo imepandwa mipira Unguja na Pemba. Mhe. Spika, tutaendelea kuwahimiza ili maamuzi hayo tuweze kuyafanya haraka.

Mhe. Spika, kuhusu ghala la *Living Stone* hili aliliuliza Mhe. Mtando. Ni kwamba maghala yale wamepewa *ZRB* ndio wanaojenga pale. Kwa hivyo, kama utataka ufafanuzi zaidi utamsubiri Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, wengi waliuliza kama kuna ripoti za utafiti zinatolewa. Mhe. Spika, ni kwamba ripoti zinatolewa kila mwaka juu ya tafiti mbali mbali zinazofanywa ndani ya nchi yetu. Lakini niseme kwamba sio nchi yetu, wataalamu wetu hivi sasa wamekuwa mali hata wa nchi jirani kwa hatua kubwa tulopiga sisi kwa uvumbuzi wa mbegu mpya na zinazostahamili mazingira na kuweza kuhimili pia maradhi katika nchi yetu na ukanda huu. Kwa hivyo, pia wanaalikwa maeneo mbali mbali kutoa *paper* hizo juu ya namna tulivyoweza kufikia hatua ambayo tumefikia sisi.

Mhe. Spika, nafikiri kwa asilimia kubwa nimeweza kukidhi mahitaji ya hoja mbali mbali waliouliza Waheshimiwa Wajumbe labda moja kituo cha Chambani. Mhe. Spika, tuna vituo vya aina mbili vya tafiti na vya uzalishaji. Kituo cha Chambani kilikuwa kinatumika zaidi katika uzalishaji wa matunda,

uzalishaji huo hatufanyi tena kwa maana wizara au serikali haisimamii uzalishaji wa matunda. Pale zaidi hivi sasa tunasimamia uzalishaji wa mbegu, kwa maana tunayo ile miti vile vilele katika kufanyia *graphting* ndio tunazipatia pale. Kwa hivyo, ni kweli kituo kile majengo yalianguka na baadae yakaondoshwa na hata wafanyakazi wameondoshwa pale.

Lakini kama utakumbuka wakati najibu suala nafikiri kikao kilichopita tulilizungumza hilo na pia nikakueleza kwamba serikali au wizara itazingatia upya kama ipo haja ya kurejesha kituo pale. Mhe. Spika, nataka nimuhakikishie kwamba dhamira yetu sisi kuwa ni karibu zaidi na wakulima. Kwa hivyo, hilo tutalizingatia na inshaallah Mwenyezi Mungu atatupa uwezo tutafikia pahala pazuri.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri hoja imetolewa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Kilimo na Maliasili wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 20 – WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba 39,000,000
Kifungu 0401 Idara ya Mipango na Sera

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nilikuwa nataka maelezo juu ya suala langu lile nilouliza wakati nilipokuwa nachangia hotuba hii juu ya eneo lile la Living Stone, Mhe. Waziri amesema sijui wamepewa *ZRB* mimi nilikuwa nataka ufafanuzi zaidi. Ni kwamba wamepewa *ZRB* kwa ajili ya kitu gani na kwa utaratibu upi?

Mhe. Mwenyekiti: Tunakusudia kukusanya mapato hapa una hofu na haya.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	2,000,000
Kifungu 0501	Kamisheni ya Kilimo, Utafiti na Elimu/Wakulima	24,000,000
Kifungu 0701	Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka	175,000,000
	Jumla ya Fungu	**240,000,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko y oyote)

FUNGU 20 – WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	1,388,302,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ndio ile ile ambayo niliizungumza pale ukaniambia nisubiri kwenye matumizi, kwamba eneo lile Mhe. Waziri katika majibu yake amesema wamepewa *ZRB* nilikuwa nataka kujua wamepewa kwa ajili gani na kwa utaratibu upi kwa sababu kwa taarifa tulizonazo au nilizozipata mimi ni vyengine kinyume na hivi, kwa hiyo nilikuwa naomba maelezo zaidi juu ya hilo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya wizara yangu kama nilivyosema wamepewa *ZRB* wameomba na wamepewa kwa maana ni taasisi ya serikali. Kuhusu wanafanya nini Mhe. Mwenyekiti, mimi sijui na ndio maana nikasema kwa maelezo zaidi atakapokuja kusoma Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pengine ataeleza zaidi na yeye nimeshampa taarifa hiyo naamini kwamba atatoa majibu ambayo pengine yanafaa. Kwa sababu ambayo iko nje ya mamlaka yangu mimi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri sijui kuna barua yoyote ambayo inaonesha hilo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, ndio lazima katika utaratibu wa kubadilishana mali za serikali maandiko lazima yawepo, hayawezi kuwa kwa mdomo tu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba hiyo barua.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri

nataka kidogo nitoe ufafanuzi juu ya suala la Mhe. Mtando. Mhe. Mwenyekiti, awali ndugu zetu wa *ZRB* walikuwa wanatafuta eneo la kujenga Ofisi ya Makao Makuu na walifikiria kwamba pale pangeweza kuwafaa, lakini baadae wakaona kwamba lile eneo ni dogo wakapewa eneo la Kilimani Bar nalo vile vile wakaona lina matatizo ya ule mtaro kwa hiyo napo wakaona hapafai, ndio wakapewa eneo la Mazizini kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu.

Lakini kimsingi taasisi moja inapokabidhiwa eneo au inapokabidhiwa majengo inapotaka kuhamisha jengo hilo kwenda katika taasisi nyengine kwanza huwa tunafanya tathmini kujua kwamba lile eneo thamani yake ni kiasi gani, halafu inafanyika *transfer official***.** Mhe. Mwenyekiti, nataka kuthubu kusema tu hivi sasa hivi tuna zoezi kama hilo baina ya mimi na Mhe. Mazrui katika baadhi ya maeneo yake nataka niyachukue mimi na baadhi ya maeneo yangu ayachukue yeye, tunafanya zoezi hilo. Mhe. Mwenyekiti, huo ndio utaratibu wa kiserikali na taarifa hizo zipo na Mhe. Mtando akizitaka baadae tunaweza tukampatia akaziona.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo sijakubaliana na maelezo yake mimi nilichoomba kwa mara ya mwisho kwamba nilikuwa nataka ile barua ambayo imeonesha kwamba wanaomba pale kwa ajili ya shughuli hizo. Lakini maelezo ya Mhe. Waziri naona yameenda kwengine kabisa, nilikuwa naomba hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimueleze Mhe. Mtando kwamba ukiniuliza baadhi ya vitu hapa sitakuwa navyo kwa sababu ungelisema tokea juzi au jana kwamba unataka barua hiyo tungeweza kuitafuta tukaja nayo hapa. Lakini hilo la barua ameiomba hapa kwa hapa sasa nikisema mimi nitamtolea mfukoni nitamdanganya bure, ni kwamba akubali maelezo yangu kwamba tutampatia hiyo barua aione kesho Jumatatu ofisi zetu zinafunguliwa tutaitafuta hiyo barua tutampa. Lakini huo ndio utaratibu wa kiserikali huwezi ukaondoa mali iliyopo katika Wizara ya Kilimo ukaipeleka Wizara ya Fedha kwa kienyeji lazima kuwe kuna barua na barua zipo tutamtafutia na tutampa, hayo ndio maelezo yangu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na maelezo aliyoyatoa Mhe. Waziri mimi hoja yangu nimeianza jana na hata juzi nilipokuwa najadili Wizara ya Mifugo na Uvuvi hapa tulitaka mikataba hapa na Waziri wa Mifugo alikuwa nayo kwa sababu alijiandaa kwamba nitaulizwa katika hoja hii na huu hapa ushahidi wangu katika hilo. Na katika hili mimi jana ndio nilipochangia nafikiri mpaka leo ilikuwa ni vizuri Mhe. Waziri alikuwa ajitayarishe kuja na vitu vyote ambavyo vinaonesha kile ambacho mimi nilikuwa nahoji, na nilisema kwamba nataka maelezo kamili katika hili.

Kwa hivyo, atakapokuwa Mhe. Waziri anasema leo ndio kaambiwa sio kweli mimi nilizungumza jana suala hilo, kwa hiyo nafikiria ilikuwa ni vyema akatuletea hilo kwa sababu ninachouliza hapa wananchi ndio wanataka kujua.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mtando *hansard* zipo jana hukuhitaji hii barua ya *transfer* hukuhitaji, usipokuwa ulitaka maelezo juu ya jengo hili na tayari umeshapewa. Kwa hivyo, leo umeona yale maelezo hayakutosha unataka barua ya *transfer* hiyo hanayo kweli, lakini tukubali ahadi kwamba barua hiyo ataileta na atakuonesha. Nafikiri tukiendelea na hoja za aina hii kwa kweli inaweza ikatucheleweshea shughuli zetu, nadhani tuendelee.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi langu ni suala tu kwa kuwa niuliza kuhusu Karakana mbili hizi iliyoko Mbweni na ile iliyoko Machomane. Mhe. Mwenyekiti, sisi tulipopita katika ziara zetu miaka mitano iliyopita ilikuwa kuna suala la kisera la kuwa ile Karakana ziwe idara au zibakie shirika, na kwa kuwa zinakuja chinia katika shughuli zake. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilimuomba Mhe. Waziri atueleze ni msimamo upi uliochukuliwa na wizara kwa zile Karakana, lakini naona kama sikusikia likitajwa hili suala la Karakarana hivyo naomba Mhe. Waziri atupe maelezo kidogo kuhusu hilo.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, suala la Karakana wakati na jumuisha nililieleza lakini nimuongezee kidogo Mhe. Rashid ni kwamba hivyo anavyoeleza ni sahihi mwelekeo wa sera bado upo kwamba aidha iwe idara au iwe shirika. Lakini nimeeleza kuwa hivi sasa Karakana zote mbili ziko chini ya Idara ya Kilimo kama ni Kitengo cha *Mechanization* ili ziendelee kutoa huduma kwa ufanisi zaidi kwa wakulima wetu. Kwa hivyo, hayo masuala ya sera bado yana nafasi ya kutosha tu ya kuendelea kufikiriwa na hatimae utekelezaji wake wakati utakapofika tutayazingatia hayo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina wasi wasi ni ile hali ya umuhimu wa zile Karakana na maendeleo yetu ya kilimo ndio iliyonipelekea kusema hivyo. Kwa hivyo, naomba tuendelee.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niitumie fursa hii nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake makini na hivyo ndivyo anavyotakiwa waziri awe makini. Kwa hivyo, wakati nachangia mimi nilimuuliza suala dogo ambalo nilitaka ufafanuzi kwamba katika suala la kuendeleza kilimo na kuwashajihisha wananchi ili wajielekeze katika masuala ya kilimo Mhe. Rais wa awamu ya sita alitoa agizo kwamba ili kuonesha mfano viongozi hasa wawakilishi wapewe mashamba ili walime. Kwa hivyo, utekelezaji wa agizo lile hadi sasa hivi haujatekelezwa kwa hiyo nadhani ilikuwa Mhe. Waziri aeleze namna gani kwa nini agizo lile la serikali halijatekelezwa.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, agizo la Mhe. Rais litaendelea kubaki pale pale bahati mbaya nimepitikiwa kidogo tu, kwa hivyo nalipokea nitakaa na watendaji wa wizara yangu ili tuingie katika utaratibu wa kutekeleza agizo lile.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa kauli hiyo nampongeza Mhe. Waziri sasa naomba tuendelee.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango na Sera	950,200,000
Kifungu 0402	Chuo cha Kilimo Kizimbani	

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nikasema kwamba kwa kuwa tuna visiwa viwili na nimeipongeza juhudi ya serikali kuanzisha Chuo cha Kilimo kule Kizimbani ambacho kitatoa wataalamu wetu wenyewe na sasa hivi kinaelekea kutoa hata wataalamu wakubwa kwa kuunganishwa na Chuo cha *SUZA*. Lakini nikatoa ombi kwamba kwa sababu Pemba hakuna tawi lake yaani *annex* na ni ardhi ambayo inatoa mazao mengi. Haoni kuna haja Mhe. Waziri ya kuanzisha kituo hiki au tawi la chuo hiki kule kwa sababu kitasaidia hata hao wanaojifunza hapa kwenda kule kuweza kujifunza na udongo wa kule na ardhi za kule zinavyootesha na mambo mengine. Mhe. Waziri amejaribu kujibu lakini sikuridhika na majibu, hakuonekani kwamba kumeekewa mkakati wa kuanzisha kule. Hebu Mhe. Waziri namuomba atupe tena maelezo ya ziada.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane nae Mhe. Rashid kwamba Pemba ina umuhimu wa pekee kwa kilimo chetu na niwashukuru sana ndugu zangu walioko Pemba kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kilimo na pia ni kweli nikubaliane nae kwamba nilikuwa sina mkakati wa kuanzisha *extension annex* ya Chuo cha Kilimo Kizimbani Pemba na ndio maana nikasema kwamba mkakati wangu wa kuimarisha Chuo cha Kilimo Kizimbani nimeeleza. Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia kitivo cha Chuo Kikuu chetu cha *SUZA* nimeeleza humu pamoja na kuimarisha miundombinu, mabweni, rasilimali watu na kadhalika yameelezwa kwa kina sana.

Lakini ni kweli sina mkakati wa kuanzisha *annex* ya chuo hicho Pemba na ndio maana nikawaambia Waheshimiwa Wajumbe yeye na wenzake walioiuliza hilo, kwamba waliyonieleza tutayazingatia kwa upeo wake kutokana na umuhimu wa Kisiwa cha Pemba kwa kilimo chetu. Kwa hivyo, naomba anikubalie na aridhike na maelezo yangu, kwamba hayo tutayazingatia kwa upeo wake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwepo katika Baraza hili kipindi kilichopita, ujamadari wake na imani yake naijua. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0402	Chuo cha Kilimo Kizimbani	500,000,000/-
Kifungu 0701	Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka	946,164,000/-
Kifungu 1101	Idara ya Umwagiliaji Maji	451,268,000/-
Kifungu 1301	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	170,700,000/-
Kifungu 1401		

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia kuhusu huduma za matrekta nilimueleza Mhe. Waziri pongezi zangu kwanza kwa ununuzi mpya wa matrekta na namna yanavyofanya kazi. Lakini nikamueleza kwamba tatizo walilonalo wananchi wengi ni ule utaratibu wa huduma ya lile trekta, hakuna utaratibu maalum unaopangwa na wananchi hubidi kutuagiza sisi twende tukafuatilie na tukienda kule hatuoni kwamba kuna utaratibu uliopangwa hasa wa kuhudumia kama shehia fulani au maeneo fulani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atupe maelezo ya ziada ya namna gani wizara ilivyojipanga sasa kuanzisha utaratibu huu ambapo wananchi watajua kwamba tarehe fulani au kipindi fulani matrekta yatakwenda katika maeneo yao.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu tunao na hili nilizungumza wakati najumuisha. Utaratibu wa matumizi ya trekta kwa wilaya na shehia tunao. Nikubaliane na Mhe. Mjumbe kwamba kutokana na uhaba na ubovu wa matrekta mara nyengine utaratibu huo hautekelezeki tunavyotaka utekelezeke. Kwa hivyo, kimsingi nikubaliane nae kwamba ipo haja ya kuwa na utaratibu maalum na mzuri zaidi pamoja na hayo matrekta mapya ambayo tunategemea yatakuwepo basi kwa msimu ujao nafikiri utaratibu wetu utaimarika zaidi. Nawaomba bado Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waendelee kutusaidia, wakati wa msimu wawe karibu sana na sisi pale ambapo wanahisi hawajaridhika na utaratibu basi tutakuwa tayari kuwasaidia.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru majibu ya Mhe. Waziri, namuomba jambo moja tu. Wale maafisa wao tukiwa kuna haja ya kwenda sisi yaani tutakapokwenda wawe wawazi kidogo katika kutueleza pale walipokwama basi. Ikiwa kuna mkwamo watueleze kwa sababu inawezekana matrekta yanalima pahali pengine wananchi wanayaona halafu ukienda ukiwaambia trekta ni bovu wanakwambia mbona mahali fulani yanalima. Sasa kuwe na kitu kama hicho ambacho maafisa watakuwa tayari kujibu yale

masuala yetu tukienda ili kuwe na uwazi zaidi. Nakushukuru tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 1401	Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe	140,400,000/-
Kifungu 0501	Idara ya Kilimo	2,430,921,000/-

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, jana wakati nachangia nilizungumzia jinsi ya hizi shamba za mipira hususan zile ninazozifahamu sana zilioko Pemba, inaonekana kwamba watu wana wasiwasi sana kwamba shamba hizi zinaendeshwa na serikali au zina mpangaji. Lakini mimi hapa ninachotaka kujua ni kwamba makisio yake katika kipindi cha mwaka 2009/2010 kilichopatikana ni shilingi 206.2 milioni, lakini makiso ya mwaka 2010/2011 yameteremka mpaka kufikia shilingi 130 milioni. Sasa nataka niulize kuna tatizo gani la kitaalamu lililosababisha kuteremka kwa makisio, yaani kile kilichopatikana mwaka 2010 kikawa ni kikubwa lakini makisio yetu ya 2011 yakawa ni madogo.

Pili, je, katika ukodishwaji wa haya mashamba ya mipira kunatangazwa *tender* au mtu anayejulikana tu ndio anapewa?

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, kikawaida kitu kishakuanza kuwa na thamani kitaulizwa na wengi, bei ya mpira ilipokuwa chini hakuna mtu aliyekuwa anaitaka mishamba yetu ya mipira na hakuna mtu aliyekuwa anauliza. Kupanda na kushuka kwa makisio inatokana na *exchange rate* kwa sababu hawa wanatulipa kwa pesa za kigeni. Utangazaji wa *tender* wakati huo yalipokodishwa sikumbukii vizuri Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu yamekodishwa miaka mingi nyuma. Kikawaida ndio utaratibu mzuri ambao unafaa katika ukodishwaji, lakini pia serikali ina utaratibu mwengine pia wa utoaji wa mali zake. Lakini kama nilivyokwishamueleza Mjumbe kwamba hapa tulipofika mipira yenyewe haizai tena, kwa maana uzazi wake umepungua kutokana na sasa kufikia *optimum age* ya uzalishaji. Tunafikiria upya sasa namna tutavyoweza kuishauri serikali juu ya hatma za mashamba haya.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kukubali kuendelea naona nitumie fursa hii kumpongeza waziri kwa jibu lake zuri. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0501	Idara ya Kilimo	2,430,921,000/-
Kifungu 1701	Taasisi ya Utafiti wa Kilimo	145,045,000/-
Jumla ya Fungu:		**7,123,000,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapojuu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mMabadiliko yoyote)

FUNGU 20 – WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI

Kifungu 0401	- Idara ya Mipango na Sera	8,139,849,000/-

Jumla ya Fungu: **8,139,849,000/-**

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirejea)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako liyakubali makadirio haya.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na makadirio hayo wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nakushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa ya shughuli zetu. Nilipokea dharura za wajumbe wengi lakini naomba tujigawe ili shughuli inayofuatia iweze kuendelea. Shughuli inayofuata hapa ni uwasilishaji wa Hotuba ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa hivyo, mnadhimu wa wajumbe wa upande wa Wawakilishi wa CCM atafanya utaratibu juu ya kujigawa na shughuli nyengine ambayo inatukabili, nadhani atazingatia kwamba kikao hiki kiwe kinaendelea. Basi sasa nimuombe Mhe. Mwenyekiti wa Baraza, Mhe. Mgeni Hassan Juma aje kukalia kiti.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Mwenyekiti, Naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae Kama Kamati ya matumizi ili niweze kutoa maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kukutana hapa leo katika Baraza hili tukufu, kwa lengo la kujadili masuala muhimu ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumpongeza Mhe. Dkt Ali Mohammed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Pia nampongeza Mhe. Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kuwa Makamo wa Pili wa Rais. Nawaombea kila la kheri na ufanisi mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, nakupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza letu tukufu. Tunakutakia kila la kheri katika kuliongoza Baraza lako. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kwao. Wote nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu ya kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar katika kuwaletea maendeleo yao.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii adhimu, kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniteua mimi kuiongoza wizara hii na kwa uamuzi wake wa busara wa kuchanganya Sekta za Vijana, Wanawake, Watoto na Ustawi wa Jamii jambo ambalo litatuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ushirikiano, kutoa miongozo, maelekezo na ushauri wao kwa masuala ya wizara ambayo yametuwezesha kufanikisha shughuli zetu kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa naomba kuliarifu Baraza lako tukufu kuwa tarehe 15/04/2011 wizara ilipata msiba mkubwa wa kifo cha aliyekuwa Katibu Mkuu na Mtendaji Mahiri mwenye uwezo mkubwa na hodari Ndugu Rahma Mohammed Mshangama. Ndugu Rahma alikuwa ni mahiri katika kutafuta michango mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha malengo na mipango ya wizara yanatekelezwa kwa ufanisi. Alifanikiwa kuanzisha miradi mikubwa ya kimaendeleo katika sekta mbali mbali alizozihudumia wakati wa uongozi wake. Wizara inamshukuru kwa mchango wake mkubwa alioutoa katika kuleta maendeleo ya Wanawake, Vijana, Watoto na jamii kwa ujumla, tunamuomba Mwenyezi Mungu Ailaze Roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi**,** Amin.

Mhe. Mwenyekiti, **w**izara imepata faraja kubwa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumteua Ndugu Fatma Gharib Bilal kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Ndugu Fatma ni miongoni mwa wanawake mahiri, mwenye sifa na uwezo mkubwa aliyeandaliwa vizuri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kabla ya uteuzi wake akifanyakazi katika Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu Duniani, tunampongeza sana na kumtakia utendaji mwema wa kazi zake, tunaahidi tutampa mashirikiano mema.

Mhe. Mwenyekiti, Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2011/2012 imezingatia na kulenga Mipango na Mikakati Mikuu ya Serikali ifuatayo: Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA I na II), Malengo ya Milenia, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), 2010 – 2015, Mwelekeo wa Sera za CCM 2010 – 2020, Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein aliyoitoa katika uzinduzi wa Baraza la Nne la Wawakilishi na Hotuba aliyoitoa katika maadhimisho ya Sherehe za Miaka 47 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, Maagizo ya Mhe Rais alipokutana na uongozi wa wizara, Mpango Mkakati wa Wizara 2011 – 2015 na Sera za Kisekta.

MALENGO MAKUU YA WIZARA

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kipindi cha miaka minne (2011/2015) kwa mujibu wa Mpango Mkakati imejipangia kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

1. Kuhakikisha kuwa mapungufu katika Sheria na Sera zinazohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee yanafanyiwa kazi.
2. Kukuza uwezo wa wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.
3. Kuimarisha uratibu wa mwitiko wa wadau na watoa huduma wa masuala yanayohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.
4. Kuimarisha hali za kiuchumi, utamaduni na maendeleo kwa, Wanawake Vijana, Watoto,na Wazee.
5. Kuangalia hali halisi ya Haki na Maendeleo ya Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee zinafuatiliwa na kutolewa taarifa kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeundwa na idara tano na Ofisi Kuu Pemba kama ifuatavyo: Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; Idara ya Uendeshaji na Utumishi; Idara ya Ustawi wa Jamii; Idara ya Maendeleo ya Vijana; Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto na Ofisi Kuu Pemba.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2010/2011

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kiungo kikuu cha wizara. Idara hii ina jukumu la kupanga, kusimamia shughuli za utafiti, sera na kuratibu shughuli za wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, idara ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi watendaji 35 wa wizara, ili kuwaongezea uwezo na ujuzi wa kazi zao.
2. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya wizara.
3. Kukiimarisha Kitengo cha Habari na kuendelea kukusanya habari na kutoa taarifa za maendeleo ya wizara.
4. Kutekeleza programu ya kupambana na UKIMWI katika maeneo ya kazi.
5. Kuendelea kukiimarisha Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini cha wizara.
6. Kuandaa miradi na programu mbali mbali kwa ajili ya kutekeleza Sera na Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2010/2011, wizara imefanikiwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ndani na nje ya nchi watendaji 23, kati ya hao 17 Wanawake na 6 Wanaume (**Angalia kiambatisho Nam. 1**).

Mhe. Mwenyekiti, **k**atika kipindi cha mwaka 2010/2011, wizara kupitia kitengo chake cha habari imetayarisha vipindi hamsini (50), taarifa 210 na makala 34 ambavyo vimerushwa kupitia vyombo mbali mbali vya habari.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeandaa Mpango Mkakati wa Wizara kwa kipindi cha miaka minne (4) 2011-2015. Aidha, wizara iliandaa ripoti mbalimbali za utekelezaji zikiwemo utekelezaji wa Mwezi, Miezi mitatu, Miezi tisa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

MIRADI INAYOSIMAMIWA NA IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, idara katika kipindi cha mwaka 2010/2011 imesimamia utekelezaji wa miradi miwili (2) ifuatayo:-

Mradi wa Jinsia Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu Duniani (*UNFPA*) na una lengo la kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kuzingatia masuala ya Jinsia katika Sera, Sheria, Mipango na Bajeti za Maendeleo.
Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 mradi huu umetekeleza yafuatayo:-

Wizara imeanzisha Kamati ya Kitaifa ya Kudhibiti Vitendo vya Udhalilishaji wa Kijinsia ambayo imezinduliwa mwezi wa Oktoba, 2010 na inajumuisha Wajumbe kutoka Wizara yetu, Polisi, Afya, Mahkama, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Katiba na Utawala Bora na Washirika wa Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara iliandaa mafunzo ya Uchambuzi wa Takwimu kwa kuzingatia masuala ya kijinsia. Aidha, tarehe 8 Disemba, 2010 wizara ilifanya maadhimisho ya Kitaifa ya siku 16 za wanaharakati wa kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia huko Wilaya ya Micheweni - Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imefanya mkutano wa robo mwaka na Maafisa wa Jinsia ili kuangalia utekelezaji wa uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika sekta zote za serikali Unguja na Pemba.

2. Programu ya Kuijengea Uwezo Wizara (*JP5*).

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inalenga kutoa mafunzo kwa wajasiriamali, kuweka mfumo imara wa Hifadhi ya Jamii, Mpango wa Kukuza Ajira kwa Vijana pamoja na masuala ya Ustawi wa Afya ya Mama na Mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeanza mchakato wa utayarishaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii Zanzibar ambayo itazingatia Hifadhi ya Jamii kwa makundi yote. Sera hii ina lengo la kuendeleza na kuiimarisha mifumo yote ya hifadhi ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imo katika hatua za mwisho za mchakato wa utayarishaji wa Sera ya Mafunzo Kazi ambayo ina lengo la kuwapa taaluma Vijana ili waweze kujiajiri na kuajiriwa. Sera hiyo ipo katika rasimu ya mwisho ili iweze kupelekwa katika vikao vinavyohusika kwa maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imetayarisha Mpango wa Utekelezaji wa Kisekta dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia ambao unalengo la kuweka mtandao wa sekta na kuunganisha jitihada za kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Aidha, wizara imekamilisha muongozo wa kufundishia watendaji wa afya jinsi ya kuyashughulikia masuala ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inaendelea na mchakato wa Utayarishaji wa Sera ya Jinsia na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Sera hiyo. Rasimu ya Sera hiyo imeshapitiwa na Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi.

PROGRAMU YA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hiki, Wizara imeweza kutekeleza programu ya UKIMWI kama ifuatavyo:-

- Imetayarisha Vijumbe (*Slogans*) na Vipindi vinavyohamasisha jamii kujikinga na UKIMWI ambavyo vimerushwa katika vyombo vya habari.
- Wizara kupitia Kamati yake ya UKIMWI imefanya mikutano ya ndani kuwaelimisha wafanyakazi wake juu ya kujikinga na janga la UKIMWI Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuhakikisha kuwa upungufu katika Sheria na Sera zinazohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee yanafanyiwa kazi.
2. Kukuza uelewa wa jamii katika masuala ya msingi yanayohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.
3. Kuimarisha ukusanyaji Kuimarisha ukusanyaji wa taarifa, uwekaji wa kumbukumbu na kutayarisha mfumo wa mawasiliano wa Wizara.
4. Kusimamia uandaaji wa tafiti zinazohusu Watoto, Wanawake, Vijana na Wazee.
5. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.
6. Kutekeleza Programu ya kupambana na UKIMWI katika maeneo ya kazi.
7. Kupanga na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango**,** Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne na Thelathini na Nne (434,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara na Shilingi Milioni Thelathini (30,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ni moja kati ya Idara mpya zilizoundwa katika kila Wizara kufuatia mabadiliko ya Muundo wa Serikali ya Awamu ya Saba. Idara hii ina jukumu la Kusimamia shughuli za Utawala, Mafunzo na Maslahi ya Wafanyakazi kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa malengo ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ililazimika kuhama katika Jengo la Mwanakwerekwe na kuhamia jengo lililopo Shangani pamoja na kufanya matengenezo makubwa ya jengo hilo yakiwemo kugawa sehemu *(partition)*, kupaka rangi, kununua samani na vifaa vyengine vya kufanyia kazi. Mbali na matengenezo hayo, bado Wizara ina ufinyu mkubwa wa nafasi kwa watendaji wake kutekeleza kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2011/2012, Idara imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kufanya tathmini ya uwezo wa Rasilimali Watu katika Wizara.
2. Kutayarisha Mpango wa Mafunzo wa Wizara na kuutekeleza.
3. Kukuza uwezo wa Uendeshaji wa Wizara.
4. Kufuatilia suala la Ujenzi wa Majengo ya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Utumishi na Uendeshaji iweze kutekeleza majukumu yake iliyojiwekea kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shillingi Milioni Mia moja na Thelathini na Sita. (136,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

IDARA YA USTAWI WA JAMII

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Ustawi wa Jamii ina wajibu wa Kuratibu na Kusimamia huduma za Kijamii kwa Wazee, Watoto na Watu walio katika Mazingira Magumu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara ya Ustawi wa Jamii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia utumiaji wa Mfumo wa taarifa za Watoto wanaoishi katika Mazingira Magumu zaidi *(MVC – Data Management System).*
2. Kutengeneza Sera ya Taifa ya Watoto wanoishi katika Mazingira Magumu.
3. Kuendelea kufanya utambuzi kwa Watoto wanoishi katika Mazingira Magumu kwenye Shehia 21 zilizobakia katika Wilaya ya Wete na Magharibi.

4. Kutoa mafunzo kwa Kamati za Watoto waishio katika Mazingira Magumu katika Shehia 120 za Unguja na Pemba.
5. Kukamilisha, Kusimamia na Kufanya tathmini ya Mradi wa Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara ya Ustawi wa Jamii imetekeleza yafuatayo:-

Wizara inaendelea kutunza watoto katika Nyumba ya Kulelea Watoto, Mazizini. Hadi sasa kituo kina jumla ya Watoto 49, (Wanawake 27 na Wanaume 22). Watoto wanaosoma Skuli za Chekechea ni kumi (10), Skuli za Msingi ni ishirini na sita (26), Sekondari ni wanane (8), Chuo Kikuu ni mmoja (1) na watoto wanne (4) hawajafikia umri wa kuanza masomo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeanzisha Seksheni ya Nyumba za Kulelea Watoto kwa lengo la kuratibu shughuli zote za Malezi ya Watoto katika Vituo vyote vya Serikali na vya binafsi Zanzibar. Wizara pia, ipo katika mchakato wa kukamilisha Muongozo wa Kuendeshea Nyumba za Kulelea Watoto. Aidha, Wizara imetayarisha, kuchapisha na kusambaza Muongozo na Mpango kazi wa miaka mitano wa Hifadhi na Ustawi wa Mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imekamilisha zoezi la majaribio la Utambuzi na Usajili wa Watoto walio katika Mazingira Magumu katika Wilaya za Wete na Magharibi. Jumla ya watoto elfu saba mia saba na kumi na moja (7,711) katika Shehia 39 za Wilaya ya Magharibi Unguja na watoto elfu nne mia saba na arubaini na mbili (4,742) katika Shehia 32 za Wilaya ya Wete Pemba walisajiliwa. Aidha, Wizara imeendesha zoezi la Ufuatiliaji na Tathmini ya shughuli hiyo. (Angalia Kiambatisho Nam. 2a na 2b).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kwa kupitia Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto imepokea jumla ya kesi 74 za udhalilishaji wa watoto kwa kipindi cha Julai hadi Mei 2011. (Angalia Kiambatisho Nam. 3). Aidha, Wizara imeanzisha Kamati ya Kitaifa ya Hifadhi ya Mtoto yenye Wajumbe kutoka taasisi zinazoshughulikia watoto. Wizara pia imeshughulikia malalamiko 121 kwa Unguja na malalamiko 142 kwa Pemba ya Utunzaji na Huduma kwa watoto. Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Watoto na Waratibu wa Wanawake na Watoto wa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Wizara imesimamia na kutetea Kesi za Watoto wanaotiwa hatiani kwa makosa mbali mbali Mahkamani.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inatunza Wazee katika Nyumba zilizoko Sebleni na Welezo kwa Unguja na Limbani na Gombani kwa Pemba. Jumla ya wazee mia moja na kumi na tisa (119) wanatunzwa katika nyumba hizo. Kati ya wazee hao, sitini na tano (65) ni wanaume na hamsini na nne (54) ni wanawake. Wazee wa Welezo wanapatiwa huduma muhimu kama vile chakula, matibabu,

nguo, malazi, uangalizi pamoja na posho la shillingi elfu saba (7,000/=) kila mwezi. Wazee wa vituo vyengine hupatiwa shilingi elfu ishirini na tano (25,000/=) kwa mwezi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango wa kuwaongezea wazee posho kufikia Shilingi Arubaini elfu (40,000/=) baada ya Bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kwa mashirikiano na Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo inalifanyia ukarabati mkubwa jengo moja la Nyumba za Wazee Sebleni baada ya kuungua moto ikiwemo ujenzi wa paa jipya, utiaji wa milango, madirisha, miundombinu ya maji, umeme na rangi. Hatua ya ujenzi wa ukuta wa Nyumba za Wazee Sebleni zimeanza kwa madhumuni ya kuwahifadhi na kuweka usalama wao. Naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefanya tathmini ya uwezo wa Idara ya Ustawi wa Jamii katika kutekeleza majukumu yake ya msingi. Ripoti ya zoezi hilo imebaini mapungufu katika maeneo ya Rasilimali Watu, Fedha na Utaalam na kutoa mapendekezo ya namna ya kuondoa mapungufu hayo. Wizara imeshatayarisha Mpango wa Utekelezaji kwa kuzingatia mapendekezo ya tathmini hiyo. Wizara pia ilitoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Idara ya Ustawi wa Jamii *(Para Social Workers)* ili kuimarisha utendaji wa kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inashughulikia fidia kwa wafanyakazi waliopatwa na ajali kazini. Katika kipindi cha Julai, 2010 – Machi, 2011 kesi 32 ziliripotiwa Unguja na Pemba ambapo kesi 28 zina thamani ya shilingi milioni thelathini na mbili, laki nne tisini elfu, mia tano arubaini na saba na senti hamsini na mbili (32,490,547.52/=). Wizara imefanya malipo kwa wafanyakazi kumi na tisa (19) walioumia kazini ambapo jumla ya shilingi milioni kumi na sita na hamsini elfu, (16,050,000/=) zilitumika Unguja na Pemba.

Aidha, jumla ya kesi sitini na tatu (63) za wafanyakazi serikalini zenye thamani ya shilingi milioni sitini na tano, laki nane sabiini na moja elfu, mia saba tisiini na tatu na senti thelathini na tano (65,871,793.35/=) zinahitaji malipo kwa Unguja na Pemba. (Angalia Kiambatanisho Nam. 4)

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imepokea maombi arubaini na tatu (43) ya msaada kutoka kwa wanafamilia wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Aidha, Wizara ilisaidia familia sitini na moja (61) kwa kuwapa shilingi elfu kumi na tano (15,000) kwa kila mwezi, hadi Juni, 2011 shilingi milioni kumi, laki nne, hamsini na tano elfu (10,455,000) zilitumika Unguja na shilingi laki tisa sitini elfu (960,000) Pemba. Vile vile, Wizara imezika jumla ya maiti thelathini (30) wasiokuwa na wenyewe kwa gharama ya shilingi 2,721,000/=. Maiti watano (5) Pemba na maiti ishirini na tano (25) Unguja. **(**Angalia Kiambatanisho 5a na 5b).

Mhe. Mwenyekiti, Ziara ya Mafunzo nchini Zambia ilifanyika ili kuangalia namna Zambia wanavyoshughulikia udhalilishaji wa kijinsia. Ziara hii ilipelekea uanzishwaji wa Kituo cha Majaribio cha Huduma za Pamoja yaani Mkono kwa Mkono *(One Stop Center)* kwa waathirika wa udhalilishwaji wa kijinsia kilichopo Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kituo kimezinduliwa rasmi tarehe 26/05/2011 na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Kituo kama hicho kipo katika mchakato wa kuanzishwa katika Hospitali ya Chake Chake Pemba na baadae kuanzishwa katika Hospitali zote za Wilaya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba wananchi kukitumia kikamilifu kituo hicho ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka kwa waathirika wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na wahusika wa vitendo hivyo wanatiwa hatiani. Aidha, natoa msisitizo kwa wadau wote wanaohusika kutoa huduma katika kituo hicho kufanya kazi zao ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Idara ya Ustawi wa Jamii imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kutoa misaada ya kiustawi kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi na watu walio katika makundi maalumu Unguja na Pemba.
2. Kuimarisha huduma kwa wazee.
3. Kutayarisha Sera ya Ustawi wa Jamii, miongozo na tafiti na kusimamia utekelezaji wake.
4. Kutoa elimu kwa jamii na wadau juu ya umuhimu na wajibu wao katika kuwatunza watoto, wazee na walio katika mazingira magumu zaidi.
5. Kuimarisha huduma kwa watoto wanaolelewa katika Vituo na Hifadhi ya Mtoto kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi milioni mia nne thelathini na nane (438,000,000/=) kwa kazi za kawaida na mishahara na shilingi milioni mia moja na hamsini (150,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Vijana ina jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli za Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii kwa Vijana.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara ya Maendeleo ya Vijana ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuendelea na hatua za Uundaji wa Baraza la Vijana Zanzibar.
2. Kuratibu na kusimamia Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa.
3. Kuendelea kuimarisha Uhusiano na Ushirikiano na Taasisi za Vijana Ndani na Nje ya Nchi pamoja na kuendeleza Kambi Kazi za Vijana Zanzibar.
4. Kuendeleza na kuimarisha vikundi vya Vijana vya Uzalishaji Mali kwa kutoa Mafunzo ya Uanzishaji na Uendelezaji wa *SACCOS*, Ujasiriamali, Uongozi na Utunzaji wa Hesabu.
5. Kuendeleza Mafunzo ya Mpango wa Kukuza Ajira kwa Vijana katika Sekta za Kilimo, Biashara na Utalii.
6. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Malezi kwa Vijana kwa kutoa Mafunzo ya Ushauri Nasaha, Stadi za Maisha, Afya ya Uzazi, Vita dhidi ya UKIMWI na Dawa za Kulevya.
7. Kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara katika kipindi cha mwaka 2010/2011 imeendelea na mchakato wa Uundaji wa Baraza la Vijana ambapo Rasimu ya Katiba ya Baraza imepitiwa na Wataalam na kufanyiwa masahihisho na sasa ipo katika hatua ya mwisho ya kupelekwa kwenye Vyombo vya Maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefanya tathmini ya Mbio za Mwenge wa Uhuru kwa mwaka uliopita na kufanya maandalizi ya mbio hizo kwa mwaka huu. Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja iliibuka kuwa Mshindi kwa Kanda ya Zanzibar. Jumla ya Miradi sabiini na saba (77) ya Zanzibar ilizinduliwa, kuwekewa mawe ya msingi na kufunguliwa ambapo Jumla ya Shilingi Milioni hamsini, Sitini na sita elfu na Mia tatu (50,066,300/) zilichangwa kupitia Wilaya zao kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo iliyopitiwa na Mwenge. (Angalia Kiambatisho Nam 6a na 6b).

Mhe. Mwenyekiti, Maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani yaliadhimishwa kwa kufanya Makongamano ya Vijana. Katika maadhimisho hayo vijana walibadilishana mawazo kuhusu Sera ya Maendeleo ya Vijana, Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki, Uundwaji wa Baraza la Taifa la Vijana la Zanzibar na kujadiliana changamoto wanazokabiliana nazo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na UVIKIUTA iliandaa Makambi Kazi kumi (10) ya Kimataifa ya kujitolea katika Wilaya ya Magharibi, Kati na Kusini ambapo jumla ya vijana 94 (Wanawake 52 na Wanaume 42) kutoka nchi mbali mbali za dunia walishiriki. (Angalia kiambatisho Nam. 7)

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanane (8) (wanaume 5 na wanawake 3) wa Zanzibar walishiriki Makambi Kazi ya kujitolea nchini Kenya na vijana 2, (mwanamke na mwanamme) walishiriki safari ya Japan katika Mpango wa Ubadilishanaji Vijana *(Youth Exchange Programme).*

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuanzisha Mfuko wa Kukopesha Vijana utakaoendeshwa na Benki ya *CRDB*. Jumla ya Shilingi Milioni Mia tatu zimeshatengwa kwa ajili ya kuanzisha mfuko huo na Vespa 3 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mfuko huo zimenunuliwa. Aidha, vikundi kumi 10 vitano (5) kutoka Unguja na vitano (5) kutoka Pemba vimepatiwa mafunzo ya uanzishaji na uendeshaji wa *SACCOS*, Ujasiriamali, Uongozi na Utunzaji wa Hesabu.
Mhe. Mwenyekiti, Wizara imekipatia vifaa vya uzalishaji na uhifadhi wa maziwa ya ng'ombe Kikundi cha Vijana JUWAPO - Fuoni vyenye thamani ya TSh. 5,440,000/-. Jengo la mradi wa JUWAPO limewekewa jiwe la msingi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein tarehe 13/06/2011. Vile vile, Wizara imewapatia mafunzo ya uendeshaji na upatikanaji wa soko wanawake 35 kutoka vikundi 10 vya Ujasiriamali vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Vijana unaoendeshwa na Shirika la *UN-HABITAT* na kugharamiwa na Serikali ya Norway chini ya uratibu wa Wizara umezinduliwa rasmi tarehe 20/02/2011 wenye lengo la kuwaendeleza vijana kiuchumi. Jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Arubaini na Tisa (149,000,000/-) zimetengwa kwa ajili ya Vijana wa Zanzibar watakaoweza kufikia masharti ya mfuko huo.

Wizara iliunda timu ya wataalam ambayo ilifanya utafiti kwa Vikundi vya Vijana vya Kiuchumi na Kijamii na kuweza kupata vikundi 26 vya Wilaya za Unguja na vikundi 34 vya Wilaya za Pemba ambavyo vimetimiza masharti na kutuma maombi**.** (Angalia Kiambatisho Nam. 8a na 8b).

Hadi sasa Shirika la *UN – HABITAT* linaendelea na mchakato wa kupitia maombi hayo ambapo matokeo ya waliofikia masharti ya kupata fedha hizo yatatolewa mwanzoni mwa mwezi wa Agosti, 2011.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ilifanya zoezi la kuwahamasisha vijana wa Mkoa wa Mjini Magharibi kupima afya zao kwa hiari ikiwa ni hatua ya kupunguza maambukizo mapya ya Virusi vya UKIMWI. Jumla ya Vijana mia tano na sabini na nne (574) walijitokeza, wanaume mia tatu na tisini na moja (391) na wanawake mia moja na themanini na tatu (183). Kati ya hao, vijana wawili (2) wa kiume walikutwa na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kupewa ushauri nasaha. Aidha, Wizara imetayarisha Muongozo wa Mafunzo ya Stadi za Maisha kwa Vijana.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefanya warsha kwa vijana 92 wa umri kati ya miaka 10 - 19 wa Unguja na Pemba ambao wamewahi kudhalilishwa kijinsia kwa lengo la kuwapa stadi za maisha ili waweze kujiamini na kutoa taaluma waliyoipata kwa vijana wenzao.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara iliandaa Shindano la Uandishi wa Miradi kwa vikundi 8 vya uzalishaji mali, Pemba. Washindi wa uandishi huo ni Kikundi cha Ufugaji Kupata si Nguvu cha Birikau Wesha ambacho kilibahatika kupata shilingi milioni kumi, laki saba arubaini elfu, mia nane hamsini na tano (10,740,855/=) na *Pemba SACCOS* ya Chake Chake kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa ulipata shilingi milioni kumi na nne, laki saba hamsini na mbili elfu, mia moja na ishirini na tano (14,752,125/=).

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Idara ya Maendeleo ya Vijana imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kukuza uwezo wa kiutendaji wa Idara.
2. Kukamilisha Uundaji wa Baraza la Vijana Zanzibar.
3. Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa.
4. Kuendeleza na Kuimarisha Vikundi vya Vijana vya Uzalishaji Mali kwa Kutoa Mafunzo ya Uanzishaji na Uendelezaji wa *SACCOS*, Ujasiriamali, Uongozi na Utunzaji wa Hesabu.
5. Kutayarisha Mpango wa Maendeleo ya Vijana.
6. Kufanya Mapitio ya Sera ya Vijana.
7. Kujenga Uwezo wa Vijana kupitia Stadi za Maisha, Vita dhidi ya Ukimwi na Dawa za Kulevya.
8. Kuendeleza Mashirikiano na Uhusiano wa Taasisi za Vijana Ndani na Nje ya Nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Vijana ili iweze kutekeleza malengo yake ya mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Nne (114,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara na Shilingi Milioni Ishirini (20,000,000/**=)** kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Haki za Wanawake na Watoto ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria, Programu na Mikataba ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ilijipangia kutekeleza Malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia na kulinda Haki za Wanawake na Watoto pamoja na kushajihisha jamii kuziheshimu.

2. Kuinua hali za wanawake kiuchumi kwa kuwapatia ushauri na mafunzo.

3. Kuendelea na utayarishaji wa Sheria ya Mtoto.

4. Kuimarisha mashirikiano ya Kitaifa na Kimataifa katika kuhakikisha kuwa Haki za Wanawake na Watoto zinalindwa.

5. Kutoa Mafunzo kuhusu Sera ya Hifadhi na Maendeleo ya Wanawake na Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Watoto kwa Waratibu wa Maendeleo ya Wanawake na Watoto wa Shehia.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imeendesha mafunzo ya Haki na Wajibu wa Mtoto kwa Wajumbe wa Mabaraza ya Watoto. Aidha, Wizara imeandaa rasimu ya kwanza ya Mfumo wa Kukusanya Taarifa za Watoto kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Vile vile, mtoto mmoja ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Watoto alishiriki kikao cha Baraza Kuu la Watoto nchini Rwanda. Lengo ni kupata uzoefu wa shughuli za uendeshaji wa Mabaraza ya Watoto nchini humo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuhakikisha wanawake wanaendelezwa kiuchumi, Wizara imeanza hatua ya kukusanya taarifa za Vikundi vya Wanawake katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Taarifa za vikundi hivyo zitaisaidia Wizara kupanga mikakati madhubuti ya kuviinua vikundi hivyo na hali ya wanawake kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yalifanyika Kitaifa kwa Kongamano katika Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja na Chake Chake Pemba ambapo ujumbe wa mwaka huu ulikuwa “Usawa katika Upatikanaji wa Elimu na Mafunzo ya Sayansi na Teknolojia Huwapelekea Wanawake Kupata Kazi zenye Heshima” na Wilaya ya Kaskazini “B” ilifanya Maandamano ya kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ujumbe ulikuwa “Vitendo vya Udhalilishaji wa Kijinsia sasa basi**.”**

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imefanya Mafunzo ya Ujasiriamali kwa Vikundi vya Wanawake kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba. Jumla ya vikundi sita (6) kutoka Unguja na vinne (4) kutoka Pemba vilipatiwa mafunzo hayo.

Aidha, jumla ya vikundi kumi na tano (15) vya Ujasiriamali vimepatiwa mafunzo ya Biashara na Mpango wa Masoko kwa Wilaya zote za Pemba na jumla ya vikundi mia moja na tisa (109) vya Ujasiriamali vimetembelewa (Unguja 20 na Pemba 89) kwa tathmini na uelekezi. Wizara, pia imewajengea uwezo Waratibu wa Wanawake na Watoto ishirini (20) wa Shehia za Pemba na Waratibu na Masheha wa Shehia zote za Unguja. **(**Angalia Kiambatisho nam. 9a na 9b).

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia mafunzo hayo, *Tujuane SACCOS* ya Konde imeimarika na ina mpango wa kuanzisha Benki yao ya Wanawake. Jumla ya Wanawake 78 wamejiunga na *SACCOS* hiyo ambayo ilianzishwa kwa mtaji wa shilingi milioni nne na laki mbili (4,200,000/=). Benki ya *CRDB* wamewasaidia shilingi 1,300,000 kwa ajili ya utengenezaji wa jengo na kuwapa mafunzo ya kompyuta. Hadi sasa *SACCOS* hiyo ina mtaji wa shilingi milioni kumi na nane na laki tatu (18,300,000/=). Nawapongeza sana wanawake wa Konde.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imewasilisha Mswada wa Sheria ya Mtoto ya Zanzibar na kupitishwa na Baraza lako Tukufu hivi karibuni. Sheria hii imezingatia upatikanaji wa haki, fursa na ulinzi wa watoto kupitia taasisi husika na jamii kwa jumla. Wizara pia imekamilisha kazi ya kukusanya taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto *(CRC)*, taarifa hiyo itajumuishwa na Taarifa ya Wizara inayoshughulikia Watoto ya SMT kwa ajili ya kuwasilishwa Umoja wa Mataifa Januari, 2012. Vile vile, Wizara imeandaa taarifa ya utekelezaji wa Haki za Mtoto ambayo imewasilishwa katika Baraza lako Tukufu katika kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea na kazi ya kukusanya taarifa za Udhalilishaji wa Watoto kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba. Kumalizika kwa kazi hiyo kutatoa taswira halisi ya masuala ya Udhalilishaji wa Watoto nchini. Wizara pia, imechapisha kitini kitakachotumika katika kutoa mafunzo ya kuwasilisha Ujumbe wa Haki za Watoto kwa Watendaji wa shughuli za Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu na Kusimamia Haki za Wanawake na Watoto.
2. Kuratibu utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Zanzibar.
3. Kuhakikisha kwamba Mabaraza ya Watoto yanafanya kazi katika Wilaya zote.
4. Kuwainua Wanawake kiuchumi pamoja na kuanzisha Benki ya Wanawake.
5. Kuimarisha Mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa katika kuhakikisha kuwa Haki za Wanawake na Watoto zinalindwa.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Sita (116,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara na Shilingi Milioni Thelathini (30,000,000/=) kwa kazi za maendeleo.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba inasimamia shughuli zote za Wizara na kutekeleza malengo ya Idara zote za Wizara iliyojipangia kwa upande wa Pemba. Utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2010/2011 na malengo ya Ofisi kwa mwaka 2011/2012 tayari yameshaelezwa katika utekelezaji wa kila Idara ambazo zinahusisha na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ukosefu wa Jengo la Ofisi Kuu Pemba, Wizara imefanikiwa kupata kiwanja katika eneo la Tibirinzi. Ujenzi wa Ofisi hiyo unasimamiwa na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Kutokana na tatizo hili Serikali imeamua kukodi jengo kwa muda kwa ajili ya Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Ofisi Kuu Pemba kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi milioni mia tatu na mbili (302,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilitengewa jumla ya shilingi bilioni tatu, milioni mia sita arubaini na sita na tisiini elfu (3,646,090,000/=) kwa kazi za maendeleo ambapo shilingi milioni mia moja na hamsini (150,000,000/=) ni mchango wa Serikali na bilioni tatu, laki nne tisiini na sita na tisiini elfu (3,496,090,000/=) ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo. Fedha zilizotolewa na Serikali kwa kazi hizo mpaka kufikia Juni, 2011 ni Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini (150,000,000/=) ambazo ni sawa na asilimia 100 ambapo fedha zilizotolewa na Washirika wa Maendeleo ni Shilingi Bilioni Moja Milioni Themanini na Mbili Laki mbili na tisini na Nane Elfu Mia Nane na Kumi na Tisa (1,082,298,819/=) sawa na asilimia 31%. Kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011, Makadirio ya matumizi ya kazi za kawaida yalikuwa ni Bilioni Moja, Milioni Mia tatu thelathini na mbili, Laki nane sitini elfu Mia nane hamsini na tatu (1,132,860,853/=). Hadi kufikia Juni 2011, fedha zilizotolewa ni Shilingi bilioni Moja Milioni Mia Moja na kumi Laki nane sabiini na moja elfu Mia moja na kumi na mbili, (1,110,871,112/=) ambayo ni sawa na asilimia 98%**.** (Angalia Kiambatisho Nam. 10a na 10b).

Mhe. Mwenyekiti, Wizara pia ilipata fedha za Amana (*Deposit Account*) Jumla ya Shilingi Milioni Mia mbili kumi na tisa, laki nne na arubaini elfu(219,440,000/=) kwa kazi za ujenzi wa Ukuta na Ukarabati wa Nyumba za Wazee Sebleni. Nawapongeza sana wazee.

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuzishukuru Nchi, Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zilishirikiana na Wizara katika kutekeleza majukumu yake. Nchi hizo ni kama zifuatazo; **India, Japan, Norway, Marekani, Uingereza na Jamhuri ya Watu wa China.** Mashirika ya Kimataifa ni**; ILO, UNDP, UNFPA, UNICEF, SAVE THE CHILDREN, FHI, Tunajali Program, CHAI, UNESCO, ADB, USAID, DANIDA, DFID, UN HABITAT na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.** Mashirika ya kiserikali: **Zanzibar Road Funds, BOT, PBZ, CRDB, AKIBA BANK na POSTAL BANK.**

Taasisi zisizokuwa za kiserikali ni; ***ZAYADESA, Modesty Tours and Safari Limited, ZACA, ZAIADA, PEMBA PRESS CLUB, ZAFELA, ZAMWASO, ZANGOC, ZLSC, COWPZ, PIRO,*** **UVIKIUTA,** ***WEDTF, TAWLA, TAMWA, CHANGAMOTO, PRIDE, TGNP, UWT*****,** **ZANZIBAR** ***GENDER COALITION*** na nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuwashukuru sana Waandishi wa Habari kupitia Vyombo vyao vikiwemo Televisheni, Redio na Magazeti ambavyo vimefanya kazi kubwa ya kuhamasisha na kuelimisha jamii juu ya shughuli zinazotekelezwa na Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, Aidha, naomba kuwashukuru Wafanyakazi wote wa Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto chini ya Uongozi wa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi, kwa kufanya kazi kwa juhudi kulikoniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara kwa ufanisi mkubwa. Nawaomba wazidishe juhudi zaidi katika kutekeleza malengo ya mwaka huu ili tuwaletee maendeleo endelevu Wanawake, Watoto, Vijana, Wazee na Jamii kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein, Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi nawatakia wote afya njema na maisha marefu ili watuongoze na kutuletea maendeleo Wazanzibari wote.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za pekee kwako kwa jinsi unavyoliendesha Baraza lako tukufu kwa busara na kunipa mimi nafasi ya kuwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Ninakuombea kila la kheri, afya njema na mafanikio katika kazi zako.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wapokee, wajadili, watupe ushauri na maelekezo, hatimae kupitisha makadirio ya matumizi na kuidhinisha jumla ya Shilingi bilioni moja, milioni mia tano na arubaini (1,540,000,000/=) ikiwa ni fedha za kazi za kawaida na Mishahara, Shilingi Milioni mia mbili thelathini (230,000,000/=) zikiwa ni fedha za kazi za Maendeleo na Shilingi Milioni tisa na mbili, laki Tano hamsini na Moja elfu (902,551,000/=) ikiwa ni Mchango wa Wahisani kwa kipindi cha mwaka 2011/2012. (Angalia Kiambatisho Nam 11).

Mhe.Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: (Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Wanawake): Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwako wewe Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya kamati yangu juu ya Bajeti ya Wizara ya Ustawi wa jamii Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto.

Mhe Mwenyekiti, Shukurani zangu za dhati ziwaendee wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kwa kuniamini na kunipa jukumu hili la kuwasilisha maoni ya Kamati yetu kwa niaba yao wajumbe wenyewe ni kama wafuatao:-

1.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mwenyekiti
2.Mhe. Hija Hassan Hija	Mkamo/Mwenyekiti
3.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
4.Mhe. Ashura Ali Sharifu	Mjumbe
5.Mhe. Asha Abdu Haji	Mjumbe
6.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
7.Mhe. Saleh Nassor Juma	Mjumbe
8.Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
9.Ndg Shemsa Maabad Mohamed	Katibu
10Ndg Talib Enzi Talib	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa pongezi za dhati kwa Wizara kwa kuanzishwa kituo cha (*One Stope Center*) au mkono kwa mkono ambacho kina shughulikia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia, kilichopo hapa Unguja katika Hospitali ya

Manazi Mmoja. Pongezi zetu za dhati pia ziwaendee washirika wetu wa maendeleo Shirika la Save the Children kwa kutoa msaada mkubwa kwa kuanzishwa kwa kituo hicho.

Mhe. Mwenyekiti, ni imani yetu kuwa zile takwimu za zamani ambazo zinazoonyesha kuwa katika mwaka 2010 jumla ya kesi zilizoripotiwa ni 71, kesi zilizopelekwa Mahakamani ni 64, wahusika walioshitakiwa ni 2, kesi zilizofungwa na Polisi 10 na kile cha kusikitisha zaidi ni kuwa hakuna muhusika hata mmoja aliyehukumiwa na kupewa adhabu yeyote.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii mara nyingi tunaambiwa inatokana na kutopatikana kwa ushahidi wa kutosha wa kuweza kumtia hatiani mshitakiwa. Kutokana na kuanzishwa kwa kituo hicho cha mkono kwa mkono tunaamini kuwa kutakuwa na uwezekano mkubwa wa kupatikana kwa ushahidi pindi matokeo ya udhalililshaji na ubakaji yakifanyika. Tunaiomba Serikali kufanya juhudi za kukipatia kila aina ya msaada na nyenzo zinazohitaji ili kukiwezesha kufanya kazi zake vizuri na tunaamini kila mmoja katika kituo hicho atafanya kazi yake ipasavyo ili kulinda maslahi bora ya mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuwa kimezinduliwa kituo tunaiomba wizara kufanya juhudi za makusudi ya kukitangaza kituo hicho kwani watu wengi hawajaelewa uwepo wa kituo hicho na huduma zinazopatikana hivyo elimu zaidi inahitajika katika jamii ili kukiwezesha kituo hicho kiweze kufahamika vizuri zaidi na pia wale watakaobainika kutenda vitendo hivyo basi adhabu kali zichukuliwe na kutanganzwa ili iwe fundisho kwa wengi na pia kuweza kudhibiti vitendo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa vitendo vya udhalilishaji ubakaji wa watoto vinafanyika sana katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kuliko mikoa mingine, hivyo sisi tunajiuliza, kwa nini vitendo hivyo vitokee katika Mkoa huo zaidi na kwa sababu zipi? au kuwa Mkoa huo kuna Watoto wengi? au watoto wengi waliopo katika Mkoa huo wapo katika mazingira hatarishi? au kuna vitu vinavyowashawishi wabakaji na kupata fursa ya kutenda vitendo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, masuala haya yote yanahitaji majibu yake na majibu yake yatapatikana pindi tukiwa wabunifu wa kuweza kufanya utafiti na kujua chanzo na sababu ya kadhia hii. Hivyo tunaiagiza Wizara kufanya utafiti wa kina ili tuweze kuwa na majibu ya uhakika ya maswali yote hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoelewa kuwa Zanzibar tukiwa kama ni nchi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama zilivyo nchi nyengine tumekubali na kuridhia Mkataba wa Afrika wa Haki za Ustawi wa Watoto wa mwaka 1999 tarehe 16 Machi, 2003. Hata hivyo bado hatujaweza kuvitekeleza

baadhi ya vipengele katika Mkataba huo. Mfano mzuri katika kipengele cha 16 kinachotaka haki ya kulindwa kwa watoto dhidi ya kuumizwa au kutendewa vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, watoto waliohukumiwa na kuwekwa katika vyuo vya mafunzo pamoja na watu wazima wanaendelea kutumiwa vibaya na kudhalilishwa, Kamati yangu inaiomba sana serikali kuwatenganisha watoto hao na watu wazima katika sehemu hizo, Mchanganyiko wa watu wazima na watoto unapelekea watoto hao kupata athari ya kisaikolojia na mara tu wanapomaliza kifungo na kuingia katika jamii wanageuka na kuwa majambazi, sugu au wahalifu wazoefu badala ya kuwa watoto wema.

Mhe. Mwenyekiti, Aidha, katika vituo vya polisi tulivyonavyo pamoja na Mahkama zimekuwa zikiendesha mashauri ama kesi zinayowahusu watoto katika sehemu zile zile ambazo watu wazima nao wanapelekwa na kusikilizwa mashauri yao. Utaratibu huu pia unawajenga watoto kuwa masugu zaidi na kuathirika kisaikolojia na kuzowea katika vituo vya polisi na mahkama na kupaona sawa na nyumbani. Kuna haja kuandaliwa mazingira ya kuwepo mahala maalum kwa ajili ya vituo vya mafunzo vya watoto watukutu.

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuwakinga watoto wasifanye makosa, hilo ni jambo la kawaida hata hivyo tunaweza kuwanusuru watoto hao wanaofanya makosa wasipate athari za kisaikolojia. Tunaishauri Serikali kuwatengea Mabaraza ya usuluhishi watoto ili kuweza kusaidia kutatua migogoro yao.

Mhe. Mwenyekiti, katika kufanya juhudi za kuwakomboa wanawake kiuchumi *SACCOS* ya Konde imeweza kuanzisha Benki ya wanawake ambapo jumla ya wanawake 78 wameweza kujiunga na Benki hiyo. Benki hiyo imeanzishwa kwa mtaji wa shilingi milioni nne na lake mbili Jambo hili ni zuri sana na la kupongezwa. Tunaishauri Wizara kuwashajiisha kinamama katika sehemu nyengine waweze kuanzisha Benki hizo katika maeneo mengi zaidi hasa sehemu za Vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, huu ni mwanzo mzuri na pia ni mfano wa kuigwa na ni matarajio yetu kuwa vikundi vyengine vilivyobaki ambavyo vinamitaji mikubwa au midogo, vitahamasishwa na kuviandalia mipango mizuri ili na wao waweze kujikusanya na kufungua benki zao, hasa wale kina mama walioko katika sehemu za ukanda wa pwani ambao wanajishughulisha na ulimaji wa mwani na wale mama ntilie

Mhe. Mwenyekiti, suala la kuwepo kwa Mabaraza ya Watoto ni muhimu kwa lengo la kujitambua wao wenyewe na kujua haki zao na kutoa taaluma ya haki hizo kwa wenzao ndani ya jamii. Mabaraza haya yanasaidia kutoa elimu na kuwajengea uwezo watoto katika kuendesha mambo yao.

Mhe. Mwenyekiti, hali ilivyo hivi sasa inaonyesha kuwa uwakilishi katika Mabaraza hayo ni finyu na upo katika maeneo ya mjini zaidi kuliko vijijini, ambapo kuna idadi kubwa ya watoto ukilinganisha na mjini. Ni vyema ikiwa mabaraza haya yakagawa kwa kila Wilaya au ki majimbo na wajumbe wa Baraza lako tukufu wapewe fursa ya kuyatambua mabaraza hayo ili kufanya kazi pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inapongeza Shirika la *UN-HABITAT* kwa kuanzisha mfuko wa msaada kwa vijana ambapo lengo lake ni kuwaendeleza vijana kiuchumi. Jumla ya shilingi 149,000,000/ zimetengwa kwa ajili ya vijana ambao wataweza kufikia masharti ya kupewa mkopo. Jambo la kuzingatiwa zaidi hapa ni kuwa vijana wengi bado hawajapata elimu ya kutosha ya ujasiriamali ambayo itawawezesha kuitumia mikopo hiyo na kujikwamua kiuchumi. Tunaishauri Wizara kuvipatia mafunzo vikundi vya ujasiriamali vya vijana hao ambao watakaoweza kufikia masharti ya mikopo hiyo kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametueleza kuwa wameanza kutayarisha sera ya hifadhi ya jamii ambayo itatoa miongozo ya hifadhi ya jamii ya makundi yote ikiwemo wazee na watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati umefika kwa wizara husika kuharakisha kukamilika kwa sera hiyo ili iweze kufikishwa mbele ya Baraza lako kwa kujadiliwa na hatimae baadae kuweza kuwa na muongoza mzuri wa kuwa na sheria kamili itakayosimamia uhifadhi wa jamii. Watoto wengi wameonekana kuwa na mazingira hatarishi na hata watu wazima wamekuwa wakihangaika katika mitaa, na omba omba wanaongezeka kila kukicha. Hivyo kuwepo kwa sheria hiyo kutasaidia kuwa na hifadhi ya jamii iliyo rasmi na inayofahamika.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho, Kamati yangu imefurahishwa sana na adhma ya serikali ya kuwaongezea posho la kujikimu kimaisha wazee wetu kutoka shilingi 25,000 hadi shilingi 40,000. Kamati yangu inasema si haba *Alhamdulillah*. Ila tunaikumbusha serikali kupitia wizara husika kuyaangalia makaazi ya wazee kule Pemba, ili na wao waweze kuishi katika mazingira mazuri. Kamati yetu haijaridhika na nyumba ya makaazi ya wazee huko Pemba.
Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa leo ni siku ya Jumapili na kwa kuwa Mhe. Waziri amewasilisha hotuba yake na kwa kuwa Mwenyekiti wa kamati husika naye amewalisha hotuba yake. Kwa hivyo, naomba niliombe Baraza lako liridhie tuliahirishe Baraza letu mpaka siku ya Jumatatu ya tarehe 25/07/2011 saa 3:00.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana. Kwa hivyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe nawaulize. Walewalioikubali hoja ya Mhe. Waziri wanyanyuwe mikono juu. Waliyoikataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa Wajumbe, ahsanteni sana kwa utulivu wenu. Kidogo nilikuwa nataka kutoa taarifa kwamba kesho tarehe 25/07/2011 saa 3:00 asubuhi tutakaporudi hapa kwa ajili ya kutoa michango yetu, tutaanza na Mhe. Asha Bakar Makame, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Mhe. Subeit Khamis Faki na Mhe. Hija Hassan Hija.

Kwa hivyo, tunawaomba hawa wajumbe wafike mapema tukijaaliwa kesho saa 3:00. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe.

(Saa 7.45 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 25/07/2011 saa 3:00)